

10 NOVEMBA, 2022

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Tisa – Tarehe 10 Novemba, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali.

Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, sasa Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 127

**Kuongeza mkopo kwa akina mama
wajasiriamali – Katavi**

MHE. MARTHA F. MARIKI aliuliza:-

10 NOVEMBA, 2022

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaongezea mkopo akina mama wajasiriamali wa Mkoa wa Katavi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Mkoa wa Katavi zimekuwa zikitoa mikopo ya uwezesaji kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kuzingatia sheria na kanuni za utoaji mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri za Mkoa wa Katavi zilitoa jumla ya mikopo ya Shilingi milioni 980 sawa na asilimia 105 kwa vikundi 124 vyenye jumla ya wanufaika 850. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 halmashauri za mkoa huo zimepanga kutoa mikopo hiyo yenye jumla ya Shilingi bilioni 1.45 sawa na ongezeko la kiasi cha Shilingi milioni 470.

Mheshimiwa Spika, halmashauri zitaendelea kuongeza kiwango cha mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kulingana na ongezeko la makusanyo ya mapato ya ndani. Ahsante sana.

10 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Martha Mariki, swali la nyongeza.

MHE. MARTHA F. MARIKI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza, naishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini ripoti ya CAG mwaka 2020/2021 imeonesha kwamba fedha hizi zimekuwa nyingi zikipotea kutokana na kutorejeshwa ipasavyo: Je, Serikali inatoa tamko gani kuhakikisha fedha hizi zinarejeshwa ili ziweze kuwanufaisha wanufaika wengine?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika mwaka wa fedha 2020/2021 na miaka ya fedha ya nyuma ya mwaka wa fedha huo, kulikuwa na kasi ndogo ya urejeshaji wa fedha za mikopo ya asilimia 10, na Serikali ilitambua changamoto hiyo, tukachukua hatua; kwanza, kwa kuongeza usimamizi na uratibu wa mikopo pamoja na marejesho ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, nilijulishe Bunge lako Tukufu sasa kwamba mwenendo wa marejesho wa fedha hizi kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 umeongezeka kwa takribani asilimia 84 sasa ikilinganishwa na miaka nyuma ambayo ilikuwa chini ya asilimia 50. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha tunaendelea kusimamia marejesho ya fedha hizi ili mfuko huu uendelee kuzunguka kunufaisha vikundi vingine.

Mheshimiwa Spika, nitoe tamko kwamba Wakurugenzi wa halmashauri zote kote nchini wahakikishe wanakopesha asilimia 10 kwa makundi yale kadri ya sheria, na wahakikishe wanarejesha fedha zile ili ziendelee kuwanufaisha wananchi wengine. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, swali la nyongeza.

MHE. NOAH L. S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa kuna kundi kubwa la watu ambao sio vijana, wenye umri wa miaka ya 35 hadi 45, wanaachwa sana na ni changamoto kwenye ajira, na bado wapo kwenye kundi la kuajiriwa na Serikali kwa maana hawajafikia ukomo.

Je, ni lini Serikali sasa itarekebisha hiyo sera au itatoa tamko kwamba sasa nao wale watu wapewe mikopo kupitia hiyo asilimia kumi, au kuongeza asilimia 10 ili kupunguza hili wimbi la ukosefu wa ajira? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mikopo hii inatolewa kwa vijana ambao wana umri wa miaka 18 hadi 35 kwa mujibu wa definition ya vijana kwa utaratibu huu wa mikopo ya *ten percent*. Ni kweli kwamba kuna vijana ambao wana umri wa zaidi ya umri wa miaka 35 ambao pia wangeweza kunufaika na mikopo hii. Kwa hiyo, naomba niichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge tukaifanyie kazi na kuona uwezekano huo na pia kuona kama inaweza ikatekelezwa ama vinginevyo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimwa Fakharia Shomar Khamis, swali la nyongeza.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Halmashauri za SMT ndiyo zinasimamia mikopo kwa ajili ya vijana, akina mama na walemavu; na kwa upande wa Zanzibar vilevile Halmashauri za SMZ zinasimamia hivyo hivyo:-

Je, Mheshimiwa Waziri kwa sababu halmashauri za bara tayari zinafanya kazi hiyo, lakini halmashauri ya Zanzibar kisheria zinatakiwa nazo zifanye kazi hiyo; utazisaidia vipi ili halmashauri zile ziweze kuwasaidia akina mama nao waweze kujikwamua katika maisha?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la

10 NOVEMBA, 2022

nyongeza la Mheshimiwa Fakharia Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa mikopo ya asilimia 10 kwa maana ya Tanzania Bara, unasimamiwa na halmashauri; na kama ambavyo amesema Mheshimiwa Mbunge kwamba Zanzibar pia inatakiwa isimamiwe na halmashauri lakini kuna changamoto.

Mheshimiwa Spika, naomba kama Serikali tuchukue hoja hiyo ili tuweze kukaa pamoja tuone namna gani tunaweza tukaboresha kwa upande wa Zanzibar pia ili huduma hiyo iweze kuimarika. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa ulize swali lake.

Na. 128

Ajira kwa wahitimu wa kada ya mazingira

MHE. ASIA A. HALAMGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaajiri wahitimu wa kada ya mazingira waliomaliza katika vyuo vikuu nchini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Deo Ndejembu, majibu.

10 NOVEMBA, 2022

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA
UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha wahitimu wa kada ya Mazingira na kada ya Afya ya Mazingira (*Environmental Health Officers*) wanaajiriwa ili kuimarisha jitihada za kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali ilitoa jumla ya vibali vya ajira 223 kwa kada ya Mazingira katika taasisi zipatazo 124 ambapo utekelezaji wa ajira hizo unaendelea. Aidha, katika mwaka huu wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga nafasi 73 za ajira kwa Wataalam wa Mazingira kwa ajili ya taasisi za Serikali zikiwemo Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hatua za utekelezaji wa ajira hizi zote zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka huu wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, jitihada hizi ni endelevu kutokana na umuhimu wa suala la utunzaji wa mazingira ikiwa ni miongoni mwa mikakati ya nchi na dunia kwa ujumla ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

SPIKA: Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

10 NOVEMBA, 2022

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kuweka mazingira mazuri ya kuweza kuwavutia wawekezaji.

Je, nini mpango wa Serikali katika kuajiri watumishi wa kada ya mazingira katika miradi yote mikubwa ambayo inatekelezwa na Serikali?

Swali langu la pili; je, kwa kuwa nchi yetu kwa sasa inakabiliwa na changamoto ya tabia nchi, kwa mwaka huu wa fedha, Serikali imepanga ajira ngapi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Asia Halamga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa amekuwa hodari sana kufuatilia masuala mbalimbali ya ajira za kada mbalimbali ambazo zinahusu mkoa wake na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la kwanza la je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri watu kwenye miradi hii mikubwa; Niseme tu kwamba Serikali inaajiri kwa kuzingatia ukomo wa bajeti kama ambavyo inaidhinishwa na Bunge lako hili Tukufu. Kwa hiyo, tutaendelea kuzitenga kwenye bajeti na kuleta hapa Bungeni kuona namna gani nafasi hizi zitaongezwa.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili:Je, Serikali ilitenga jumla ya ajira ngapi? Kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga jumla ya ajira 30,000 kwa kada zote na taasisi mbalimbali za Serikali nchini na hiyo pia kama nilivyojibu katika jibu langu la nyongeza la kwanza kwamba ni kutokana ukomo wa bajeti ambao tulipatiwa. Hata hivyo tutaendelea kutenga na kuona namna gani tunaweza kuangalia hizi kada zote zikapata watumishi wa kutosha.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, kwenye jibu lako unasema ajira ambazo Serikali ilitoa vibali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ajira 223 utekelezaji bado unaendelea. Ni kwamba wale waombaji hakuna, au yaani mwaka ule uliopita kipindi kile mpaka sasa hivi bado mnaendelea au kuna changamoto kwenye sekretarieti ya ajira?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, Hapana, siyo kwamba kuna changamoto kwenye sekretarieti ya ajira, lakini hizi nafasi zote 223 zinatokana na taasisi mbalimbali za Serikali. Kwa hiyo, sekretarieti ya ajira inaanza mchakato pale tu zile taasisi zilizoidhinishiwa vibali vyao vya kuajiri zinapoanza mchakato wao kupeleka sekretarieti ya ajira. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareso, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

10 NOVEMBA, 2022

Na. 129

**Hitaji la masoko ya vitunguu maji kwa wakulima
wa Bonde la Eyasi**

MHE. CECILIA D. PARESSO aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali kwa wakulima wa vitunguu maji katika Bonde la Eyasi juu ya upatikanaji wa masoko pamoja na bei ya zao hilo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA
BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhakikisha mazao yanayozalishwa nchini yanapata soko la uhakika, na kuwa mkulima anapata bei nzuri na kunufaika.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Idara ya Maendeleo ya Biashara na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (*TanTrade*) inaendelea kutafuta masoko ya uhakika ya zao la vitunguu maji vinavyolimwa hapa nchini, ikiwa ni pamoja na vitunguu kutoka Bonde la Eyasi ili kupata bei nzuri itakayo wanufaisha wakulima wa zao hilo hapa nchini. Nakushukuru.

10 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja na soko kutokuwa na uhakika, kumeibuka utamaduni wa wanunuzi kufika mpaka mashambani, wao ndio wanapanga bei na aina ya vifungashio ambapo kwa kiwango kikubwa inamuumiza mkulima.

Je, Serikali inasema nini kuhusiana na hili?

Swali la pili, je, Wizara ipo tayari sasa kwenda kukaa na wakulima hawa kusikiliza changamoto zao lukuki walizonazo ili waweze kupata ahueni na kuondokana na changamoto hiyo? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Paresso kwa kufuatilia hili la mazao hasa kwenye zao la vitunguu. Ni kweli kumekuwa na changamoto hiyo ya wanunuzi wengi na wakati mwingine hata wa nje kufika kwa wakulima kule vijijini. Tumeshatoa maelekezo mara nyingi hasa kwa wenzetu wa halmashauri tuendeleo kushirikiana kuhakikisha tunaendelea kujenga *collection centers*, yaani maeneo

10 NOVEMBA, 2022

ya kuuzia kama masoko. Maeneo hayo ndiyo maalum kwa wakulima ili waweze kuuza kwa tija na kwa vipimo.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kusema kwamba Wakala wa Vipimo ambao wako chini yetu waendeleo na waende eneo hili maalum wakaone changamoto hii iliyopo ili kukomesha ufungashaji wa mazao yetu kwa njia ambayo siyo sahihi. Maana tumeelekeza mazao yote yauzwe kwa vipimo, siyo kwa vifungashio. Pia kulikuwa na hii habari ya lumbesa, naamini tulishasema na ninarudia tena, kuhakikisha wanauzi kwa vipimo na tuhamasishe halmashauri waweke *collection centers* ili wakulima wapate bei yenye tija kwa mazao yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwenda kukagua; nitaenda, na niagize WMA waende kwanza, nasi tutaenda kuona changamoto hasa katika eneo hili Bonde la Eyasi ili tuweze kutatua changamoto hii ambayo nadhani ni sehemu zote nchini na tunaendelea kufanyia kazi hilo. Nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri, kumekuwa kuna shida sana ya masoko kama alivyosema kwenye swali la msingi, lakini kumekuwa na matangazo ya uwongo redio wakisema zao la *vanilla* linauzwa kwa kilo moja Shilingi milioni moja: Unatoa katazo gani kwa watu wanaowadanganya wakulima katika zao hili? (*Kicheko*)

10 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na matangazo ambayo wakati mwingine yanaleta taharuki na hasa kwenye hili zao la *vanilla* kwamba linauzwa bei kubwa na wakati mwingine nadhani hii imekuwa kama zile biashara za kwenye mitandao. Kwa sababu hiyo, Serikali na kwenye maeneo mahususi kwa mfano maeneo ya Njombe, kumeshatokea utapeli huo.

Mheshimiwa Spika, tumeshaelekeza wenzetu kwenye halmashauri waone namna gani kweli hawa ambao wanadhani wanataka kusaidia wakulima, washirikiane na halmashauri kuona kweli hilo zao kama ni *vanilla* au mazao mengine kweli yanaweza kustahili kulimwa lakini pia kuwa na njia sahihi kuhamasisha ulimaji huo badala ya kuwa na biashara mtandaoni ambazo mara nyingi ni utapeli.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme, kwa kweli sisi kama Serikali tunaendelea kufuatilia matapeli wanaotumia biashara mtandao kutapeli wakulima au wananchi kutoa fedha ambazo mwisho wa siku haziwezi kuwa na tija kama ambavyo wamelenga. Nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Konde, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa.

10 NOVEMBA, 2022

Na. 130

TBS na ZBS kufanya kazi kwa ushirikiano

MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA K.n.y. MHE. MOHAMED SAID ISSA aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha TBS na ZBS zinafanya kazi kwa ushirikiano?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Jimbo la Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) wana hati ya makubaliano (*Memorandum of Understanding*) iliyosainiwa Mei, 2015 kwa kipindi cha miaka mitano na pia imehuishwa tena mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, katika makubaliano haya yanajikita katika maeneo yafuatayo:-

- (i) Uandaaji wa viwango vya Kitaifa;
- (ii) Udhhibiti wa ubora na usalama wa bidhaa;
- (iii) Huduma za metrolojia na upimaji;
- (iv) Mafunzo ya kitaalam kwa maafisa wa ZBS; na
- (v) Kutambua bidhaa zilizothibitishwa ubora baina ya mashirika haya mawili.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, swali la nyongeza.

MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kwa niaba ya Mheshimiwa Mohamed Said Issa.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, utekelezaji wa makubaliano hayo umefikiwa kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali ipo tayari leo kutoa tamko kuwa bidhaa zilizotambuliwa na moja katika mashirika mawili hayo hutumika nchi nzima bila ya utambuzi wa Shirika lingine lolote nchini? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, samahani swali la pili sijasikia vizuri.

SPIKA: Swali la pili, anataka kujua kama bidhaa zilizotambuliwa na TBS zitauzwa Zanzibar na bidhaa zilizotambuliwa na ZBS zitauzwa Bara bila utambuzi tena mwingine wa chombo kingine.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khalifa Issa Mohamed, kama ifuatavyo:-

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa makubaliano haya umeshaanza na unaendelea kama nilivyosema kwenye maeneo yale yote matano kwa maana viwango vile tunavyokubaliana vinatekelezwa, lakini pia na bidhaa zote zinatambuliwa katika pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la pili, ndio hii moja ya vitu ambavyo tumesisitiza katika sehemu ya tano, kwamba lazima bidhaa zote ambazo zimethibitishwa na ZBS au na TBS kwa upande wa Bara zinatambuliwa katika pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, hii si kwa Tanzania tu ni kwa Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki kwamba hata ukienda kwenye bidhaa ambazo zimetoka kwenye nchi hizi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo taasisi zao za udhibiti wa viwango zimethibitishwa, zikija huku kwetu zinatambuliwa. Kwa hiyo, si kwetu tu kwa maana ya Zanzibar na Tanzania Bara, lakini pia hata Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 131

Mradi wa Maji Kiwira

MHE. SUMA I. FYANDOMO aliuliza:-

10 NOVEMBA, 2022

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya Mradi wa Maji wa Kiwira ili uanze kutekelezwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha mapitio ya usanifu kwa ajili ya mradi utakaotumia chanzo cha Mto Kiwira kupeleka maji katika Jiji la Mbeya na Mji wa Mbalizi. Hatua inayoendelea sasa ni manunuzi ya Mkandarasi na katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga shilingi 4,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa chanzo na utekelezaji wa mradi utafanyika kwa awamu.

SPIKA: Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, swali la nyongeza.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Napata shida sana mimi pamoja na wananchi wa Mkoa wa Mbeya, kwamba mradi wa zaidi karibu bilioni 300 sasa hivi unapewa shilingi 4,000,000,000, any way, ngoja niende kwenye maswali ya nyongeza.

Swali la kwanza; je, ni lini sasa Serikali itakamilisha mradi wa *phase II* ili kuhakikisha Wilaya ya Mbarali, Rungwe, Kyela na Chunya, Mbeya Mjini na Mbeya Vijijini ili waweze kupata maji?

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Rais alivyokuja mwezi Agosti, 2022 alipita pale Wilayani Rungwe, alitoa agizo kwamba kufika mwezi Oktoba mradi wa maji unaoendelea pale Tukuyu uwe umekamilika, lakini sasa hivi Kata zote Bagamoyo, Msasani, Buliaga, Bitigi, Makandana, Kawetele maji ni shida kweli kweli. Sasa je, ni lini Serikali itakamilisha mradi huo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante lakini swali namba moja sijampata vizuri.

SPIKA: Mheshimiwa rudia swali lako la kwanza.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba niulize hili swali namba moja. Kwenye Mradi huu wa Kiwira kuna *phase II* ambayo ikikamilika itahudumu maji kwenye Wilaya ya Mbarali, Chunya, Rungwe, Kyela, Mbeya Mjini pamoja na Mbeya Vijijini. Je, ni lini utakamilika huo mradi wa *phase II*? (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Suma Fyandomo amekuwa akifuatilia mradi huu muhimu, ni mradi wa kimkakati, *phase II* ambayo

10 NOVEMBA, 2022

anaiulizia kupitia wilaya nyingine zote, itafanyika baada ya *phase one* kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi tayari kupitia Mhandisi Mshauri ameshamaliza kuandaa nyaraka za zabuni kwa kufikia tarehe 26 Oktoba, kupitia Mamlaka ya Maji na tayari Mamlaka ya Maji imetoa nyaraka za zabuni za kandarasi za ujenzi katika mradi huu na tunategemea kwa namna ambavyo wakandarasi wameshapatiwa tarehe 8 Novemba, kandarasi nne zimeshafanikiwa kufika kwenye eneo la mradi, kuangalia hali ya mradi ili sasa ifikapo tarehe 7 Disemba tunatarajia vitabu vya zabuni viwe vimetoka, kwa hiyo wataenda kuvichukua. Ikifika mwisho wa mwezi Disemba sasa hapo ujengaji wa mradi *phase one* ndio unaanza. Kwa hiyo kwa maeneo hayo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, yatafanyiwa kazi baada ya *phase one* kukamili.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na agizo la Mheshimiwa Rais, binafsi nilifika Tukuyu, nilikwenda kwenye chanzo, nilihakikisha tarehe ambayo tulimwahidi Mheshimiwa Rais, tuliweza kufikisha maji yale kutoka kwenye kile chanzo na tulishayaingiza kwenye *existing line* za Tukuyu Mjini na maji tayari yalishaanza kuingia kwenye maeneo yote. Kwa hiyo, kipindi hiki cha ukame, sio tu Tukuyu wala sio tu Mbeya, ni maeneo yote ya Tanzania tunapitia changamoto kwa sababu vyanzo vyetu vya maji kina kimeshuka.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Bunge lako Tukufu, niombe sisi Wabunge wote tumwombe sana Mwenyezi Mungu mvua zinyeshe, hiyo ndio itakuwa suluhu na maeneo yote tutaendelea kupata maji kwa uzuri.

10 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimewaona wote mliosimama. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Katika kipindi cha bajeti niliuliza swali la msingi kuhusiana na utekelezaji wa maji ya kutoka Mto Rufiji, nikaelezwa kwamba katika mwaka huu wa fedha wa 2022/2023, upembuzi yakinifu ungefanyika, sasa napenda kujua Serikali imefikia hatua gani katika upembuzi yakinifu uliotarajiwa? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mto Rufiji ni moja ya mito muhimu sana kwa vyanzo vya maji ambavyo sisi tunavitumia. Tayari wataalam wetu wameshaanza kazi na tunatarajia watakamilisha upembuzi yakinifu kwa namna ambavyo muda umepangwa.

SPIKA: Mheshimiwa Sebastian Kapufi, swali la nyongeza.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda kwa kipindi hiki ina tatizo kubwa sana la maji. Naishukuru Serikali tuko katika Miji 28 lakini tunacho chanzo kizuri cha Ikorongo kwa kipindi hiki cha shida ya maji, Serikali inasema nini kwa kutu-support ukizingatia upembuzi yakinifu umeshafanyika? *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sebastian Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa *crisis* ambayo tuko nayo sasa hivi ya ukame, vyanzo vyote ambavyo tunaviona bado vina maji mengi tunakwenda kuvitumia ili kuhakikisha tunakwenda kupunguza shida ya maji katika jamii zetu. Hivyo nitalichukua hili la chanzo cha Ikolongo na nitaagiza mara moja watu wetu ambao wako Mpanda kuhakikisha wanakifikia hiki chanzo na kuona kinatumika ipasavyo. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwenye Mji wa Liwale upo mradi wa kuupatia maji mji ule na tumechimba visima vitatu Kijiji cha Turuki, lakini mradi ule sasa umesimama kwa muda mrefu. Je, lini hatima ya mradi ule ili Mji wa Liwale upate maji safi na salama?

(Hapa Mhe. Zuberi M. Kuchauka alizungumza bila kutumia kipaza sauti)

SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka, sijui huwa una shida gani na kisemeo. Kwa nini huwa unakipeleka pembeni kabla hujamaliza kuongea. Haya malizia ili Taarifa Rasmi za Bunge ziweze kujua uliuliza nini.

10 NOVEMBA, 2022

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, kuna mradi kwenye Mji wa Liwale kwa ajili ya kuupatia maji Mji wa Liwale na mradi ule tumechimba visima vitatu kwenye Kijiji cha Turuki, lakini mradi ule umesimama sasa ni muda mrefu. Nini hatima ya mradi ule ili Liwale iweze kupata maji safi na salama?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulifika Liwale, mwenyewe nilikwenda Liwale, lakini vile vile Mheshimiwa Waziri amekwenda Liwale na huu mradi uliosimama, naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge nitaufuatilia leo hii na baada ya Bunge hili naomba tuonane.

SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa suluhisho pekee la kumaliza changamoto ya maji Wilaya na Nkasi, Mkoa wa Rukwa ni maji kutoka Ziwa Tanganyika. Ningependa kufahamu mchakato huo umefikia wapi wa kutoa maji Ziwa Tanganyika?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Ziwa Tanganyika yapo kwenye mkakati wa Wizara na tayari baadhi ya maeneo tumeshaanza kuyatumia maji ya Ziwa Tanganyika. Hivyo kwa maeneo ya Nkasi na maeneo yote ambayo yapo karibu na Ziwa Tanganyika, tunaomba waendeleo kuvuta subira tutakwenda na tutahakikisha chanzo hiki cha uhakika tunakitumia.

SPIKA: Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Hali ya upatikanaji wa maji katika Kata ya Makanya, Kwekanga na Kwayi ni mbaya sana na ukizingatia sisi hatuna matatizo ya vyanzo vya maji. Je, ni lini Serikali itapeleka maji kwa haraka iwezekanavyo katika kata hizo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kata hizi alizozitaja pamoja na Makanya zipo kwenye utendaji wa kiwizara. Naomba nitumie Bunge lako Tukufu kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba nitasimamia kuhakikisha ndani ya mwaka huu wa fedha haya maeneo yanapata maji.

SPIKA: Mheshimiwa Hassan Mtenga, swali la nyongeza.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mheshimiwa Spika,

10 NOVEMBA, 2022

kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Jimbo la Mtwara Mjini ni jimbo ambalo kidogo lina shida ya maji, lakini niishukuru Serikali kwa kutuletea bilioni 19 kwa ajili ya usambazaji wa maji kwenye Jimbo la Mtwara Mjini. Hata hivyo, tumechimba visima toka mwaka jana na vile visima vitatu mpaka sasa hivi havina mwelekeo wowote. Je, ni lini Serikali itamaliza visima hivi ili wananchi wapate maji kwenye Jimbo la Mtwara Mjini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nnaomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nipende kupokea pongezi zake kwa Serikali kwa kazi kubwa ambayo imeshafanyika Mtwara. Kupitia visima hivi hata jana tumeongea na Mheshimiwa Mbunge, tayari nimeshawaagiza wale watendaji wetu pale Mtwara wanakwenda kulifanyia kazi na hili ni agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu, maeneo yote ambayo visima vilishachimbwa sasa hivi watendaji ni lazima kuvipa vipaumbele ili kuhakikisha vinasambaza maji kwenye maeneo yote ya wananchi.

SPIKA: Mheshimiwa Daniel Awack, swali la nyongeza.

MHE. DANIEL A. TLEMAI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Je, ni lini Serikali itamalizia Mradi wa Bwawani katika Mji wa Karatu ili kukidhi uhitaji wa maji katika Mji wa Karatu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

10 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel Awack, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ameulizia kuhusu kumaliza mradi ambao tayari upo kwenye utekelezaji. Miradi hii tunapoianza inakuwa na ukomo wake, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutasimamia vizuri mradi ule ambao Mheshimiwa Waziri yeye mwenyewe ndio alifika pale na kutatua hii changamoto, hivyo tutasimamia kuhakikisha ndani ya muda wa mkataba mradi unakamilika.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ukame unaoendelea nchini kama ulivyosema ni muhimu nafikiri Wabunge wameshashauri mara kadhaa Serikali kutumia vyanzo vya maji vya uhakika, kwa maana ya maziwa tuliyonayo. Vile ni vyanzo vya uhakika, yale maji huwa hayapungui na hayaendi popote. Kwa hiyo ni muhimu kuanza, ni miradi mikubwa inahitaji pesa nyingi, lakini huko mbele lazima tutazame haya mabadiliko ya tabianchi yanahitaji uwekezaji huo mkubwa.

Kwa hiyo mnaweza kuanza na baadhi ya haya maziwa, pengine tuanze kufanya kama ambavyo umeme tuna Gridi ya Taifa na umeme popote unapotoka unaingia kwenye Gridi ya Taifa. Tuwe na Gridi ya maji kwani haiwezekani ili maziwa haya sehemu ambazo kunakuwa na changamoto zaidi basi maji yanaweza kupelekwa kutoka kwenye vyanzo vingine.

Tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

10 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante, ushauri nimeupokea.

SPIKA: Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 132

Hitaji la Kituo cha Polisi Kintinku- Manyoni

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA aliuliza:—

Je, kuna mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi Tarafa ya Kintinku Manyoni?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchini, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na Kituo cha Polisi pamoja na nyumba za makazi ya askari katika Tarafa ya Kintinku. Kwa sasa wakazi wa eneo hilo hupata huduma toka Kituo Kidogo cha Polisi kinachotumia jengo lililokuwa ghala la mazao ya kilimo waliloazimwa na Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Serikali inamshauri Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na Uongozi wa Wilaya na Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, kutenga eneo mahsusi kwa ajili ya kujenga kituo na nyumba za askari ili Serikali iweze kukiingiza kituo hicho katika mpango wake na kukitengea fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, swali la nyongeza.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa majibu mazuri kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa tayari wananchi wa Tarafa ya Kintinku wameshatenga eneo la zaidi ya hekari nne katika Kijiji cha Lusilile kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi. Je, Naibu Waziri yuko tayari kuambatana nami kwa ajili ya kuona hilo eneo kama linafaa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; katika Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya ya Manyoni, tuna upungufu mkubwa sana wa nyumba za watumishi hususani OCD na Mpelelezi wa Wilaya.

Je, nini *commitment* ya Serikali kuhakikisha kwamba tunawajengea watumishi hawa nyumba za kuishi? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

10 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze wananchi wa Tarafa ya Kintinku kutenga hizo hekari nne ili kujenga Kituo chao cha Polisi, nami nitaungana na Mheshimiwa Mbunge wakati wowote atakapokuwa tayari kwenda kujiridhisha juu ya kituo hicho. Hata hivyo, hata kabla mimi sijaenda, niutake Uongozi wa Polisi Mkoa wa Singida waanze kutembelea eneo hilo na kama wanaona linafaa waweze kuwashauri ipasavyo wananchi hawa ili nitakapofika basi ni uamuzi uwe unafanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la ukosefu wa nyumba za watumishi akiwemo *OCD* Manyoni, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge, tumeripoti hapa wakati wa bajeti kwamba tunao mpango wa ujenzi wa vituo vya polisi na makazi ya askari na tutakwenda kujenga kwa awamu kwa kutegemea upatikanaji wa fedha. Ni matarajio yetu kabla ya mwaka 2025 Manyoni pia watakuwa mmefikiwa. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nini mpango wa Serikali kuwasaidia wananchi wa Kata wa Kamwanga, Wilayani Longido Mkoa wa Arusha, kumaliza Kituo cha Polisi ambacho walianza kukijenga kwa juhudu zao wenyewe?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

10 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tuwapongeze wananchi ambao wamejitokeza kujenga Kituo cha Polisi huko Longido, niuelekeze Uongozi wa Polisi, Mkoa wa Arusha waweze kufuatilia kufanya tathmini kituo hicho kimefikia hatua gani na kinahitaji kiasi gani cha fedha ili kukamilisha ili tuweze kuingiza kwenye mpango wetu kutegemea upatikanaji wa fedha. Hilo jambo likishafanyika, basi tutakamilisha kituo hicho.

SPIKA: Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Uvinza?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunafahamu Uvinza ni Wilaya mpya na kama zilivyo Wilaya nyingine hazijawa na Vituo vya Polisi vya ngazi ya Wilaya. Nimpe matumaini Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeanza ujenzi wa Vituo vya Polisi kwenye hizi Wilaya zote mpya kadri

10 NOVEMBA, 2022

tunavyoendelea kupata bajeti tutaifikia Wilaya ya Uvinza ambayo tunatambua iko mpakani itapewa kipaumbele katika ujenzi huo. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Jumanne Mtaturu, swali la nyongeza.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba tulipitisha bajeti ya Bilioni Moja na Milioni Mia moja kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi pale Ikungi na leo ni mwezi wa Novemba. Je, ni lini sasa Serikali italetwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho kama bajeti ilivyopitishwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtaturu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba bajeti hiyo ilipitishwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho kinachofanyika ni Jeshi la Polisi limewasilisha mpango wa ujenzi ambao utakapopitishwa na Wizara utawasilishwa Hazina kwa ajili ya kutoa fedha. Ni matarajio yetu fedha za maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki kwa vile zinatoka kwenye Mfuko ambao tunauzungumzia kwa ukamilifu wiki iliyopita zitatoka kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa kituo hicho kuanza. Ninaashukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

10 NOVEMBA, 2022

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa. Wananchi wa kata za Mbokomu na Uru-Shimbwe katika Jimbo la Moshi Vijijini wamejenga Vituo vya Polisi na bado havijakamilika.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hawa waliotumia nguvu zao kujenga hivi vituo na kuwajengea nyumba Polisi wa Kata?

SPIKA: Sasa hapo umeuliza maswali mawili na wewe unaruhusiwa kuuliza swali moja tu la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri jibu moja kati ya hayo aidha Nyumba za Watumishi au Vituo vya Polisi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Patrick Ndakidemi, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze yeye na wananchi wake kwa kuanza ujenzi wa vituo hivi kwa kutumia nguvu zao na jitihada zao Mbokomu na Uru. Kama nilivyojibu kwenye swali lililoulizwa na moja ya Wabunge hapa tutawatuma Askari wetu upande wa Kilimanjaro ili wafanye *assessment* ya kiwango kilichofikiwa, kiasi gani kinatakiwa ili vituo hivi viweze kukamilishwa hatimaye tuviingize kwenye mpango wa ujenzi. Nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Hivi karibuni kumekuwa na wimbi la uhalifu katika Mikoa mbalimbali nchini. Je,

10 NOVEMBA, 2022

Serikali ina mkakati gani wa kuunga mkono juhudi za wananchi nchi nzima ambao wameanzisha ujenzi wa Vituo vya Polisi ili kuweza kuvimalizia na hatimaye ulinzi uweze kuwa imara?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chaurembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza uwepo wa wimbi la uhalifu ambao tumekuwa tukisema hapa uhalifu ni matokeo ya tabia na mwenedo wa jamii tunaupiga vita kwa nguvu zetu zote. Ndiyo maana yalivyojitokeza matukio haya ya *panya road*, ni jeshi halikulala hatimaye nchi imekuwa tulivu pia niwapongeze wananchi kwa kujenga Vituo vya Polisi mahala vinakohitajika ili mapolisi wawe karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kama nivyosema kwenye majibu yangu ya msingi ya maswali yaliyopita, pale ambapo wananchi wamefanya kazi niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuwasiliane na ma-OCD wetu na ma-RPC kwenye Mikoa yetu waweze kufanya tathmini kwenye kiwango cha ujenzi kilicho fikiwa na nini kinatakiwa kukamilisha, ili tuweze kuingiza kwenye mpango wa ugaramiaji kitaifa. Tukilifanya hilo itakuwa rahisi kuingizwa kwenye mipango. Nashukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Idd Kassim Idd, swali la nyongeza.

10 NOVEMBA, 2022

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni lini sasa Serikali itaanzisha ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya katika Halmashauri ya Msalala?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Msalala ni Wilaya mpya kama ilivyo Wilaya nyingine, tumeanzisha mpango wa ujenzi wa Vituo vya Polisi kwenye maeneo mapya ambayo hayakuwahi kuwa nayo, ni matarajio yetu kulingana na upatikanaji wa fedha Wilaya ya Msalala pia itafikiwa muda siyo mrefu ujao. Nashukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Hali ya Kituo cha Polisi cha Mchinga ambapo ndipo Makao Makuu ya Jimbo ni mbaya sana. Je, ni lini kitafanyiwa ukarabati Kituo hicho?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, kama ifuatavyo:-

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, tunatambua Mchinga ndiyo Makao Makuu ya Jimbo na Wilaya. Niombe Mheshimiwa Mbunge uridhie nilishaahidi kufanya ziara katika Mkoa wa Lindi, moja ya maeneo nitakayopitia ni Mchinga ili kuona kiwango cha uchakavu wa kituo hiki tuweze kufanya mpango wa ukarabati ili kikamilike kiwe kituo stahiki kufaa kukaliwa na Askari wetu. Nashukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na 133

Hitaji la Vituo Tarafa ya Gonja na Mamba – Same

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha vituo vya Polisi katika Tarafa za Gonja na Mamba/Vunta?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge Wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na vituo vya Polisi katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi. Tarafa za

10 NOVEMBA, 2022

Gonja na Mamba/Vunta hazina vituo vya polisi wala maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya polisi na Nyumba za Makazi ya Askari. Wananchi wa Tarafa za Gonja na Mamba/Vunta hupata huduma za polisi toka vituo vya polisi vya Same mjini na Gonja, na vituo vidogo vya polisi vya Kihurio na Ndungu.

Mheshimiwa Spika, ni ushauri wangu kwa Mheshimiwa Mbunge kushirikisha Halmashauri ya Wilaya ya Same kutenga maeneo katika tarafa za Mamba na Gonja kwa ajili ya kujenga kituo cha Polisi pamoja na Nyumba za Makazi ya Askari, ili Serikali iweze kuweka kwenye mpango wake wa Bajeti kwa ajili ya utekelezaji. Nashukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, swali la nyongeza.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza pia nikushukuru kwa kunipa nafasi kwamba swali hili lirudiwe leo kwa mara ya tatu.

Kwa kuwa, Kata ya Bombo lijenga Ofisi yake ya Kata na ikaweka nafasi ya Polisi pamoja na chumba cha mahabusu. Kwa kutambua kwamba hizi sehemu zote ulizoongelea ziko tambarare na hawa wakazi wa Kata Tisa zote wako milimani ambako usafiri ni shida sana. Je, Serikali haioni ianzishe kituo mnaita *Police post* ili angalau katika Kata hii ya Bombo kiwepo kusaidia wananchi walioko huko milimani?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

10 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuwapongeza wananchi wa eneo hilo kwa kujenga jengo la utawala ngazi ya Kata na kutenga eneo kwa ajili ya huduma za Kipolisi. Nitumie nafasi hii kuelekeza Jeshi la Polisi hususani Mkoa wa Kilimanjaro kutembelea eneo hilo kuona kama ujenzi ule unakidhi kuwa Kituo cha Polisi basi huduma za kipolisi zianze kutolewa kwenye eneo hilo. Nashukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Anne Kilango, swali la nyongeza.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii. Kwa kuwa, Tarafa ya Gonja na Tarafa ya Mambavunta ni Tarafa ambazo ziko kwenye milima mikubwa sana na hiki Kituo cha Polisi cha Gonja wanapata shida sana kuwafikia wananchi kule milimani.

Je, Serikali haioni umuhimu mkubwa sana wa kupeleka gari lenye uhakika kwenye Kituo cha Afya cha Gonja ili waweze kuwahudumia wananchi wangu walioko kwenye Tarafa zile ambazo ni ngumu sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anne Kilango Malacela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli hii Kata aliyoitaja ya Gonja iko milimani na ni changamoto kubwa kutoka maeneo ya tambarare kuwahudumia wanachi kule

10 NOVEMBA, 2022

milimani. Tunatambua umuhimu wa gari tumeeleza hapa juzi hivi sasa tulipata magari 78, na tumeweza Mkoa wa Kilimanjaro kuupatia magari mawili, ni ahadi yetu kwa Mheshimiwa Mbunge kulingana na changamoto ya usafiri wa eneo hilo tutakapo pata magari eneo hilo litafikiwa na kupewa kipaumbele. Nashukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Tarafa ya Kalenga katika Jimbo la Kalenga Mkoani Iringa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace Tendega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli sasa hivi mwelekeo tumekwenda mpaka ngazi ya Kata tumepeleka maofisa wetu wakaguzi na wakaguzi wasidizi kwa ajili ya kusomamia Shughuli za polisi. Sasa iwapo Kata ya Kalenga haina tutaipa kipaumbele ili kata hii iweze kingatiwa hatimaye vijana wetu waweze kufanya kazi kwenye mazingira stahiki ya kutoa huduma za usalama wa raia na mali zao. Ahsante.

SPIKA: Mheshimwa Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

10 NOVEMBA, 2022

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Jimbo la Tunduru Kusini lina Tarafa Tatu. Tarafa ya Namasakata haina Kituo cha Polisi na ndiyo iliyopo mpakani na Msumbiji.

Je, ni lini Serikali itapeleka Kituo cha Polisi katika Tarafa hii ya Namasakata?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mpakate, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge ikiwa Tarafa hii haina kituo cha kwanza tutafute ardhi. Ardhi ikishapatikana tuipime tukabidhi Jeshi la Polisi hatimaye tuweze kuingiza eneo hilo kwenye mpango wetu wa ujenzi wa Kituo cha Polisi. Kwa vile anasema kiko mpakani inahitaji kwa kweli ulinzi eneo hilo na tutakupatia kipaumbele iwapo upatikanaji wa ardhi utatekelezwa mapema. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ni muhimu Wizara, kwa sababu hapa mmezungumzia ujenzi wa vituo umewaahidi wengine kwenda kutembelea huko lakini ni muhimu sana makazi ya Polisi nchi nzima kurekebishwa kwa sababu yale hayahitaji ardhi nyingine yapo tayari pale lakini makazi yao yana hali mbaya sana maeneo mengi kwa hiyo ni muhimu sana kuwa na mpango maalumu wa kuyarekebisha yale makazi ya Polisi. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 134

Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya – Mkalama

MHE. FRANCIS I. MTINGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya katika Halmashauri ya Mkalama?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu swali la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania inaendelea kutekeleza mpango wake wa kuhakikisha kuwa kila Wilaya inakuwa na jengo la Mahakama. Aidha kwa sasa miradi inayoendelea ni ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya 18. Ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mkalama umepangwa kufanyika katika mwaka huu wa fedha 2022/2023. Kwa sasa taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zinaendelea. Ahsante.
(Makofi)

10 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Francis Isack Mtinga swali lanyongeza.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri sana ya Serikali yanayotia moyo, naomba naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Katika Kata ya Iguguno kuna Mahakama ya Mwanzo ya kisasa kabisa na ya kidigitali. Je, Serikali sasa haioni haja ya kuanza Mahakama ya Wilaya kwa muda katika Kata hii, kwani wanachi wanapa shida sana kwenda Wilaya ya Iramba kwenda kufuata Mahakama ya Mwanzo?

Swali la pili, iwapo Serikali itaridhia kutumia Mahakama hii; je, itakuwa tayari sasa kutumia mahabusu ya Singida Mjini badala ya kwenda Kiomboi kwani uhakika wa usafiri wa Singida Mjini ni rahisi na ni karibu zaidi? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kimsingi maoni yake yote tunayachukua na tunakwenda kuyafanyia kazi kuona Je, kuna uwezekano wa kuanza kutumia huduma zote hizi mbili ambazo Mheshimiwa Mbunge amependekeza. Ahsante. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Zacharia Paulo Isaay, swali la nyongeza.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Spika, ni miaka minne sasa nikiendelea kutetea ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mbulu. Kwa kuwa, sasa mahakama ya Wilaya inapitiwa na ujenzi wa barabara ya lami. Je, ni lini Serikali itatekeleza azma yake ya ujenzi wa Mahakama yetu hiyo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Wa Katiba Na Sheria, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika ahsante. Nadhani sijampata Mheshimiwa vizuri anatoka Wilaya gani ili niweze kumuelekeza hatua tulizofikia.

SPIKA: Mheshimiwa Zacharia Paulo Isaay mwambie wewe ni Mbunge wa Jimbo gani.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri ananifahamu mimi ni Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini. Nimekwenda ofisini kwake na kwake mwenyewe mara kadhaa kutetea ujenzi wa Mahakama ya Wilaya. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kutoka Mbulu. Wilaya ya Mbulu ni miongoni mwa Wilaya ambazo ziko kwenye mkakati wa kujengewa Mahakama kwa kipindi hiki cha fedha cha 2022/2023.

10 NOVEMBA, 2022

Kwa hiyo taratibu za kupata Mkandarasi kwa ajili ya zoezi hilo zinaendelea. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Joseph Kasheku Msukuma, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, wananchi wa Jimbo la Geita Vijijini wanalazima kufuata huduma za Mahakama ya Wilaya kilometa 60. Je, ni lini Wizara itakuwa tayari sasa kwenda kujenga Mahakama ya Wilaya kwenye Jimbo hilo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Musukuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuko kwenye mkakati wa kuendelea na utekelezaji wa ujenzi wa Mahakama za Wilaya katika Wilaya 18. Ninapenda tu kumwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba ujezi wa jengo ambalo linahitajika katika Wilaya yake linaenda kuanza katika kipindi cha fedha kijacho kwa ajili ya kutekeleza mpango huu wa maboresho ya Mahakama nchini. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza.

MHE. MWANTUMU M. ZODO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa, Serikali inaendelea na ujenzi wa Mahakama za Wilaya na kule Wilayani Mkinga Mahakama yetu ya Wilaya iko tayari na imeanza kazi wiki

10 NOVEMBA, 2022

iliyopita. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kukarabati zile Mahakama za Mwanzo ambazo ni chakavu sana. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu, Mbunge Viti Maalum kutokea Mkinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sasa hivi katika mpango wetu tunaoendelea nao, tunaendelea kukarabati na kujenga majengo mapya katika maeneo mbalimbali. Hivyo nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba majengo yaliyochakaa yataendelea katika utekelezaji wa mpango tulionao katika kipindi hiki tulicho nacho na kipindi kijacho kwa sababu mwisho wa mradi huu ni 2025 kuhakikisha kwamba huduma za Mahakama zote nchini katika ngazi mbalimbali tutakuwa tumezikamilsha. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa mara ya pili ninaomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, Tarafa ya Ikuwo haina Mahakama ya Mwanzo, wananchi wanalazimika kusafiri zaidi ya kilimita 100 kwenda kupata huduma za kimahakama kitu ambacho kinawafanya wananchi wakate tamaa wasiendeleo kufuatilia haki zao. Ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Mwanzo kwenye Tarafa ya Ikuwo ili wananchi wangu waweze kupata huduma hiyo. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nipende kujibu swali la Mheshimiwa Sanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida nimuombe Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane baada ya kikao hiki ili niweze kumpa mkakati ambao tumeuweka, kwa sababu katika kipindi hiki tuna miradi Sitini ambayo iko katika hatua mbalimbali na kwa sababu katika kipindi hiki tunayo miradi 60 ambayo ipo katia hatua mbalimbali na kwa sasa, kwa vile sina kumbukumbu sahihi hapa niwasiliane naye ili niweze kumsaidia kujua Mahakama yake inaenda kuanza lini ujenzi. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Uyui iko kwenye chumba kidogo sana tulichopewa na Ofisi ya DC.

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya ya Uyui? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, nipende kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kutoka Uyui kama ifuatavyo: -

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi, ni kwamba sasa hivi Mahakama ya Tanzania imeendelea katika shughuli za ujenzi wa Mahakama mbali mbali hapa nchini. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge, tuwasiliane baada ya kipindi hiki ili niweze kumuweka katika kumbukumbu zilizo sahihi juu ya lini tunaenda kuanza ujenzi katika eneo lake. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, napenda kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kujenga Mahakama mpya nzuri ya Wilaya ya Kilombero. Swali, je, ni lini Mahakama ile itazinduliwa katika Kata ya Kibaoni pale ili wananchi wawenze kupata huduma za Mahakama Mpya?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, nipende kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kutoka Kilombero. Ni kwamba wakati wowote atajulishwa utaratibu wa uzinduzi wa ile Mahakama kwa sababu haijaisha muda mrefu sana. Sasa hivi tunaharakisha uzinduzi wa Mahakama zote ambazo zimekamilika hapa nchini kwa ajili ya kuzizindua. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa John Daniel Pallangyo, swali la nyongeza.

10 NOVEMBA, 2022

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuzijenga na kukarabati Mahakama za mwanzo za Nkwaranga na West Meru, kama ilivyoahidi mwaka wa fedha uliopita 2021?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, nipende kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Pallangyo tuwasiliane ili niweze kumpa mkakati halisi, lakini mpango kazi wote umeshakamilika katika kukarabati na kujenga majengo mapya ya maeneo ambayo hayana mahakama. Kinachokosekana hapa ni kumbukumbu sahihi tu, kwa sababu swali linakuwa limekuja kwa sasa hivi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi; Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Sumve, sasa aulize swali lake.

10 NOVEMBA, 2022

Na. 135

**Ujenzi wa barabara ya Fulo – Nyambiti – Malya kwa
kiwango cha lami**

MHE. KASALALI E. MAGENI aliuliza: -

Je, ni lini barabara ya Fulo kupitia Nyambiti hadi Malya itafanywa upembuzi yakinifu na kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuifanyia Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina barabara ya Fulo – Sumve – Nyambiti hadi Malya kwa lengo la kuijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikitafuta fedha za Usanifu, Wizara kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), itaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili kuhakikisha kuwa inapitika vizuri majira yote. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya shilingi milioni 668.345 zimetengwa kwa ajili ya kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hiyo. Ahsante.

10 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza?

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Spika, Barabara hii ya Fulo kupitia Nyambiti mpaka Malya ni barabara ya muhimu sana kwenye uchumi wa Serengeti ya Kusini, na ni barabara ambayo Serikali imekuwa ikiahidi kuendelea kutafuta pesa, wakati huo Serikali ikitambua Jimbo la Sumve hatuna hata milimita moja ya lami.

Je, ni lini sasa *seriously* pesa hizi zitapatikana, mkafanya upembuzi yakinifu na kuanza kujenga barabara hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, barabara yenye urefu wa kilometa 71 inayotokea Magu inapita Bukwimba – Nkalalo – Ngudu mpaka Hungumalwa nimekuwa nikiiombea kila mara ijengwe kwa kiwango cha lami na Serikali mljibu kwamba sasa mmejipanga kujenga katika bajeti hii.

Je, sasa ni lini ujenzi huo unaanza au inaendelea kupewa ahadi kama ambavyo imekuwa kawaida ?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo: -

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye, barabara hii bado haijafanyiwa usanifu; na nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna barabara mbili tu ambazo zilikuwa bado hazijafanyiwa usanifu katika Mkoa wa mwanza ikiwepo hii. Tumeshamwagiza Meneja wa Mkoa aangalie kama kutatokea *saving* yeyote kwenye hela ya maendeleo, hii barabara tuanze. Tuhakikishie barabara hii lazima itafanyiwa usanifu katika kipindi cha mwaka wa bajeti huu tunaokwenda na mpango wa sasa.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, barabara ya Hungumalwa hadi Magu, Mheshimiwa Mbunge nishahidi, Waziri ameongea naye na tumeshaahidi. Tayari Meneja wa Mkoa ameelekezwa aitangaze kuianza kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa *TANROADS* Mkoa wa Iringa walitii agizo la kwenda kuangalia barabara ya Mchepuko wa Mlima Kitonga, na tayari wameshafanya maandalizi ya awali. Je, Serikali inasemaje kuhusu kuanza usanifu na kuijenga barabara hiyo ya Mchepuko wa Mlima Kitonga ili wananchi waweze kupita kwa urahisi? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la

10 NOVEMBA, 2022

nyongeza la Mheshimiwa Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyokiri kwamba tayari tumeshatoa maelekezo na baada ya kuipitia barabara sasa kinachofuata ni kuanza kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, suala hilo litafanyika kwa sababu ndiyo barabara itakayotuokoa ikitokea changamoto yoyote katika Mlima kitonga. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Ally Kassinga, swali la nyongeza.

MHE. ALLY M. KASSINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi ya swali la nyongeza. Barabara ya kutoka Kiranjeranje – Nanjirinji mpaka Ruangwa imefanywa upembuzi wa kina na upembuzi yakinifu kwa lengo ya kujengwa kwa kiwango cha lami. Wakati Wana-Nanjirinji tukisubiri lami, hali ya barabara hii si nzuri, hususan maeneo kutoka Mangaja – Nakiu – Nanjirinji mpaka Ruangwa, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutoa maelekezo kwa Meneja wa TANROADS Mkoa wa Lindi ili wakakagua barabara hii na wafanye utaratibu wa dharura ?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Kassinga, Mbunge wa Kilwa, kama ifuatavyo: -

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, barabara hii ilifanyiwa usanifu wa awali, na mwaka huu tunakamilisha usanifu wa kina. Kwa hali aliyoelezea nataka tu nitumie fursa hii kumuagiza meneja wa *TANROADS* aende aiangalie hiyo barabara na kama kutakuwa na changamoto kubwa inayohitaji msaada wa Wizara basi tuweze kuwasiliana; lakini tunavyoongea leo aende aitembelee hiyo barabara ili aweze kurekebisha na wananchi waendeleo na shughuli zao za kawaida. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona niulize swali la nyongeza. Pamoja na nia njema ya Serikali kupeleka miradi ya barabara za lami kwenye Jimbo la Kibamba hata hivyo pamekuwa na sintofahamu ya miradi hiyo kutobeba *components* za fidia zaidi ya migogoro na wananchi. Je, Serikali inasema nini juu ya jambo hilo?

SPIKA: Mheshimiwa Issa Mtemvu swali la msingi halina maneno ya fidia hapa. Sasa ni swali jipya kabisa hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri, labda kama una majibu nalo lakini haliendani na la msingi. Kwa hiyo, nakupa uhuru, kama unayo majibu mjibu kama huna niambie.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, naomba nimwombe Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, aweze kuwasilisha swali kama swali kwa maana ya masuala ya fidia. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

10 NOVEMBA, 2022

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali, ni lini sasa barabara inayotoka Chang'ombe kupitia *DUCE* mpaka Mgulani mtamalizia, kwa sababu sasa hivi malori ni mengi sana ambayo yanapeleka vifaa viwandani na njia haipitiki sasa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dorothy Kilave, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, labda tu nichukue nafasi hii kumuhimiza mkandarisi lakini pia na Meneja wa *TANROADS* kuhakikisha kwamba barabara hii inakamilishwa haraka. Mheshimiwa Mbunge kama kutakuwa na changamoto ya ziada naomba tuonane nae ili tuweze kutatua hiyo changamoto kama ipo kwa upande usimamizi ama kwa mkandarasi mwenyewe. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, sasa aulize swali lake.

Na. 136

Barabara ya Mnivata – Newala – Masasi

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA aliuliza: -

Je, nini kinakwamisha ujenzi wa barabara ya Mnivata – Masasi kupitia Tandahimba na Newala?

10 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imepata mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara kutoka Mnivata hadi Masasi yenye urefu wa kilometa 160. Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii zilitangazwa mwezi Julai, 2022 na kufunguliwa tarehe 18 Oktoba, 2022 na kwa sasa uchambuzi wa zabuni unaendelea. Aidha, Serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni 3.086 kwa ajili ya kulipa fidia wananchi watakao athirika na ujenzi huo, na zoezi la kulipa wananchi hao fidia linaendelea. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri. Wananchi wangu wa Mitesa Namalenga, Mdibwa, Nagaga, Chungutwa pamoja na Mpeta, wote hawa wamekuwa wakitarajia ujenzi. Sasa, kwa niaba yao nauliza, ni lini ujenzi huu utaanza?

Mheshimiwa Spika, lakini pili, kuhusu fidia, nimemsikia amejibu kwamba fidia imeanza, namuomba Waziri anijibu kwa asilimia ngapi jibu hili lina ukweli? Ahsante.

10 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri swali la pili linahitaji takwimu, kama unazo takwimu utampa, kama huna utamjibu hilo swali kwa maandishi utampatia Mheshimiwa Mbunge. Majibu kwa swali la kwanza.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lindi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa vijiji vyote alivyovitaja kwamba barabara hii itajengwa. Tulishatangaza na tumesema tumefungua; na kwa kuwa inafadhiliwa na *African Development Bank*, mchakato wa manunuzi tuna uhakika *by March* barabara hii itaanza kujengwa, japo sisi tunasema tayari tumeshaanza kulipa fidia mchakato unaendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa swali lake la pili, kwa asilimia ngapi, nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye jimbo lake, Jumatatu watakuwa hapo wanalipa fidia kwani tayari Mnivata hadi Chikwaya Wilaya ya Mtwara tayari tumeshalipa, baada ya Tandahimba itakwenda Newala na Masasi na fedha ipo tayari, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Sasa kwa jibu lako maana yake kwenye jimbo lake hawajaanza kulipwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo lake bado tunategemea kuanza Jumatatu.

10 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Sawa. Mheshimiwa Mchungahela nadhani pamoja na kwamba lilihitaji takwimu sasa umepata jibu la uhakika kwako hawajafika bado.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Spika, ni kweli.

SPIKA: Mheshimwa Jacqueline Msongozi, swali la nyongeza.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Barabara ya kilometa zaidi ya 300 ambayo inatoka Lumecha Kupitia Msindo – Mputa – Kitanda mpaka Londo kwa Mpepo Morogoro, imefanyiwa Upembuzi na usanifu wa kina kwa muda mrefu sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa haraka sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya inayoanzia Lumecha- Kilosa kwa Mpepo, Malinyi hadi Ifakara kama alivyoisema, tumejibu mara kwa mara kwamba imeingizwa kwenye mpango wa EPC+F, na hivi tunavyoongea wakandarasi wameshaoneshwa hizo

10 NOVEMBA, 2022

barabara na wako wanaandaa zabuni kwa ajili ya kujenga kwa mfumo huo wa *EPC+F*, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, swali la nyongeza.

MHE: EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Spika, Serikali itaanza lini ujenzi wa kilometa 30 kwa kiwango cha changarawe kutoka Uyogo kupita Iberansua, Mbika mpaka Urowa, ambapo barabara hii imekuwa kiungo kikubwa sana kwa wananchi na uchumi wa halmashauri wa Ushetu na mpaka tunavyoongea sa hizi magari yanadondoka ya wakulima wanaosafirisha mazao yao?

SPIKA: Sehemu ya mwisho hujasikika. Magari yanadondoka? Anzia hapo kwenye magari yanadondoka.

MHE: EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Spika, magari yanayopita barabara hiyo yanaanguka yanayokuwa yamebeba mazao ya wakulima.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Nyongeza la Mheshimwa Cherehani, Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii kama alivyosema inahitaji kujengwa kwa changarawe. Sehemu ya barabara hii ilikuwa chini ya barabara ya *TARURA* na sasa ndo imepangiwa bajeti. Nataka nimuhakikishie

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka huu tutakwenda kuikarabati barabara hiyo. Nitumie nafasi hii kumuagiza Meneja wa Mkoa wa Shinyanga aende aitembelee hii barabara na kuifanyia ukarabati wa haraka ili kuokoa maisha na mali na hayo magari ya wananchi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Wabunge niwakumbushe maswali mafupi, unapouliza marefu unawanyima wenzako fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza. Nenda moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Shamsia Mtamba, swali la nyongeza.

MHE. SHAMSIA A. MTAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya uchumi inayoanzia Mtwara Mjini kuelekea Msimbazi kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shamsia Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara iliyoitajwa tayari tumeshaifanyia upembuzi wa kina, Serikali sasa inatafuta fedha kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

10 NOVEMBA, 2022

MHE. DKT.CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, kwenye barabara ya Himo kuelekea Rombo, eneo wanalovuka wanafunzi wa Shule ya Korona na maeneo yale yanayokaribia masoko ya Kisambo na Mwika ni hatari sana kwa wapita njia lakini kwa magari pia. Je, Serikali ipo tayari kujenga matuta kwenye maeneo hayo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Charles Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, suala la matuta ni suala ambalo linategemeana na wataalam. Naomba niwaagize wataalam wa *TANROADS* hasa Meneja wa Mkoa wa Kilimanjaro, aende akafanye usanifu ili aone kama kuna umuhimu wa kufanya suala hilo. Ni vyema akawasiliana na Mheshimiwa Mbunge ili aone maeneo ambayo anahitaji suala hili linakotakiwa kufanyika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Katani Katani, swali la nyongeza.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Spika, barabara ile ya kutoka Mnivata ambayo Mheshimiwa Waziri amejiibia vizuri sana tunaomkanganyiko wa namna ya ulipaji fidia kwenye mimea.

Je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kunipa mchanganuo wa fidia ya mimea ili niweze kuelimisha wananchi wangu?

10 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mchanganuo wa mimea, sijaelewa hapo. Mchanganuo kwa maana ya kwamba wanalipa kila mmea shilingi ngapi; au mchanganuo wa mimea ukimaanisha nini?

MHE. KATANI A. KATANI: Yes, kumekuwa na shida kwenye mikorosho kule.

SPIKA: Haya, hilo linaweza kuwa swali la msingi. Labda kama unazo hizo bei au lije ama swali la msingi?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, sina.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri hana hizo bei za mimea. Kwa hiyo, utalileta kama swali la msingi.

Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya Mtoni - Bombo kwenda mpaka Bashewa, na barabara hiyo hiyo kutokea upande wa Maramba mpaka Tanga, usanifu wake lini utaanza? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mbunge, kama ifuatavyo:-

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni barabara ambayo tumeitengea fedha kwa ajili ya kukamilisha usanifu wa kina mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, nina uhakika barabara hii mwaka huu itaanza kufanyiwa usanifu wa kina. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni nini kinakwamisha ujenzi wa barabara kipande cha Haydom mpaka Labay?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hakuna kinachokwamisha ujenzi wa barabara hii. Zabuni ya kwanza ilitangazwa kilometa 25 ambayo inatoka Mbulu Mjini hadi Galbad; na kuanzia Labay - Haydom, barabara hii zabuni za kuitangaza zinaendelea. Kwa hiyo, awe na Subira, zikikamilika taratibu za manunuzi, barabara hii itatangazwa kwa kilometa nyingine 25 lakini pia barabara hii imeingizwa kwenye EPC+F. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la

10 NOVEMBA, 2022

nyongeza. Ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kinyanambo C - Mapanda hadi Kisusa katika Jimbo la Mufindi Kaskazini? Maana ilikuwa imeahidi kujenga kilometa tano tano na ni barabara ya kiuchumi.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, Iringa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja itajengwa kwa kiwango cha lami kufuatana na upatikanaji wa bajeti. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kutafuta fedha kuijenga kwa kiwango cha lami barabara hiyo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mrisho Gambo, swali la nyongeza.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, naomba kufahamu barabara ya kutoka uwanja mdogo wa *Airport Arusha* mpaka eneo la Kilombero kwa kiwango cha njia nne utaanza lini; na hasa ukizingatia kwamba barabara hii ikikamilika itasaidia kuondoa msongamano na changamoto ya mafuriko kwenye Kata za Ungalimitedi, Sombetini na Usunyai?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu

10 NOVEMBA, 2022

swali la nyongeza la Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara ya *Airport* kwenda Kilombero ni barabara ya muhimu kwenda njia nne; na ujenzi wa barabara hii kama ilivyo kwenye Majiji mengine utategemea sana upatikanaji wa fedha. Nadhani labda kwenye mpango huu tunaouendea, basi tutaomba tuweze kuanza kuweka mpango wa kuijenga barabara hii kwa kiwango cha barabara nne ili kupunguza msongamano katika Mji wa Arusha. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana.

Tunaendelea na Wizara ya Afya; Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aullize swali lake.

Na. 137

Upungufu wa wataalam wa mazoezi tiba na huduma ya utengamao

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje katika kupambana na changamoto ya upungufu wa Wataalam wa Mazoezi Tiba na huduma ya Utengamao nchini?

SPIKA: Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

10 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeajiri jumla ya wataalam 84 wa mazoezitiba na huduma mtengamao katika ajira za mwezi Julai, 2022. Hata hivyo, kufanya idadi ya wataalam wa mazoezitiba na huduma mtengamao kuongezeka kutoka 653 hadi 737.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa kuna jumla ya vyuo vikuu vinne ambavyo ni Muhimbili, KCMC, Bugando na Zanzibar vinavyotoa taaluma, hivyo kupunguza changamoto ya uwepo wa wataalam katika soko la ajira.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, swali la nyongeza.

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa vile bado tuna upungufu mkubwa wa wataalam wa mazoezitiba na utengamao:-

Je, hawaoni sababu ya kuanzisha course hii kwenye vyuo kama UDOM ambapo inachukua watu wengi ili angalau tupate wahitimu wa taaluma hiyo kwa wingi?
(Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

10 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Mbunge, Dkt. Kaijage kwa namna anavyoshirikiana na Wizara ya Afya kwa karibu hasa kwenye kushughulikia huduma ya mama na mtoto kwenye Mkoa wa Pwani. Vilevile nimwambie tu kwamba, siyo tu Chuo Kikuu cha *UDOM*, kuna mkakati wa vyo zaidi ya vitano sasa tunaongeano na kushirikiana na Wizara ya Elimu ili kuanzisha kada hizi ili kusaidia kupunguza upungufu wa wataalam kwenye soko la ajira. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Hospitali ya Machame Mkwarungo ambayo inaendeshwa kwa ubia baina ya Serikali na Kanisa la KKKT, imekuwa na changamoto za kiutawala na upungufu wa vifaatiba na kupelekea huduma inayotolewa pale kuwa hafifu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kushughulika na changamoto hizi ili kurejesha huduma kwenye hospitali hii muhimu?

SPIKA: Swali zuri, lakini inabidi lije kama la msingi, kwa sababu kanuni ya 53 inataka Waziri ajibu kwa ukamilifu. Sasa swali la msingi linahusu mazoezitiba, wataalam wa mazoezitiba na huduma ya utengamao. Sasa changamoto ya utawala na changamoto ya vifaa, tusimweke kwenye mazingira magumu Mheshimiwa Naibu Waziri ya kujibu swali letu kwa uhakika. Lije kama swali la msingi.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 138

Utafiti wa dawa zinazosababisha vifo kwa akina mama wanaojifungua kwa upasuaji

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA aliuliza:-

Je, kuna utafiti wowote ambao umefanyika ili kubaini dawa za ganzi/nusu kaputi zinazosababisha vifo kwa wanaojifungua kwa upasuaji?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tafiti mbalimbali zilizofanyika zinaonesha kuwa sababu zimegawanyika katika makundi matatu:-

- (a) Sababu za vinasaba (*DNA*);
- (b) Sababu zinazohusiana na ganzi ila siyo za moja kwa moja; na
- (c) Sababu zenye mahusiano ya moja kwa moja na ganzi.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, vifo vya namna hii hutokea mara chache sana na ndiyo maana wakati wote tunawashauri akinamama wajawazito kuhudhuria kliniki ili kutoa muda wa kutosha kufuatiliwa na pale inapohitajika kufanyiwa upasuaji usiwe wa dharura. Aidha, jamii inahamasishwa kutoa lishe bora kwa wajawazito.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri. Niliomba kujua dawa ambazo zinasababisha akinamama kufa kutokana na ganzi; naomba sasa Serikali kupitia Wizara ya Afya ifanye utafiti ili tuweze kubaini ni dawa zipi ambazo zinasababisha wanawake wajawazito baada ya kujifungua wafariki? Kwa sababu hapa ametoa sababu nyingine, siyo zile dawa ambazo ilikuwa ni swali langu la msingi. Nashukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, labda nimsaidie Mheshimiwa Mbunge kwamba leo mimi niliyesimama hapa huwa nikitumia *flagyl* nachubuka, lakini mimi kutumia *flagyl* na kuchubuka, haimaanishi *flagyl* inachubua watu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anatakiwa kujua kwamba vifo vya akina mama vimepungua kwa zaidi ya nusu kutokana na upasuaji unaofanyika na kutumia ganzi hizi hizi. Maana yake ni nini? Ganzi ambazo tunazozitumia leo hapa Bungeni, tuna Wabunge wengi

10 NOVEMBA, 2022

wamefanyiwa operesheni na wametumia dawa hizi hizi na wako salama. Maana yake ni nini? Tumesema kuna sababu za vinasaba na kuna sababu nyingi ambazo zipo; sasa hizo haziwezi kufanya tukaleta taharuki kwenye nchi.

Mheshimiwa Spika, sisi madaktari huwa ni watu ambao tuna miiko na tunaapa na tuna maadili ya taaluma. Sasa ni muhimu sana unapouliza swali uhakikishe kwamba huvuki ile mipaka ya kitaaluma na miiko kwa sababu kimsingi labda kama angetaka nimweleze ninaposema *DNA* maana yake nini; ninaposema ganzi, maana yake ni nini? Kwa sababu kuna ganzi ukipigwa hapa kwenye mgongo inasababisha mtu kutokupumua. Kuna *procedure* za kufanya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nakuomba tuonane kama wanataaluma ili tuweze kusaidiana nawe uelewe jambo linafanyikaje?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwa Wabunge na majibu kutoka upande wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, la kwanza kabla sijaleta matangazo kwenu, niwakumbushe kwamba tuliongeza idadi ya maswali kwa siku ili kwanza kuweza kuitendea haki kanuni yetu ambayo inataka maswali yajibiwe kwa ukamilifu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, leteni maswali ya msingi yajibiwe kwa ukamilifu na Serikali. Tukisubiria maswali ya nyongeza ndiyo yale kila siku hapa tunasema nasimama leo mara ya pili au ya tatu unauliza

10 NOVEMBA, 2022

jambo lile lile, na ukiuliza jambo lile lile haimaanishi Serikali ilisikia, lakini ni kwamba hata wewe ulikuwa unasubiria tu hapa ndani. Je, usingepewa hiyo nafasi? Kwa hiyo, tupeleke maswali Ofisi ya Bunge ili tupate nafasi ya maswali ya msingi na Serikali iweze kujibu kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kuna jambo lingine ambalo liko upande wa Serikali. Naibu Mawaziri ndiyo ambao mara nyingi huwa mnajibu maswali hapa, mara chache Mawaziri. Huwa mnajitahidi kutaja majina ya Waheshimiwa Wabunge na majimbo yao. Kama Mbunge humfahamu vizuri jina, kwa sababu mimi nakuwa nimeshamtaja, sema tu; naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: Usitaje jina lake kama hulijui maana mimi naletewa hapa, jina langu siitwi hivi. Ama usitaje jimbo la Mbunge kama hulijui, kwa sababu itaonekana Wabunge hapa wanauliziana maswali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, lazima wewe mwenyewe uwe umejiambia, kama unamjua Mbunge vizuri na jimbo lake, taja jina lake na jimbo lake. Kama hujui, nenda moja kwa moja, we mwite tu, Mheshimiwa Mbunge, kanuni zetu ndivyo zinataka hivyo. Ukitaka kwenda kwenye nyongeza, basi weka nyongeza yenye usahihi. Maana kuna Wabunge wa Viti Maalum humu ndani wanatajiwa majimbo, Mbunge wa Viti Maalum halafu anatajiwa jimbo badala ya mkoa pengine. Ndiyo maana hata sisi huwa hatutajwi kwa sababu kimsingi hawa ni Wabunge wa wa Taifa zima. Ni Wabunge ambao wanawakilisha kundi fulani. Kwa hiyo, hata ile mikoa ni utaratibu tu wa kuwapata waingie humu ndani. Kwa hiyo, naomba sana hilo kwa

10 NOVEMBA, 2022

sababu Waheshimiwa Wabunge wanajikuta katika mazingira tatanishi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nirekebishe Taarifa Rasmi za Bunge, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, yeye ni Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi na siyo Arumeru Mashariki. Arumeru Mashariki ni Mheshimiwa Dkt. Pallangyo. Kwa hiyo, nimelazimika kulisema hilo ili Taarifa Rasmi za Bunge ziandike, huyu ni Mbunge anatoka wapi?

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nilete sasa matangazo tuliyonayo na tutaanza na matangazo ya wageni. Tunao wageni ambao nafikiri wataingia baadaye lakini yupo mgeni mmoja ambaye yupo pale Jukwaa la Spika. Huyu ni mgeni wetu kutoka Mkoa wa Tanga na huyu ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mheshimiwa Omari Mgumba. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine ambao wataingia baadaye, ni wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika, watatangazwa wakishaingia humu Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wenu mbalimbali; tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini kutoka Taasisi ya Kimazingira *Nourish Africa* ya Jijini Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 26 wa Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya, ambaye ni Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ambao ni Waimbaji wa Shukrani Kwaya Ileje kutoka Itumba Mkoa wa Songwe, karibuni sana. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Deogratus Ndejemi ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na huyu ni Mkurugenzi Mkuu wa *Watumishi Housing Company*, Dkt. Fred Msemwa, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni saba wa Mheshimiwa Jumanne Sagini, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambao ni Viongozi Wakuu wa *LATRA* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wengine wa Mheshimiwa Jumanne Sagini, hawa ni Maafisa Waandamizi na Askari kutoka Jeshi la Polisi Jijini Dar es Salaam. Bahati mbaya sikuyapata majina yenu, lakini mnakaribishwa sana Bungeni. Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Jumanne Sagini tena ambao ni Viongozi Wakuu wa Mamlaka ya Usimamizi na Bima (*TIRA*) kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 12 wa Mheshimiwa Hamisi Taletale ambao ni Mashehe kutoka Jimboni kwake Morogoro Kusini Mashariki wakiongozwa na Shehe Mahamoud Amri Waziri, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo linasema Mashehe, lakini pale kuna watu wamesimama ambao sio mashehe, lakini hawa wote, kundi hili linatoka kwenye Taasisi ya *Al-Masjid Zawiyat Al-Qadria* Tanzania, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 13 wa Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu ambao ni Wawakilishi

10 NOVEMBA, 2022

kutoka *Kambele Investments* ya Mkoani Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 32 wa Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu tena ambao ni Watendaji wa Kata kutoka Jimboni Arumeru Magharibi, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni tisa wa Mheshimiwa Husna Sekiboko ambao ni wazazi wake pamoja na ndugu zake kutoka Lushoto Mkoa wa Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 22 wa Mheshimiwa Janet Mahawanga ambao ni Wanakikundi cha Kazi lendelee kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. Kwa hiyo, tukifikia mahali tunasema kazi iendelee, tunakitaja kikundi chenu, hongereni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Khamis Kassim Ali ambao ni wapigakura wake kutoka Jimboni Wawi, Kusini Pemba, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watano wa Mheshimiwa Oran Njeza ambao Wajumbe wa Chama cha Waandishi wa Habari kutoka Mkoani Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Taska Mbogo ambao ni wadogo zake na mtoto wa kaka yake kutoka Nchini Uingereza, karibuni sana. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watano wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni viongozi wa *Club* ya Waandishi wa Habari Songwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Abdallah Chaurembo ambaye ni ndugu yake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Nusrat Hanje ambao ni Mwakili wa *RS Company* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 28 wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ambao ni Wanachama wa Taasisi ya Wasanii Tanzania kutoka Ubungo, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ambao ni Waandishi wa Habari wa Redio Safina kutoka Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ambao ni viongozi wa CCM kutoka Mkoa wa Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na tutaanza na kundi la Walimu, wanafunzi na walezi 50 kutoka Kituo cha Chilemu *Academy* kutoka Turiani Mkoani Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wanafunzi 25 kutoka Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), karibuni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao, lakini tunalo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge; anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote, kuwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na LATRA na TIRA itaendesha semina kuhusu elimu ya usalama barabarani leo tarehe 10 Novemba, 2022 kuanzia saa saba kamili mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge hapa.

Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu ili kuwajengea uelewa wa masuala mbalimbali yanayohusu usalama barabarani ili kama wawakilishi muweze kuwa na hiyo taarifa. Pia nanyi mtoe mchango wenu kama wawakilishi wa wananchi kupunguza ajali ambazo zinawaacha Watanzania wengi wakiwa walemavu na wengine kupoteza maisha.

Waheshimiwa Wabunge, hili tangazo ni pamoja na kwamba tutapata mafunzo leo maana tupo viongozi ambao huwachochea madereva kwenda mwendo wa kasi kwa sababu umechelewa ulipokuwa unaenda. Kwa hiyo hilo nalo watalizungumza leo na ndio mmewaona wako pale juu, wako tayari kwa ajili ya kazi hiyo ili kutusaidia na sisi tusiwalazimisha wale ambao wanatuendesha kwenda mwendo kasi kuzidi ule unaotakiwa, pamoja na mambo mengine kufunga mikanda na mambo kama hayo, watatueleza yote hayo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tutaendelea na ratiba yetu. Katibu!

10 NOVEMBA, 2022

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI:
Kamati ya Mipango.

SPIKA: Kamati ya Mipango.

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa
unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa
Fedha 2023/2024 pamoja na Mwongozo wa kuandaa
Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha
2023/2024**

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Asia Abdukarim Halamga atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi ajiandae.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili kuweza kuchangia katika Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2023/2024. Nitaanza kuchangia katika Sekta ya Maliasili na Utalii. Sekta hii ndani ya Taifa letu inachangia pato la Taifa kwa asilimia 17.6, pia inachangia fedha za kigeni kwa asilimia 28. Sekta hii inafanya vizuri sana na tunaona kabisa katika pato la Taifa ni sekta muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mapendekezo yafuatayo katika sekta hii ya Maliasili na Utalii. Kwenye

10 NOVEMBA, 2022

bajeti iliyopita tuliamua kwamba ndege zetu tuongeze VAT, kwenye hili naomba tulipitie upya kwa sababu ukizingatia Sekta ya Maliasili na Utalii ilikumbwa na janga la *Covid 19* na iliweza kuathiri kidogo uchumi na hasa ukiangalia mataifa ya jirani kupitia ndege hizi za kukodi kuna kitu cha kujifunza kupitia tozo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kutatua migogoro kati ya wananchi na hifadhi, lakini mapori yetu tengefu, tutakuwa tumefanya jambo kubwa sana, kuondoa migogoro ili kuhakikisha kwamba hifadhi hizi zinaendelea kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kuweza kuanzisha na kuipa TANAPA, kutoka hifadhi 16 hadi kufikia hifadhi 22 na Hifadhi hizo zikiwa Nyerere, Burigi, Ibanda, Kyerwa, Rumanyika, Kigosi na Mto Ugala. Wote sisi ni mashihidi kazi kubwa ambayo ameifanya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kutangaza filamu ya *Royal Tour* na wote ni mashuhuda wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukifika Mkoa wa Kilimanjaro, Arusha, Manyara, kanda zote ambazo zina utalii tunashuhudia kabisa hoteli zimejaa, ziko *booked*, zingine mpaka mwakani. Kwenye hizi hifadhi mpya ambazo tumezongeza tukiweza kuweka malango kila hifadhi, ili tukatangaze utalii, sio tu kwa kanda ya kaskazini, tukaongeza na kanda zingine ili kupitia filamu hii ya Mheshimiwa Rais, ambayo imeonesha tija kwa muda mfupi na maeneo mengine yakiweza kupandishwa utalii wao, basi tutapandisha mapato katika nchi yetu na hasa kwa kupata fedha za kigeni.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kupitia fedha za UVIKO, Wizara ya Maliasili na Utalii wameweza kupata vifaa mbalimbali, mfano, Miradi ya *REGROW*, wameweza kupata vifaa vya kuweza kutengeneza barabara na leo watu wanaopita barabara ya Arusha kwenda Serengeti ni mashihidi wakubwa namna ambavyo barabara zimenyooka na zinaweza kufikika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mradi huo kukamilika, Miradi ya *REGROW*, tunaomba bajeti iangalie vizuri sekta hii ili miradi hiyo basi tutakapokuwa tumebaki nayo sisi, iweze kuwa na tija na tuweze kuiendesha. Sio tu mradi unapokamilika tushindwe kuuendesha na hasa tukizingatia tija ambayo imeonesha kwa muda huu mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna kazi hifadhi yetu ya Nyerere kule tumeweza kuianzisha, askari kule wako zaidi ya 120, lakini nyumba zao ziko 30. Tuna kitu cha kufanya ili kuendelea kuhakikisha kwamba sekta hii tunaisimamia vizuri na inaendelea kuleta tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia hayo katika Maliasili, naomba niende Wizara ya Kilimo. Katika ilani yetu ya Uchaguzi ya Mwaka 2020 - 2025, tunaona katika ukurasa wa 42(4) imeongelea suala kubwa la kusaidia nchi yetu katika suala la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ilani imeongelea kutoka tani 63,000 hadi kufika 2025 tunatarajia kuwa na tani zaidi ya 200,000 za zao la ngano. Zao la Ngano kwa sasa ndani ya nchi yetu tunatumia fedha kubwa za kigeni kuagiza zao hili nje ya nchi na hasa Nchi ya Ukraine. Bahati mbaya sana wote tunajua hali halisi ya Ukraine

10 NOVEMBA, 2022

kwa sasa, najaribu kujiuliza na kutafakari, je, vita ikizidi kuendelea Ukraine sisi tutakuwa na hali gani, ilihali tuna mashamba makubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitolea mfano wa shamba la *NAFCO* lililopo Wilaya ya Hanang ambayo lipo chini ya Mwekezaji anayeitwa *Ngano Limited*. Nimemfuata kaka yangu Bashe sio chini mara moja wala mara mbili, mtu huyu ana hekari takribani 40,000 ambazo hazina tija kwetu sisi Watanzania kwa sababu hakuna anachokizalisha. Inasadikika wamemwongezea tena hekari 10,000, tuna kila sababu ya kuiangalia eneo hili kwa jicho la pili ili tuweze kusaidia nchi yetu katika kukuza ngano na hasa tukizingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yule pamoja na kumpa hekari 40,000 pamoja na kutokuzalisha kwake, bado anaendelea kuvamia maeneo ya wananchi wadogo wadogo na anaendelea kusababisha migogoro, kati ya Serikali na wananchi, huku tukizingatia hana chochote ambacho anaingiza kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mashamba makubwa mengi katika nchi yetu *KTPL* yako kule Morogoro, yapo mashamba saba ya maua na mbogamboga kule Arusha, yako mashamba makubwa Songea ya *NAFCO*. Mashamba haya yana tija gani kwa Taifa letu. Nashauri mashamba haya makubwa yaondolewe chini ya Wizara ya Fedha na yaweze kukabidhiwa Wizara ya Kilimo na iweze kuyasimamia mashamba haya ili tuone tija kwa Taifa letu. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mashamba makubwa wenzetu wanajeshi wanalima kilimo, lakini miundombinu hatuwawezeshi tunaendelea kutengeneza malalamiko, migogoro na kuona wenzetu hawafanyi kazi ambayo inayostahili. Tunaomba mashamba yote makubwa kwenye nchi hii tuweze kuwakabidhi Wizara ya Kilimo na waje na majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano leo, JKT vijana wanafundishwa silaha, wanafundishwa kufanya kazi, wanafundishwa kilimo. Tuna mashamba makubwa katika Taifa letu, lakini tujiulize leo tunanunua ngano Ukraine, leo tunanunua alizeti nje ya nchi na bado vijana hawa hawana ajira. Serikali imejipangaje kutumia nguvu kazi ya vijana katika kuleta uchumi katika nchi yetu na hasa rasilimali tuliyokuwa nayo, rasilimali ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kuisitiza mwekezaji anaitwa Ngano *Limited* katika Wilaya ya Hanang, naomba mkataba ukapitiwe upya, hana manufaa yoyote katika Taifa letu kwa sababu hana anachokizalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa siku ya leo, mchango wangu unaishia hapa. Nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Katani Ahmed Katani atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi na Mheshimiwa Jane Jerry James Ntate ajiandae.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Allah Azza wa

10 NOVEMBA, 2022

Jallah kwa kunipa afya njema, lakini nikushuru wewe pia kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupongeze kwa kuipeleka Kamati ya Bajeti kule Mtwara hususan walipokwenda kwenye Bandari ya Mtwara. Ukisoma mapendekezo ya Mpango, Kamati ya Bajeti kuna mambo imependekeza kuhusu Bandari ya Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kuboresha Bandari zetu zote za Mtwara, Dar es Salaam na Tanga kwa zaidi ya bilioni 328 leo kwenye mpango huu ambao unapendekezwa, nimeona Waziri wa Fedha amefanya kazi nzuri sana kwenye Mradi ule wa Liganga na Mchuchuma, lakini wakati tunaweka mpango huu wa Liganga na Mchuchuma tumesahau reli ambayo itasafirisha hayo makaa ya mawe na bidhaa nyingine ambayo reli hii inakwenda Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inanipa mashaka kama Waziri amesahau au la. Mapendekezo yangu kwenye jambo hili kwa sababu Serikali ina nia njema ya kutanua wigo wa biashara na kutoa fursa, basi wanapoleta mpango sasa tuone reli hii ya kutoka Mtwara Kwenda Mbambabay nayo inakuwepo kwenye mpango wetu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona pia Kamati ya Bajeti imependekeza vizuri kwenye Mpango hususan kwenye suala la zao la korosho kwenye kuongeza thamani. Leo bei ya korosho ukiitazama haiwezi kuwa na tija kwa mkulima kwa bei ya 1,800, 1,900. Kamati ya Bajeti imependekeza kuongeza thamani. Hata hivyo, wakati imependekeza kuongeza thamani, ni Serikali hii hii iliuz

10 NOVEMBA, 2022

viwanda vya kubangua korosho. Leo tunashauri tena turejeshe viwanda ambavyo ndio mwarobaini wa kuongeza thamani kwenye korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mkataba wa kuuza viwanda vile ambavyo vimeuzwa zaidi ya viwanda vitano, mkataba ulikuwa wazi, ulikuwa unasema wanunuzi wa viwanda vile wanapaswa kubangua korosho. Matokeo yake vile viwanda havijaenda kubangua korosho hata kipindi kile cha hayati Daktari Magufuli aliposema askari waende wabangua korosho wamekwenda pale Lindi, viwanda vilivyouzwa kwa bei chee hakuna hata malighafi ya viwanda mle ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu kwa Serikali kwa jambo hili kwa sababu alionunua viwanda wamevunja mikataba. Moja Serikali ichukue vile viwanda, wapitie makubaliano ya Serikali ya kuuza viwanda na hao walionunua waweze kurejesha viwanda mikononi mwa Serikali ili tunaposema tunataka kuiongezea soko korosho, basi tuwe tuna viwanda tayari vya kubangua korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza pia kwenye Wizara hii ya Kilimo, walikuwa na mpango mzuri, tulikuwa na mapendekezo ya kujenga viwanda vikubwa vitano. Walisema wanajenga Pwani, Mtwara, Tunduru, Ruangwa, leo fedha zile wamechukua bilioni 210. Mheshimiwa Bashe anakumbuka vizuri, sasa kwa sababu amerudi kwenye Wizara hii tunataka tuone sasa tunaleta viwanda maeneo yanayolima korosho, hii ndio tija kwa mkulima. Kama juzi wakulima wanaona kwamba mfanyabiashara mmoja anakwenda Marekani kilo moja ya korosho iliyobanguliwa inauzwa kwa dola 40 zaidi ya Sh.90,000 ya

10 NOVEMBA, 2022

kitanzania, maana yake imeongezwa thamani na ni ukweli usiopingika kwamba kama tutakuwa na viwanda vya kubangua korosho leo mkulima wa Mikoa wa Kusini, Lindi Mtwara na Ruvuma hawa watu watakuwa *multi-trillionaire*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matajiri wanaozungumzwa wa Tanzania wa kwanza atatokea Mtwara kama tutaboresha viwanda vya kubangua korosho. Ni matarajio yangu kwenye mpango huo Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Kilimo wapo hapa. Wanapokuja sasa kwenye mpango wenyewe tuone mkakati madhubuti wa Serikali unaoelezea namna ya kumsaidia mkulima aidha wa korosho, kahawa kwa sababu bei hizo ukienda Songea kule bei ya kahawa na yenyewe ni kama ya korosho, haieleweki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna pekee ni kuwekeza kwenye kubangua, kuwekeza kwenye viwanda. Ushauri wangu kwa Serikali, Wizara ya Kilimo na Waziri wa Fedha ambaye ni msikivu, kama aliweza kuiongezea fedha Bajeti ya Wizara ya Kilimo mwaka jana, nadhani bajeti ijayo anaweza akaiongezea mara tatu ili tuone tija kwenye sekta ya kilimo inakaa sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu tunalo Bonde la Mto Ruvuma na hapa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo nataka anisikilize sana. Ameweka mipango yake vizuri kwenye Sekta ya Umwagiliaji, lakini ametusahau watu ambao tuna bonde lenye *floor* ya maji wakati wote. Ukija Jimboni kwangu nina Bonde pale Namahonga la Nacha, ukienda Mchichira nina Bonde pale la Ng'apa. Mabonde yale ni mazuri kwa uwekezaji huu wa umwagiliaji unaosema. Nione kwenye mpango sasa na sisi watu wa

10 NOVEMBA, 2022

Mtwara tupo. Kaka yangu Chikota nadhani ana bonde ambalo naye ukitazama ukanda ule unakwenda mpaka Ruvuma. Kuna jambo wanaweza wakalifanya kwenye umwagiliaji na tukazalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda hata Mtama kuna mabonde pale, wasitusahau watuweke kwenye mpango tuone bajeti ya 2023/2024, sisi watu wa Kusini kwenye Sekta ya Umwagiliaji tupo kwa sababu maji tunayo. Hakuna sababu ya kuona kwamba umwagiliaji unawekaweka tu maeneo ya Tabora huko ambako hakuna maji. Watuletee sisi ambao tuna maji tumsaidie uzalishaji, Taifa lipate vitu vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado najikita hapo hapo kwenye sekta ya kilimo. Mheshimiwa Waziri kuna jambo amelifikiria ambalo ni jema sana la kuwasajili wakulima. Jambo hili ukilizungumza na hakuna bajeti ya kufanya jambo hili tutazungumza *story* miaka 10 na hatutaweza kusajili wakulima. Mheshimiwa Waziri akiwaambia watu wa Bodi wasajili wakulima watamwambia wanaotaka kutumika kule ni Maafisa Kilimo hawana fedha za kuwawezesha kwa ajili ya mafuta ya kwenda mashambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tandahimba peke yake inao zaidi ya wakulima Laki Moja na kitu, ili uweze kwenda kuwasajili wale inapaswa ufanye kazi mahsus kabisa ambayo haina tofauti na Sensa. Sasa kwa sasabau umeamua kumsaidia mkulima niombe kwenye Mpango unaokuja nione umeweka *package* kabisa inayokwenda kufanya kazi ya kusajili wakulima ili unapoteleta mbolea yako ya ruzuku usipigwe mchanga wa macho. Utakuwa na takwimu sahihi utamjua Katani

10 NOVEMBA, 2022

huyo ambaye ana namba ya *NIDA*, ana cheti cha kuzaliwa kila kitu ambacho umekitaka lakini ukiweke kwenye mpango, ukizungumza nadharia tutarudi tena hapa tunazungumza habari ya kusajili wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu kwako Waziri wa Kilimo na Waziri wa Fedha upo wekeni bajeti ya fedha tuende tusajili wakulima. Tuwasaidie kwenye mazingira tunapotoa pembejeo za Serikali watu wasiweze kuwarubuni, watu wasiweze kuwaibia na mtaona mnapoweka *projections'* kwamba mnataka korosho mzalisha tani Laki Saba, Laki Nane kama mtakuwa mmesajili wakulima, kwakweli mtakuwa hamuwezi kuibiwa pembejeo lakini hata mnapopanga mipango yenu mtakuwa mnapanga mipango ya kulima ambayo mnaijua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Mapendekezo yangu machache yalikuwa ni hayo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji ni wengi sana ambao wameomba leo, na leo ndiyo siku ya mwisho. Kwa hivyo muda, mtu asije akaona kengele ikigongwa hivi kama ameibiwa muda wake. Tumepiga hesabu kwa majina yaliopo hapa mbele ya Wabunge ambao wameomba kuchangia na kwa muda tulionao imebidi dakika mpewe pungufu ya Kumi. Kwa hiyo, usije ukaona kwamba mbona mi sijapewa dakika kumi? Kwa siku ya leo dakika zimepungua kwa sababu ya majina ni mengi zaidi ya muda tulio nao.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, atafuatiwa na Mheshimiwa Janejelly James Ntate atafuatiwa na Mheshimiwa Kassim Idd Idd.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuweka mchango wangu kwenye Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajadili Mpango wa Mwaka Mmoja katika Mpango wa Miaka Mitano wa 2021/2022 hadi 2025/2026 ambao vipaumbele vyake ni pamoja na kuchochea uchumi shirikishi na shindani, vilevile kuimarisha uwezo wa uzalishaji. Ili mpango huu uweze kutekelezeka ni lazima Serikali iwekeze kwenye sekta ambazo kwanza zitaongeza uzalishaji na kwa maana hiyo katika kuongeza uzalishaji tutaongeza mauzo yetu nje jambo ambalo litasaidia kuongeza Pato la Taifa. Vilevile Serikali iwekeze kwenye sekta ambazo zitatengeneza ajira kwa wingi, jambo ambalo litasaidia kutengeneza nguvu ya manunuzi kwa mtu mmoja mmoja na kwa maana hiyo kuongeza mzunguko wa kifedha na kwa *level* ya chini kuongeza hali ya kipato kwa Halmashauri zetu na kuimarisha mfumo wa utendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuhimarisha sekta hizi nilitaka nichangie kwenye maeneo kama matatu hivi: Kwanza ni eneo la uvuvi. Ninatambua mpaka mwaka jana sekta ya uvuvi imekua kwa karibu asilimia Sita na kuchangia kwenye Pato la Taifa kwa asilimia kama 1.71. Tunaweza kuzalisha zaidi kama tutawekeza kwenye sekta hii ya uvuvi.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana kwa mfano mavuno ya samaki, tumevuna tani karibu laki nne na elfu kumi na tano. Niipongeze Wizara, pamoja na kuwekeza karibu Bilioni 20 kwenye mfumo wa ufugaji wa samaki kupitia njia ya vizimba, jambo ambalo litasaidia angalau vizimba 800 kuanzishwa lakini tunaweza tukazalisha zaidi kama tutawekeza zaidi kwenye ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu pamoja na Serikali kupitia Wizara ya Uvuvi, kuwekeza Billion 20 kwenye ufugaji wa vizimba. Ninashauri kuwe na mnyororo wa ufuatiliaji kutoka Wizara na wale watakao pewa mikopo ili kuweza kuwasaidia kutoa ushauri wa kitaalam, vilevile kusaidia kutafuta masoko ya bidhaa ambazo watu hawa watakuwa wanazalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni la utalii. Pamoja na kwamba kwenye mwaka uliyopita sekta hii ya utalii imechangia karibu asilimia 17 ya Pato la Taifa na zaidi ya asilimia 25 ya fedha za kigeni lakini tunaweza tukafanya vizuri zaidi. Nimpongeze Mheshimiwa Rais, kupitia *Royal Tour* sekta ya utalii imefanya vizuri sana baada ya uzinduzi wa *Royar Tour*, lakini nishauri maeneo kama mawili:

Kwanza, bado tuna vivutio vingi sana vya utalii atujaweza kuvitambua na kuvitangaza. Eneo kama Ukerewe tunavyo vivutio vingi, tumekuwa tunasema hapa tuna jiwe linalocheza, tunazo fukwe nzuri sana lakini bado azijaweza kutambuliwa na kuweza kutangazwa pamoja na maeneo mengine, nishauri Wizara ya Utalii, iweze kutafuta bado, kubaini vivutio vingine vingi vya utalii vilivyopo iweze kuvitangaza. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pili, lingine ni eneo la kilimo. Ni muhimu sana, wachangiaji wengi wamesema juu ya sekta ya kilimo, nami bado nashauri tunahitaji kuwekeza nguvu kubwa kwenye sekta ya kilimo. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, anafanya kazi kubwa sana kwenye sekta hii ya kilimo lakini bado tunahitaji tuwekeze kwa kiasi kikubwa sana, tuweze ku-utilize rasilimali tulizonazo ili ziweze kuwa na tija na kuongeza Pato la Taifa kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo kama Ukerewe wiki iliyopita tumeomba chakula Wizara ya Kilimo lakini kwetu Ukerewe tumezungukwa na maji, tunaweza tukafanya kilimo cha umwagiliaji tuna hekta zaidi ya elfu mbili ambazo ziko tayari kwa kilimo cha umwagiliaji. Tunachohitaji ni msaada tu wa Serikali kuwekeza ili tuweze kutumia maeneo yale kwa tija. Jambo hili pamoja na Ukerewe lakini hata maeneo mengine. Kwa hiyo, nishauri bado tunahitaji kuwekeza kwa kiasi kikubwa sana kwenye kilimo cha umwagiliaji kwenye Taifa hili kwasababu tunayo ardhi ya kutosha tunazo rasilimali maji za kutosha jambo ambalo linaweza likatufanya tukafanya kilimo cha umwagiliaji na kikawa ni kilimo cha tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uwekezaji huu kwenye sekta za uzalishaji. Kwenye sekta zinazotengeneza ajira bado haitokuwa na tija sana kama wananchi wetu hawawezi ku-move kutoka upande mmoja kwenda eneo lingine kufanya shughuli zao za kiuchumi. Nimeona kwenye mpango juu ya uimarishaji wa barabara zetu mbalimbali. Niombe kwa utulivu kabisa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, wanisikilize kwa makini kwenye ukurasa wa 24 wa

10 NOVEMBA, 2022

mpango imetajwa barabara Na. 4141 imetajwa kwa jina la Nyamswa, Bunda, Kisolya ningomba barabara hii ifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii kwa asili tokea upembuzi, usanifu wa kina imetajwa kwa barabara kwa jina la Nansio, Kisolya, Bunda, Nyamswa. Kwa hiyo, ifanyiwe marekebisho na kwenye hoja yangu kwenye eneo hili, ili kuimarisha mawasiliano kwa sababu barabara hii ilitengenezwa kwa *Lots* tatu, *lot* ya kwanza na *lot* ya pili tayari inaendelea basi ikamilishwe *lot* ya tatu ya kutoka Kisolya kwenda Nansio ili kurahisisha mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Haya, ahsante sana. Jamani wahudumu wa humu ndani wamepotelea wapi tena? Jamani leo wahudumu wenu humu ndani tumevaa bluu hebu tupigieni makofi kidogo. *(Makofi)*

Sasa wengine wamechelewa basi wewe soge kidogo hapa walau na wewe upo? Haya jamani hii ndiyo sare yetu siku ya leo wahudumu wenu, ahsanteni sana. Kwa hiyo, mkimuona yeyote hata mkiniona mimi mahali unataka kunituma wewe fanya *faster* leo ni siku yako, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Janejelly James Ntate, atafuatiwa na Mheshimiwa Kassim Iddi Iddi na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ajiandae. *(Makofi)*

MHE. JANEJELLY J. NTATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia siku ya leo.

10 NOVEMBA, 2022

Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na afya, nitakuwa mwizi wa fadhila nisipomshukuru Mheshimiwa Rais, kwa niaba ya Vyama vya Wafanyakazi kwa jambo alilolifanya la wenzetu waliyopata ajali ya kughushi vyeti kuruhusu walipwe akiba yao waliyokuwa wakichangia wao wenyewe ni jambo la kiungwana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile najikita kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuhusu Mpango na Maendeleo aya ya 33 kipengele cha Nne, wanasema watachochea maendeleo ya watu hasa kwenye elimu, afya, maji na ardhi. Leo naenda na elimu na afya. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ameonyesha nia thabiti ya kupigana na umaskini, ujinga na maradhi na ndiyo maana sasa hivi nchi nzima tuna zahanati 5,123, vituo vya afya 650, shule za msingi 17,181 na sekondari 4,211, hizo zinamilikiwa na Serikali tu. Hata hivyo hivi vyote havitakuwa na maana kama hatuna rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya wataamu wa afya ni 126,294 waliopo ni 61,304 pungufu ni 64,960, sawasawa na asilimia 52. Lakini upande wa walimu shule za msingi mahitaji ni 299,210, waliopo ni 167,245 pungufu ni 131,965 sawa na asilimia 44 hizo ni shule za msingi. Vilevile walimu wa sekondari wanahitajika 174,632, waliopo ni 84,700 pungufu ni 89,332 sawasawa na asilimia 51.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwa na rasilimali watu hii hakuna tutakachofanya na ninaona huruma kwa hela tulizoweka kwenye zahanati na shule hasa tulizojenga na COVID. Kama hakuna walimu shule zile zitageuka magofu, zile zahanati zitakuwa magofu. Haiwezi kuwa zahanati kama haina wataalamu na wale wanaoenda

10 NOVEMBA, 2022

kutibiwa pale na bila kukazania hivi vitu adui umasikini hatutumtoa Tanzania. Naomba na nimeangalia mpango mnasema mtawaboresha watumishi lakini hamjasema mkakati thabiti wa kuajiri walimu na watalaam wa afya na hawa ndiyo wakuhudumia hivi vitu nilivyovitaja. Ninaomba huu mpango uoneshe mwaka huu kuna mkakati gani wa kuongeza kada hizi za watalaamu wa afya na walimu wetu ili hayo majengo yasije yakageuka magofu na hela tuliyoweka huko ikapotea kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe bajeti hii ituonyeshe ajira, itoke tu tutoe bajeti ya mwaka mmoja tuseme mkakati ni kuajiri walimu na watalaamu wa afya tu ili tuweze kupunguza hii asilimia hamsini na mbili na asilimia arobaini na moja. Nilikuwa na ushauri tu, ushauri wa kwanza ni hiyo Serikali kuweka mkakati wa namna ya kuajiri hizi kada mbili ili tuweze kufikia malengo tuliyoyaweka, pendekezo la pili Halmashauri zinazo vyanzo vya ndani vya mapato waruhusiwe watalaam wako wengi mtaani, waajiri kwa mkataba ili kuziba pengo hili ili tuweze kumsaidia Mama Samia Suluhu Hassani kufikia nia yake yakufuta masikini, ujinga na maradhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni huo leo, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Kassim Idd Idd, atafuatia na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajiandae.

MHE. IDD K. IDD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Leo ningependa kutoa mapendekezo yangu katika

10 NOVEMBA, 2022

mpango huu wa Mwaka Mmoja wa 2023/2024 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu kwamba Wizara na Serikali imetueleza hapa, kwamba imejipanga kuhakikisha kwamba inaboresha mazingira mazuri kwa wafanyabiashara hata hivyo pia mazingira mazuri katika ufanyaji biashara na uwekezaji katika nchi yetu hii ya Tanzania.

Leo mchango wangu na ushauri wangu utajielekeza kuelekeza Serikali kuongeza bajeti na kutenga bajeti na fedha katika kuhakikisha kwamba ina *invest* kwenye Jeshi letu la Polisi hasa katika kuwekekeza zana za kisasa katika kuweza kupunguza matumizi ya Askari Polisi barabarani. Ni ukweli usiopingika kwamba tunapozungumzia ukuaji wa uchumi na tunapozungumzia mazingira mazuri ya uwekezaji inaonesha ya kwamba ni lazima tutengeneze mazingira yanayoenda na uhalisia wa kumwezesha mfanyabiashara kutekeleza majumu yake kwa wakati au biashara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii utaona Jeshi letu la Polisi katika nchi yetu hii ya Tanzania imekuwa ni *obstacle*, imekuwa ni kikwazo kikubwa katika kuhakikisha ya kwamba inamwezesha mfanyabiashara kutimiza majukumu yake na kumwezesha kutimiza majukumu yake kwa wakati. Leo hii utaona unapozungumzia habari nzima ya uwekezaji ni lazima uzungumzie habari ya miundoimbinu. Serikali yetu nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuweka fedha kuimarisha miundombinu ya barabara. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii utaona barabara ambayo Serikali ime- *invest* fedha nyingi ili kumwezesha mfanyabiashara huyu aweze kutimiza majukumu yake ya kwa wakati, Jeshi la Polisi na hususan Usalama wa Barabarani wanasimama barabarani kuhakikisha ya kwamba ukaguzi wa magari yale, pia mara zote kuhakikisha ya kwamba huyu mfanyabiashara anaweza kutoka hapa kwa namna moja ama nyingine wanaweza kumzuia mfanyabiashara huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga barabara ya njia Nane kutoka Dar-es-Salaam kuja mpaka Chalinze lakini utaona kila baada ya mita tano Askari Polisi hasa *traffic* hawa wamejaa barabarani, lengo ni ukaguzi ambao ukaguzi huu unamchelewesha mfanyabiashara kwenda kutimiza majukumu yake kwa wakati. Sasa niombe Serikali iweze kuona namna gani inaweza ku-*invest* fedha ili iweze ku-*invest* kwenye Jeshi la Polisi kuwa na mitambo ya kisasa kuhakikisha kwamba inafanya kaguzi mbalimbali kwenye maeneo ya barabarani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala zima la Madini. Niipongeze sana Wizara, mimpongeze Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba anaweka jicho lake kumsaidia mchimbaji mdogo mdogo katika maeneo yale. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika sekta ya madini. Ninaomba na ninashauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha upo hapa, leo hii mchimbaji mdogomdogo hasa sekta ya madini na Mheshimiwa Rais alitoa maealekezo kwamba anahitaji Wizara ya Madini, iweze kuchangia Pato la Taifa sasa ili Wizara ya Madini, iweze kuchangia Pato la Taifa lazima Serikali iweke mkakati na bajeti kubwa kuhakikisha

10 NOVEMBA, 2022

ya kwamba inamwezesha huyu mchimbaji mdogomdogo. Kwa hiyo, naomba nishauri Wizara na Serikali iweze kutenga fedha ili iweze kuwakopesha hawa wachimbaji wadogowadogo katika kwenda kufanya uwekezaji kwenye maeneo yao ili waweze kuzalisha kwa wingi na kuweza kuchangia Pato hili la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nizungumzie suala zima la barabara. Leo miundombinu ya barabara yetu katika maeneo yetu haya niipongeze Serikali na nimpongeze Mheshimiwa Rais kwenye Jimbo langu la Msalala, ametoa maelekezo kwa ajili ya ujenzi wa barabara yenye kiwango cha lami kutoka Bulyanhulu kwenda mpaka Kahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na urasimu katika utekelezaji wa miundombinu hii kwa wakati. Sasa niombe Wizara kwamba ihakikishe pale ambapo tunatenga fedha na bajeti kwenda kujenga barabara wapitie upya mambo ambayo yanakwamisha utekelezaji wa miundombinu hii ya barabara ili kuwezesha barabara hizi ziweze kutekeleza kwa wakati na kumwezesha mfanyabiashara kutumia barabara hizi katika kutekeleza majukumu yake kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara yangu ambayo tayari Mgodi wa Bulyanhulu umetenga fedha kiasi cha Dola Million 40 kwa ajili ya utekelezaji wa barabara. Barabara hii kwa muda mrefu sana tumeweza kuipambania Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni shahidi, mpaka dakika ya mwisho Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan, ametoa tamko kwamba barabara ile sasa fedha ipo tayari na barabara ile ianze kujengwa maana ya kutoka

10 NOVEMBA, 2022

Bulyanhulu mpaka Kahama, lakini leo hii utaona Wizara ya Miundombinu na Ujenzi kutoa tu kibali cha kuweza kuitangaza barabara hii ianze kujengwa mpaka leo bado hakijatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe ili mpango huu ambao tunaujadili hapa uweze kutekelezeka kwa wakati ni lazima tupunguze urasimu ndani ya Serikali. Tunapanga mpango huu sisi wenyewe lakini sisi wenyewe hawa hawa tunaukwamisha huu mpango. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Katibu mkuu wa Wizara ya Ujenzi, aweze kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kuanza kutangaza barabara hii na ianze kujengwa kwa wakati, barabara yenye kilometa 77 ambapo fedha zake anayelipa ni mgodi na mgodi upo tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana leo hii tunaona fedha zile tumepewa na Mhisani hivi ikitokea leo madini yamepotea fedha zile tutazitoa wapi? Mlipaji yupo tayari na anataka kujenga barabara ile kwa wakati lakini Katibu Mkuu kutoa tu kibali barabara ile ianze kujengwa hajatoa mpaka leo ilkitokea leo madini yale yamepotea tunafanya nini? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda atafuatia na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha ajiandae.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia Mpango huu wa Mwaka Mmoja.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie habari ya tozo ambazo huwa tunatozwa kwenye miradi mbalimbali ya Serikali inayofanywa. Binafsi ninasikitika sana kwa sababu pesa ambazo Wakandarasi wakubwa wa nje na Wakandarasi wa ndani ambao wanakuja kudai Serikali ni pesa nyingi sana. Mpaka sasa zaidi ya Bilioni 12 tumelipa kama Serikali kwa ajili ya faini mbalimbali ambazo hawa Wakandarasi wameipiga Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba Mheshimiwa Waziri, tunapoweka mikataba yetu naamini tunao wanasheria mahiri sana katika Taifa hili ambao wamesomeshwa kwa kodi za wananchi inakuwaje wanachelewesha kuwalipa na kupelekea Taifa Kwenda kulipa pesa nyingi kiasi hiki kwa ajili ya kulipa faini ambazo zinaendelea. Inabidi iundwe Tume maalum ya kuangalia tatizo hili, inawezekana kuna watu wanafanya maksudi na wanafanya hizo *deal* ili waweze kula hela za Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siamini kwamba tunajua tunahitaji kuendelea kulipana kwa wakati halafu Maafisa Masuuli hawawalipi Wakandarasi hawa mwisho wa siku deni lile linaenda kwa mwananchi wa kawaida ambae ndiye mlipa kodi ambaye pesa yake hii Bilioni 12 ilikuwa na uwezo wa kwenda kuongezea madarasa haya ambayo yanajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema kitu hiki ni kibaya? Miradi inapocheleweshwa na tunakwenda kulipa faini, kwanza inaondoa *value for money*, miradi ile pia inakuwa haiendi kwa wakati, lakini pia inakuwa chini ya kiwango kwa sababu usimamizi unakuwa si mzuri. Kama mradi ulitakiwa kwisha mwaka huu unapomalizia mwakani hata ufuatiliaji wake, ile monitoring and

10 NOVEMBA, 2022

evaluation haiendi sawa. Mimi ninafikiri sasa ni wakati kama Taifa tuhakikishe maafisa masuuli na wanaohusika kuchelewesha watu kulipwa wachukuliwe hatua kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ifike hatua sasa Serikali ilete muswada hapa Bungeni ili kupitia Muswada huu itungwe sheria ambayo itafanya yeyote anayechelewesha achukuliwe hatua ili tuweze kusonga mbele kama taifa; na fedha nyingi sana ambazo zinapotea ziweze kurudi

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mifano ya miradi ambayo tumewalipa hela nyingi sana. Kigongo – Busisi kwa mujibu wa CAG ripoti yake ya mwezi Machi, ukurasa wa 185 anasema tulichelewesha kuwalipa na wao wakatupiga *fine* ya bilioni 1.5 hizi fedha ni nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ripoti ya CAG huyohuyo kuhusiana na SGR anasema tulipochelewa kuwalipa wale wakandarasi tumeweza kuwalipa kama Taifa pesa zaidi ya bilioni 3.144. Hizi fedha ni nyingi sana kwa Watanzania, zingeweza kusaidia kwanye bajeti ya nchi na tukaendelea na maendeleo kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie miradi ya barabara. Kumekuwa na ahadi nyingi sana za barabara. Tunaambiwa tumetoa fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu. Tumetolewa fedha, kwa mfano kuna barabara inayokwenda Soni – Bumbuli mpaka Korogwe kilometa 74. Hii ilitolewa fedha takribani milioni 924 kwa ajili ya upembuzi yakinifu, lakini ukifika wakati wa bajeti nyingine inakuta bado tuko palepale hatujaanza kuufanyia mradi ule kazi, zile fedha zinakuwa zimelala. Na hiki

10 NOVEMBA, 2022

inawezekana ni kichocho ro cha watu kupitishia fedha za kuweza kuliibia Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya Mtwara – Newala na Masasi kilometa 221; zimepelekwa fedha za upembuzi yakinifu wakati huohuo inatengwa bajeti na mwaka mwingine ukija bajeti bado iko palepale. Tunaomba ufuatiliaji wa miradi kama huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mfumuko wa bei. Tunapozungumzia mfumuko wa bei kiukweli unamzidishia mwananchi wa kawaida maisha kuwa magumu; chakula na mahitaji ya muhimu ya kimsingi bei imekuwa juu sana. Kama Taifa na Mheshimiwa mwenye Wizara husika tunaomba tumsaidie mwananchi wa kawaida ambaye kimsingi mfumuko wa bei kwa sasa umepanda umekuwa asilimia 7.8 ilhali inahitajika tusivuke asilimia tatu kama Taifa. Mfumuko wa bei unapokuwa juu maisha yanapanda. Tunaomba tusimamie tuhakikishe tunakuwa tuko sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya ninaunga hoja, lakini tuhakikishe tunasimamia yale ambayo tumekubaliana kama Taifa. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Fedha naona umesimama.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuheshimu mchango na hoja ya msingi kuhusu gharama za maisha na uhusiano wake na mfumuko wa bei, nilitaka kusahihisha takwimu tu. Kwamba, mfumuko wa bei wa nchi yetu uko kwenye

10 NOVEMBA, 2022

asilimia 4 na bado upo kwenye *range* ya asilimia 3 mpaka 5 hatujaenda huko unakosema.

MWENYEKITI: Umepunguza sana sauti. Sina hakika kama Taarifa zetu Rasmi za Bunge zitakuwa na huo ufafanuzi wako.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naongea na bondia mstaafu. Ninachosema ni hivi kwamba...

MWENYEKITI: Zungumza kama unaipongeza Yanga. Maana ndio huwa unaongeza sana sauti. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nasema, pamoja na kuheshimu mchango wa mchangiaji na hoja anayojenga ambayo ina ukweli kuhusu uhusiano uliopo kati ya mfumuko wa bei na gharama za maisha, lakini nilitaka nirekebishe takwimu kwamba, mfumuko wa bei wa nchi yetu ni asilimia 4.0 na bado haujavuka *range* iliyowekwa kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ni kati ya asilimia 3 mpaka silimia 5.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, atafuatiwa na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha; Mheshimiwa Cosato David Chumi ajiandae.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu kwenye Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2023/2024. Mimi ningependa kujikita kwa kuanzia na sekta ya kilimo.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali kwa kuongeza fedha katika bajeti yake toka shilingi bilioni 294 hadi shilingi bilioni 954 kati ya mwaka jana na mwaka huu wa fedha. Na ningependa kuchangia eneo hili kwanza kwa sababu, wananchi wetu asilimia 65 ajira zao ziko kwenye kilimo, lakini pia hata Pato la Taifa ni asilimia 26 ya Pato la Taifa linatokana na mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa kusema kwamba, bado sekta hii haijatumika vizuri katika kuifanya nchi yetu iweze kupata mapato mengi zaidi. Ni imani yangu kwamba, kama rasilimali tulizonazo za ardhi, lakini pia kuwa na utaratibu bora wa kusimamia hiki kilimo ungefanyika basi mambo yangekwenda vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiifuatilia taarifa iliyotolwa na Mheshimiwa Waziri na ile iliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, nimeona pale tuna jumla ya hekta milioni 29 za ardhi ambazo zinafaa kwa ajili ya kilimo; lakini ni asilimia 2.75 tu ya eneo hilo ndilo linalotumika kwa kilimo hivi sasa. Kwa hiyo kuna hekta zaidi ya milioni 28 hazitumiki kwa kilimo hivi sasa. Kwa hiyo nilikuwa nafikiri kuna jambo la kufanya katika eneo hili; kwanza ni kuhakikisha kwamba, hizi pesa ambazo zimeongezwa ziendeleo kuongezwa ili tuweze kuhudumia miundombinu mbalimbali pamoja na mikakati mbalimbali ya kuboresha kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nimeona hapa idadi ya mabwawa ambayo yatajengwa hapa nchini kulingana na ule mpango wa maendeleo ni machache sana. Nilifikiri Serikali yetu niishauri ijikite katika kuongeza idadi ya mabwawa katika mikoa yote ya nchi nzima na si baadhi tu ya mikoa, kwa sababu nafahamu katika mikoa

10 NOVEMBA, 2022

yote karibu ina idadi kubwa ya mito ambayo inatiririsha maji katika kipindi cha mwaka mzima. Kwa hiyo, ukiondoa Dar-es-Salaam mikoa mingine yote tuna uwezo wa kujenga mabwawa na kuwafanya wakulima wetu wakaweza kuzalisha kwenye hili eneo kubwa ambalo limebaki *idle* halitumiki kwa ajili ya shughuli za kilimo na kufanya uzalishaji wa mazao ya kilimo, yale ya chakula na ya biashara, yaweze kuzalishwa kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itaongeza uchumi kwa sababu, sasa hivi bei ya chakula imepanda sana. Na imepanda si kwa sababu, sisi Tanzania hatulimi, tunalima, lakini tunalima kwa kiasi kidogo na tunahuidumia hadi nchi zinazotuzunguka ambazo kwa sasa zina hali mbaya ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ningepomba Serikali ijikite katika vile vituo ambavyo ni vya kutolea huduma kwa wakulima. Kwanza iviongezee majukumu nje ya yale ambayo yameainishwa kwenye mpango wa maendeleo. Moja kati ya majukumu ambayo ningependekeza yaongezwe ni kufuatilia wakulima wetu, mpaka wale wadogo kabisa, ili kujua changamoto zao zikoje, lakini pia kuona namna ya kutatua hizo changamoto ambazo zinawakabili. Wapo wakulima ambao wanakosa mitaji kwa ajili ya kulima, lakini wapo wakulima wengine wana changamoto mbalimbali. Kwa hiyo zitajulikana kupitia hivi vituo. Na hivi vituo visambae si tu kwa mikoa mitano bali viwepo katika mikoa yote ambayo inalima, ukiondoa Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ningependa kuzungumzia masuala ya utalii. Tumepata mafanikio makubwa kupitia mpango ambao uliasisiwa na

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, wa *Royal Tour* kuhusu ongezeko la mapato kutokana na watalii ambao waliongezeka. Taarifa inaonesha kwamba, asilimia 114.7 iliongezeka katika mwaka wa fedha huu uliopita ukilinganisha na ule uliotangulia. Kiasi kama cha dola zaidi ya 1,000 milioni ziliongezeka kwenye pato la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba sekta hii ya utalii imechangia kwa asilimia 17 katika mwaka wa fedha uliopita kwenye Pato la Taifa. Kwa hiyo nilikuwa naomba hii *Royal Tour* iwe *extended*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitarajia nione kwenye mpango wa Serikali wa maendeleo uainishe basi ni wapi sasa tunakwenda baada ya mafanikio yale ambayo tumeyapata katika mwaka uliopita. Kwa hiyo nilitarajia zile hifadhi zetu mbalimbali ambazo hazijapitiwa na mpango ule wa kwanza, mbuga, mpori ya akiba, kumbukumbu za majimaji kule Lindi kwa maana ya Kilwa na Songea, lakini pia hata yale magofu ya kule Kilwa Kisiwani na Songo Mnara. Kuna wale viboko maalbino tuone waingie hata kama kwa *phases*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, tuone namna ambavyo tutaboresha miundombinu, kwa sababu hizi sekta za usalishaji zinategemeana sana na miundombinu ya barabara. Tuone barabara mbalimbali ambazo sasa zina changamoto kubwa zinakwendaje kusapoti katika uendelezaji wa hizi sekta ambazo ni za uzalishaji mali; kuna barabara ya Nangurukuru – Liwale pale kilometa 258 ipo miaka inaenda miaka inarudi, ule upembuzi yakinifu umefanyika, lakini bado haijajengwa.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimalizie na sekta ya elimu. Niiombe Serikali sasa iangalie pia kwa walimu. Walimu wamekuwa wakiishi katika mazingira magumu, hawana nyumba, walimu wanakaa watatu-watatu kwenye nyumba za vyumba vitatu-vitatu na familia zao kubwa. Wangalie na upande huo pia ili kuboresha elimu yetu kwa kusudio ambalo limekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nasema naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, atafutiwa na Mheshimiwa Cosato David Chumi. Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam ajiandae.

MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza mchango wangu kwa kunukuu maneno ya Biblia takatifu; “watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Taifa tunapoangalia matatizo yanayotukabili ama yasababishwa na kiwango cha chini, ama yanasababishwa na ukoesefu wa maarifa, hasa ya sayansi na teknolojia. Tangu tupate uhuru mpaka sasa tunapoangalia mipango yetu ya maendeleo bado dhamira ya mipango yetu haijabadilika sana, lengo letu ni kupambana na umasikini na kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo baadhi ya watu wanajiuliza mbona tumechukua muda mrefu sana kukabiliana na matatizo ya umaskini? jibu nitalitoa baada ya kunukuu maneno ya Abraham Lincoln, mmoja wa

10 NOVEMBA, 2022

Marais wa Marekani, alisema maneno ha yana ninaomba tuyatafakari. Alisema, nikipewa kazi ya kukata mti na nimepewa saa sita, saa nne za kwanza nitazitumia kwa kunoa shoka na saa mbili za mwisho ndiyo nitaanza kati ya kukata mti; sasa tatizo letu la msingi lipo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Taifa tunaujua ukweli huu, lakini bado tunashindwa kuutekeleza kwa vitendo. Kwa maoni yangu, ninapoangalia mpango sioni waziwazi kama elimu ndicho kipaumbele chetu namba moja. Watu wenye maarifa ya kutosha na sahihi wana uwezo mkubwa sana wa kufanya mambo makubwa katika Taifa lao. Wanaweza kulibadilisha jangwa kuwa ardhi ya kilimo, nitatoa mfano. Hakuna jambo linalonisikitisha sana kama kiongozi na kama Mtanzania ninapona nchi ya Misri ambayo asilimia 60 ya nchi yake ni jangwa, wamejifunza sayansi na uhandisi wa kutumia maji ya kilimo cha umwagiliaji maji zaidi ya miaka 1,000. Watanzania tuna mito, tuna maziwa, tunashindwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marehemu Baba wa Taifa alitambua sana umuhimu wa elimu hasa ya ufundi, ndiyo maana alitujengea vyuo vingi sana vya kati vya elimu ya ufundi, lakini kwa bahati mbaya sana viongozi tuliokuja baadaye tulivibadilisha vyuo hivi na kuwa vyuo vikuu. Kama kuna kosa la kiufundi tumelifanya basi ni jambo hili. Ushauri wangu ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, naiomba Wizara ya elimu kama kweli tuna lengo la kupambana na umasikini tuwekeze fedha za kutosha, angalau asilimia 20 ya bajeti kwa ajili ya ufundishaji vijana wetu, hasa masomo ya sayansi na teknolojia, ili kukuza uwezo wa

10 NOVEMBA, 2022

vijana wetu wa kufikiri, wa kubuni, wa kutatua matatizo na kutafuta mbinu na vifaa vya kutatua matatizo yetu. Na kama tunatoa elimu ambayo haina uwezo wa kuwasaidia vijana kufikiri, basi tunapaswa kufikiri upya. Na kama tunadhani elimu ni ghali basi naomba tuujaribu ujinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, hebu uende pale kwa Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha ukamsikilize hoja yake, uielewe na mkaifanyie kazi huko Wizarani kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Cosato David Chumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ajiandae.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Na mimi napenda kutumia nafasi hii kupongeza maandalizi ya mpango pamoja na Taarifa ya Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa sababu, mimi ni mwanamichezo nitumie nafasi hii kuwapongeza Wananchi, jana wametuheshimisha, wamefuata nyayo na wameweza kuuthibitishia umma kwamba kumbe hata sisi ugenini tunaweza na hivyo wameenda hatua ya makundi. Nawapongeza sana. *(Makofi/vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na pongezi hizi zinzendana na kama siku zote ambavyo nasema michezo ni uchumi, michezo ni biashara; kwa sababu kwa Yanga kuingia

10 NOVEMBA, 2022

katika makundi sambamba na Simba maana yake ni kwamba, timu hizi zinapocheza kwa mfano hapa Dar-es-Salaam tunaona watu wanafanya biashara, magari yanasafiri yanajaza mafuta tunapata *fuel levy*, akinamamantilie wanauza chakula, n.k. Kwa hiyo michezo ni biashara tuendeleo kuwekeza katika michezo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuseme hayo napenda kutumia nafasi hii kuipongeza Serikali, hasa kwa suala la ruzuku ya mbolea. Kwa kweli sisi watu wa Nyanda za Juu Kusini tulikuwa na kilio kikubwa. Pamoja na changamoto ndogondogo ambazo wananchi wanakabiliananazo huko *site* lakini kwa kweli ni jambo ambalo linaenda kuinua kilimo chetu, linaenda kuongeza mapato kwa sababu, kutokana na kilimo ambacho ni takriban asilimia 60 wananchi wetu wataongeza kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwa ujenzi wa barabara ya Mafinga kwenda Mgololo, Iringa kwenda *Ruaha National Park* na Uwanja wa Ndege wa Iringa. Hivi vyote vikikamilika kwa sisi watu wa Iringa vitaenda kulisimua sana uchumi kwa sababu utalii ukiongezeka sisi watu wa Mafinga, pamoja na kwamba, tutauza mbao na mirunda lakini pia wakulima wetu watauza mbogamboga, wakulima wa parachichi watauza matunda. Ni jambo la kupongeza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na pongezi hizi nitoe tahadhari. Nimeona katika Taarifa ya Kamati, Ukurasa wa 34, kwamba wana mashaka na *EPC+ Financing*. Sasa na sisi tuliambiwa barabara ya Mafinga – Mgololo itajengwa kwa *EPC+Financing* kwa hiyo,

10 NOVEMBA, 2022

nimuombe Mheshimiwa Waziri anapokuja ku-*wind up* tuweze kupata ufafanuzi kutokana nah ii hoja ya kamati, tunaendaje mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni suala la Tanzania ya Kidijitali. Ukienda katika Ukurasa wa 14 na 15 wa Kamati, uchambuzi unasema kwamba, Kamati imebaini kwamba mapato mengi ya Halmashauri hasa yale yanayokusanywa nje ya mfumo hupotea bila kuingizwa kwenye akaunti za Serikali. Lakini pia Kamati inasema kwamba pamoja na jitihada na kazi inayofanywa na Mfuko wa Mawasiliano imebaini kuwa kuna ugumu wa kuyafikia baadhi ya maeneo kimtandao kutokana na uwezo wa kifedha au kutokana na kwamba, yale maeneo hayana vivutio vya kibiashara kwa hiyo, kampuni za kibinafsi haziwezi kujenga minara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunataka tuongeze mapato. Kwamba hoja ya kwanza, ili tudhibiti upotevu wa mapato lazima tuwe na mifumo ya kidijitali lakini *at the same time* hatuwezi kuwanayo kwa wakati kwa sababu, gharama za kujenga minara na hiyo miundombinu ni kubwa mfuko tu peke yake hautoshi. Kwa hiyo, kamati imesema nini? Kamati imeshauri kwamba, pawepo na vivutio maalum vya ki-kodi kwa ajili ya ujenzi wa minara na uendeshaji kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, wakati kamati inashauri hivyo nataka nikupe *contradiction* iliyopo. Kwa mfano kwa wenzetu nchi jirani hapa *East Africa*, kwa mfano Kenya ukijenga huo mkongo kwa urefu wa kilometa moja Serikali ina-charge dola 50, yaani ukipitisha katika ile *road reserve* au ile *open space* ambayo ni ya jiji,

10 NOVEMBA, 2022

wenzetu Uganda wanatoza dola 30, Rwanda kwa sababu wanavutia zaidi wanatoza dola 0, sisi tunatoza dola 1,000 kwa kilometa moja ukitaka kujenga ile *fibre*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaweza ukaona, wakati huku tunapendekeza nafuu ya kikodi kumbe sisi wenyewe bado kuna baadhi ya *charges* zinaweza kutusaidia kupunguza hizi gharama ambapo mwisho wa siku itasaidia kupunguza hata haya malalamiko ambayo kila siku tunamlilia Mheshimiwa Nape kwamba, “punguza bando, gharama ni kubwa.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile haitoshi, unapopitisha miundombinu ya maji kwa Kilometa moja, unalipa wastani wa Dola 50. Ukipitisha *Sewage system* Dola 50, ukipitisha *wire overhead* Dola mbili, ukipitisha *cable* Dola 50, ukipitisha miundombinu ya gesi na *oil* Dola 50, lakini ukipitisha *fibre* unatozwa Dola 1,000. Kwa hiyo, kama unataka tuwezeshe hii mifumo ili kudhibiti upotevu wa mapato na kwenda *online* na hii Tanzania ya kidijitali, maana yake ziko taratibu, sheria na kanuni, na ni lazima kwanza tuweze kuzipitia hata kabla hatujaanza kufanya unafuu wa kikodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuoneshe faida; kwa mfano, *BRELA* toka walipoenda *digital*, makusanyo yao mwanzoni yalikuwa Shilingi bilioni 11 kwa mwaka. Mwaka uliofuatia wakakusanya Shilingi bilioni 18, sasa hivi wanakusanya mpaka Shilingi bilioni 29. Nikufahamishe, leseni hizi za biashara za halmashauri, kimsingi vile vitabu vinatolewa na *BRELA*. Halmashauri A inaweza kupewa vitabu viwili, ikaenda kutengeneza vitano, ndiyo maana kunakuwa na upotevu ambao Kamati imesema. (*Makofi*)

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mwisho wa siku ni lazima tuiwezeshe Serikali na Wizara ya Mheshimiwa Nape ili kusudi huu mkongo wa Taifa ujengwe hata kwenye maeneo ambayo hayana vivutio kibiashara, tuweze kuwa na miundombinu ambayo itatuwezesha kukusanya mapato kwa njia ya kidijitali ili hayo mapato yatusaidie kujenga miundombinu ya elimu, madarasa, vituo vya afya na gharama nyingine kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baada ya kusema hayo naona kengele imelia, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasamu, atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, ajiandae.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Leo naelekeza mchango wangu katika maeneo mawili. Maeneo hayo ni suala la Wizara ya Ujenzi na suala la Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Mapinduzi kilitoa Ilani yake ya Uchaguzi yenye kurasa 303 ambayo mimi ni mwanachama wake na ni Mbunge wa Jimbo la Sengerema kupitia Chama cha Mapinduzi. Ilani hii inanipa nafasi ya kulinda yaliyomo kuhakikisha yanatekelezwa ili Chama changu kiwe salama pamoja na mimi. Ilani hii ya uchaguzi Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni miongoni mwa watu walioiandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa tisa wa Ilani yetu ya Uchaguzi una maneno mazuri sana, unasema katika aya ya 12, “Mapinduzi ya uchumi kwa maendeleo ya

10 NOVEMBA, 2022

watu.” Maneno mengine pale yako hapo. Mheshimiwa Waziri ataenda kuuangalia. Kwa hiyo, mpango wowote atakaokuwa anauandaa lazima basi akaangalie ukurasa huo wa tisa. Tukitoka katika eneo hilo sisi watu aina ya Tabasamu huwa hatukubali, lakini kwa sababu mambo yaliyoelezwa pale yana upana mkubwa katika Taifa hili, Mheshimiwa Waziri atakwenda akaangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naanza mchango wangu. Wizara muhimu sana katika nchi hii kwenye ukuaji wa uchumi ni Wizara ya Ujenzi. Kwa ukubwa wa miradi iliyopo katika Wizara ya Ujenzi tunazo kilomita za lami ambazo zinaunganisha barabara zetu kuu za Taifa, barabara zetu za Mkoa. Wakati huo huo tuko na shughuli za kupanua Bandari, kutengeneza Bandari mpya, kutengeneza reli pamoja na viwanja vya ndege. Kazi hii kubwa inafanywa kwa maono ya Mheshimiwa Rais ambaye anachukua katika tafsiri ya mpango wa miaka mitano. Sasa tukija katika mpango wetu huu wa bajeti yetu, ni kwamba lazima tukaangalie mpango huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina kazi nyingi. Mchango wangu leo nataka kutoa ushauri tu kwa mamlaka kwamba sasa imefika wakati ili tukatekeleze miradi hii, tunatakiwa tuwe na kitu kinachoitwa *contract management* tukahakikishe kwamba lazima tukazigawe Wizara hizi zipate ufanisi. Tuwe tuna Wizara ya Uchukuzi, wakati huo huo tuwe na Wizara ya Ujenzi kwa sababu miradi hii iliyopo ili twende 2025 imetekelezwa. Kwa kuwatumia Manaibu Waziri halafu Waziri mmoja ambaye yuko safari, hawa wanashindwa kutoa maamuzi, hili jambo linaweza kutuchelewesha. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti kama Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ushauri wangu ni kwamba hili tuliangalie. Siyo vibaya kuwa na Wizara kwa sababu matirioni ya fedha yanaenda huko Wizara ya Uchukuzi. Sasa hivi tuna reli, tuna bandari, tunataka tukuze bandari. Leo mzigo unaopokelewa bandarini unasafirishwa, na kusafirishwa kwa njia ya reli ni asilimia mbili, kwa njia ya barabara asilimia 98. Hili ni jambo la hatari sana. Sasa hili tunaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha akaliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Shirika letu la Reli lipewe *exemption* ya mafuta likajiendeshe lenyewe. Mnakwenda kuwapa *exemption* wawekezaji wa nje, mnashindwa kulilinda Shirika lenu la Reli mkawapa *exemption* ya mafuta nao wakaagiza mafuta yakapita hapa zero zero wakapata faida kwa ajili ya kwenda kutanua uchumi unaoelekea huko pembeni kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la nishati kwa miradi iliyopo ya TANESCO na REA. Pamoja na kuwa na miradi mikubwa kama hiyo ya TANESCO, mabwawa ya Mwalimu Nyerere, miradi tuliyonayo zaidi ya ishirini na kitu ambayo inaandaliwa kwa ajili ya kupata umeme wa maji na gesi; lakini ukiangalia usambazaji wa umeme, kuweza kuwafikia wateja, tunaomba Mamlaka kwamba sasa umefikia wakati tuwe na Wizara ya Mafuta na Gesi na tuwe na Wizara ya Nishati ya Umeme *(steamer)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo maombi yangu leo kwa Watawala. Ahsante sana, nakushukuru kwa muda huu.

10 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, na Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, ajiandae.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na mpango aliouleta. Pia naipongeza Serikali kwa ujumla kwa kuendelea kusimamia bajeti yetu vizuri ambayo tuliipitisha mwaka wa fedha unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali, nimeona kwenye taarifa ya utekelezaji tayari mmelipia ndege tano, na katika hizo ndege tano, ndege moja ni kwa ajili ya mizigo. Ninaipongeza sana, na hii inatukumbusha kwamba uchumi tunaokwenda kuupigania ni uchumi ambao hakuna namna, lazima kama tunataka kukuza utalii tuwe na ndege za kutosha. Juzi tukio la kuanguka kwa ndege kule Bukoba, linatupa picha kwamba kama nchi tunapaswa kuwa na a *very strong airline* ambayo inaaminika na yenye ndege ambazo watu wanapokuja Tanzania wana uhakika nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi tunachangia hoja za Kamati juzi, mchangiaji mmoja alisema anashangaa kuona Shirika limewekeza Bima fedha nyingi *compared* na *Precision Air*. Sasa *factor* namba moja ndiyo hiyo kwamba Shirika letu lina ndege mpya nyingi na pengine ndiyo sababu na tahadhari ambazo zimechukuliwa zinaweza kutufundisha kuwa na Bima nzuri zaidi yanapotokea majanga. Mheshimiwa naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo nataka kulizungumza haraka haraka, huko nyuma tulipiga kelele sana kuhusu *blueprint* na ikazungumzwa sana kwenye *level* ya juu, lakini hii *blueprint* nadhani imekomea kwenye *level* za juu na haijatafsiriwa kwenye halmashauri zetu. Mwenyekiti wa Kikao cha wafanyabiashara kwenye Wilaya ni Mkuu wa Wilaya, halafu *DED* ni Mjumbe (mtu wa kawaida), lakini *DED* ndiye anaye-*deal* na wafanyabiashara. Kwa hiyo, naomba Serikali iiteremshe hii *blueprint* kule chini ili ikasaidie kutafsiri tulichokiwaza wakati tunaianzisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka kuzungumza hapa kwa haraka ni utalii. Kwenye eneo hili nazungumza eneo moja tu. Miaka yote ya nyuma nimeangalia bajeti ya Mheshimiwa Waziri, tumetoka kwenye makadirio ya Shilingi trilioni 41, tumekwenda kwenye Shilingi trilioni 43. Tunahitaji kubuni maeneo ambayo tutapata fedha nyingi. Kuna eneo moja ambalo tunaweza tukalifanya vizuri vikiungana mkono na ndege zinazokuja na huu ni utalii wa mikutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwenye michango yangu muda fulani kwamba utalii wa mikutano siyo kama wa watu wanaokuja kwenye *holiday tourism*, hapana. Ila ni lazima tuwe na kitengo cha kufanya *lobbying* kuvuta mikutano mikubwa ije Tanzania. Bila kufanya hivyo, tutaisikia tu mikutano mikubwa inafanyika nchi jirani, halafu sisi hatuwapati hao watalii tunaowazungumzia. Kwa hiyo, sasa lazima Serikali ifanye jambo hilo na ianzishe sasa kwa bidi kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo nataka kuzungumza sasa kwa kina kidogo ni uvuvi. Nimeona

10 NOVEMBA, 2022

Serikali imetenga eneo la uvuvi, nami nataka kusema kwamba mpaka leo bado hatujatumia vizuri uwepo wa Ziwa Victoria na bahari. Nilikuwa naangalia takwimu za Wizara, nikaangalia *trend ya export ya Nile page*, ukiangalia kwenye *latest report* pamoja na ukubwa wa ziwa tulilionalo, tulipata dola 132,000 ambazo ni takribani kama shilingi bilioni 300 za Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jirani yetu ambaye anamiliki asilimia saba mpaka tisa alipata karibu shilingi bilioni 400 hadi shilingi bilioni 500, maana yake hatujatumia vizuri. Baharini, huku hali ni mbaya zaidi. Pamoja na ukubwa wa *territorial* na maji tuliyonayo yote yale, tuliuzua nje thamani ya fedha zisizozidi dola 40,000 na Serikali ikapata kodi ya dola milioni 62; na hizi ni taarifa *latest* kutoka Wizara yenyewe. Naangalia hapa shida iko wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, hatujafanya uwekezaji wa kutosha. Ni kweli Waziri amesema tunatenga fedha kwa ajili ya kujenga meli baharini, lakini *it is very scientific* kwamba meli ile yenyewe tu peke yake haiwezi kutuongezea mapato. Kwa sababu Meli ambazo zinaweza kutuongezea mapato ni lazima ndani ya muundo wenyewe wa meli mle ndani iwe na miundo ya kufanya *processing*, kufanya *parking*, *freezing* na unapovua samaki unapata *bycatch* nyingi. Kuwe na mfumo wa kutoa zile *bycatches* lakini na *link* ya masoko. Naangalia Serikali inataka kufanya hiyo biashara, itaweza? Tutaweza kweli ku-*breach* hiyo *gap* tunayoifikiria? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tulikuwa na TAFICO, nami wakati nasoma *fisheries* nilifanya *field TAFICO*. Kwa nini ilikufa? Ni kwa sababu Serikali ilifikiri ikiwa

10 NOVEMBA, 2022

na meli yake inaweza ikafanikisha kupata mapato ya uvuvi baharini, lakini ni jambo lingine kabisa. Sisi tunge-*invest* kwenye kuhakikisha kwamba tunapata teknolojia *latest* ikawawezesha Watanzania ambao wanavua samaki Ziwa Viktoria na baharini, kuwa na teknolojia ambayo ni *latest* wakaweza kuvua kuhifadhi, ku-process na kutafuta masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alizungumza mtu mmoja hapa juzi kwamba kuanzia Tanga mpaka Mtwara hakuna kiwanda cha samaki. Ukitengeneza meli za Shilingi bilioni 40, ukanasa samaki kule tani 60, utauza raw, utapeleka Soko la Kariakoo, na kadhalika, ili uweze ku-*transform* fikra za kufikiri tukapata fedha za kigeni. Kwa sababu lazima uwe na viwanda na viwanda havijengwi na Serikali. Tuwe na Kiwanda kikubwa kinachoweza kuprocess Samaki, kinachoweza kutafuta masoko nje; na masoko ya samaki ni *very competitive*. Sisi kwenye *Nile page* tunapambana na Kenya, Uganda na Tanzania, lakini *always* Tanzania bei yetu ni ndogo kuliko hizi nchi nyingine. Kwa hiyo, lazima tufikirie ku-*invest* peke yake na hizi meli kubwa hakutatusababisha tuongeze mauzo ya nje, jambo ambalo nadhani ni la msingi sana kwenye fedha hizi tunazowekeza, kwamba lengo letu ni kuongeza mapato na kuongeza wigo wa bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, atafuatiwa Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, ajiandae.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia. Nami leo

10 NOVEMBA, 2022

sitahangaika na mambo makubwa sana ya Kitaifa, bali nitaenda kwenye mambo ya kawaida ambayo yatatusaidia kusonga mbele kama jamii. Nakubali na naipongeza Serikali, na ninajua kinachoisukuma Serikali kwa sababu tunayo matatizo mengi, kwa hiyo, kila hatua inayofanyika ina ahueni upande fulani. Katika mpango, yale maeneo matano ya kujikita, kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza biashara na uwekezaji, kuchochea maendeleo ya watu na mwisho kabisa kuendeleza rasilimali watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa upana wake, huo ndiyo uhalisia wa yale ambayo tunayahitaji kama nchi. Tunachokikosa ndani, ni namna tunavyoweka vipaumbele. Hii nikawaida, ukiwa na matatizo mengi; kwa mfano, una njaa, wakati huo huo una kiu, wakati huo huo kichwa kinauma, wakati huo huo hujaoga, kila *solution* unaiona ni ya maana, lakini kuna *solution* ambayo ikija itasaidia hizo nyingine kuweza kushughulikiwa. Yaani kuna vile vipaumbele. Kuna mzungumzaji mmoja alisema tunakosa ufungamanishaji wa mipango ya Wizara moja na Wizara nyingine. Wengine wakaja mpaka na mpango wa kurudisha ile *Big Result* wengine wakasema tuwe na Tume ya Rais ya ufuatiliaji wa matokeo, lakini mimi naona haya yote ni mle.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukurasa namba 19 wa hotuba ya Waziri, ameongelea sekta binafsi ameweka na takwimu. Sote tunajua kwa hawa watu wote milioni 61 Serikali haijaajiri hata milioni moja. Kitu kinachoweza kuajiri watu wengi ni sekta binafsi. Sasa ni nini kifanyike kwenye sekta binafsi ili iajiri? *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimwa Mwenyekiti, sasa kwenye sekta binafsi, ukiangalia leseni unazotakiwa kuwa nazo kufungua biashara, mfano biashara ya hoteli; kuna leseni sijui, kuna TALA kuna OSHA, kuna TRA hapo, kuna fire kuna NEMC, TFDA, TBS sijui huko halmashauri ukiacha leseni, kuna leseni za vileo, halafu zote unakuta mtu amezi-frame, ameziweka kwenye ukuta, hata nafasi ya kuweka decoration hakuna. Kwa nini usiwe na mfumo ambao unapoenda Manispaa, hivi vitu vingine vyote vimeunganishwa? Kwa hiyo, unalipia tu una-tick na inakuwa ndiyo precondition ya leseni kutoka badala ya kila mamlaka kujichukulia jinsi inavyotaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kubwa zaidi ni procedure ya kuzipata hizo leseni. Kwa mfano, NEMC yenyewe, process yake na gharama za ile Certificate ni shughuli hasa! Kuna baadhi ya Taasisi huelewi; wanakuja watu wa OSHA na Fire kwa pamoja, na wote wanaangalia mfumo wa umeme, wote wanaangalia uokozi kama ikitokea dharura, wote wanachukua hela na wote wanaongozwa na sheria tofauti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, OSHA inatoa namna ya kupata leseni yao. Ukipata inasema, ulipe baada ya siku 30. Ila ukienda kwenye kanuni iliyotungwa na Waziri ni kwamba baada ya siku 30 kama hujalipa unachajiwa asilimia tano ya lile deni kila siku. Maana yake ni nini? Huyu mtu anayejiipanga amechelewa kulipa unam-discourage kabisa hata kulipa, lakini je, hizi shughuli za OSHA zinafungamana moja kwa moja na uzalishaji wa hizi biashara tunazoziongelea, jibu ni hapana.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha huu usumbufu kwenye biashara, ukienda kwenye Deni la Taifa ambalo tumeambiwa limefanyiwa *auditing* limeonekana tuna uwezo nalo, ni nini kinaelekeza Serikali ikope kiasi gani na kwa ajili gani? Hatuna, kwa sababu hatuna yale maeneo ambayo tumeyatenga. Kwa mfano, hivi kweli katika nchi hii ambayo tunataka wafanyabiashara, tunataka wawekezaji wa nje, bado maji ya kunywa ni shida kwa watu, maji ya kuoga ni shida kwa watu, bado umeme ni shida kwa watu huyu mwekezaji anakuja kufanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni nchi ambayo tuko katika Maziwa Makuu, tuna mito ya kutosha, tuna kila *resource* iliyoko karibu na sisi. Kwa nini hili Deni la Taifa tusiweke dheria ambayo inasema kwa miaka mitano mkopo wowote ambao tutachukua uelekezwe asilimia fulani kwenye maji na umeme kwa miaka mitano mpaka hilo tatizo liishe. Tujue kabisa kwamba umeme na maji sio tatizo tena kwetu ili tuwaite hao wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Ardhi, ni kweli tuna rasilimali nzuri sana ya Ardhi, nafikiri sisi tuko vizuri sana uki-*compare* na wenzetu wa Afrika Mashariki ukiacha Congo. Hata hivyo kwa jinsi tunavyotumia hii ardhi hatuna maeneo tuliyotenga kuendana na *advantage* za kijiografia kwa ajili ya matumizi fulani. Sehemu ya makazi iwe makazi, kilimo iwe kilimo, kila mahali wanafanya jinsi wanavyoona. Nitatoa Mfano Mkoa wa Kilimanjaro, eneo lililokuwa zuri zaidi kwa kulima kahawa ni kule chini pembezoni ya mlima lakini huko ndiko tumejenga zaidi. Eneo lile la tambarare ambalo hakuna mvua, hamna udongo wa *volcanic* tumepaacha ndiyo kwa ajili ya mashamba ambayo yatanyeshewa na nini? Kwa hiyo hakuna Mpango wa Serikali unaosema maeneo haya

10 NOVEMBA, 2022

yatakuwa ni ya kilimo tu, maeneo haya yatakuwa ni ya kazi hii tu na mwisho wake tumebaki na *EPZ* zile ambazo tumeziweka kati kati ya miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *solution* niliiongelea juzi, mikopo chechefu ndani ya nchi. Ie mikopo chechefu tunavyoangalia sio kwa ajili tu ya zile biashara au zile benki kukosa hela, lakini inawapa watu umaskini. Mtu anakuwa na access ya kukopa kuliko uwezo wake wa kurudisha, maana yake ni kwamba atashindwa *manage* ile hela, ataingia kwenye madeni, ndio unaona kila siku mikopo yetu hailipiki. Nilisema ni rahisi kuwa na *system* ambayo itai-connect *TRA*, mahesabu ya wafanyabiashara, lakini ita-connect *NBAA* kama Msimamizi Mkuu wa Mahesabu lakini na hizo benki, yaani kwamba ukiangalia tu mtu anataka kukopa bilioni moja, ukiangalia kodi zake anazolipa kwenye biashara zake ina-*justify*, ukiangalia mahesabu ambayo amepeleka *NBAA* yana-*justify*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilivyo sasa hivi tunakuwa na vitabu vingi, yaani *NBAA* hao ambao ni *certified account* anatengeneza kitabu anaki-*certify* hicho ni kwa ajili ya *TRA*, anatengeneza kingine anaki-*certify* hicho ni kwa ajili ya benki na kingine hata ukitaka cha kwako cha nyumbani anakutengenezea. Sasa sio mfumo, hatuendeshi uchumi kwa namna inyotakiwa. Kwa hiyo nashauri sana hiyo mifumo iunganishwe ili iweze kuleta tija kwa hawa wafanyabiashara na hata hizo taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni huduma za uokozi, hii lazima tukubaliane. Ni kichocheo pia kwenye uchumi hasa kwa wawekezaji wa nje. Nakumbuka *at one time* Dubai waliendelea sana wakiwa

10 NOVEMBA, 2022

na maghorofa makubwa, wakawa *challenged* na *fire and rescue services* waliyokuwa nayo. Hawakuwa na *fire* ambayo inaweza ikafika ghorofa ya 100 wakati wakiwa na hayo majengo. Sina hakika hata sasa hivi kama Dar es Salaam tuna gari la *fire* ambalo katika zile ghorofa tulizonazo pale, moto ukitokea juu kuna *mechanism* ya kuuuzima. Hiyo ni kichocheo cha namna ya kuwakaribisha wawekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda wangu umeisha, nakushukuru na naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt Thea Medard Ntara, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga na, Mheshimiwa Patrick Alois Ndakidemi ajiandae.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mtanisamehe sana leo sauti sio nzuri kama ile mliyoizoea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita, kitendo cha kutoa trilioni 1.3 ziende kwenye miundombinu, imesaidia sana sana kwa madarasa na sasa tunaamini kweli watoto wakiingia kwenye madarasa yetu yapo na yamekaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo niombe Waziri wa Fedha kwenye Mpango tuone sasa tunaongeza bajeti kwenye *research*. Kwenye ile mikopo ya wanafunzi tusipoongeza fedha, *research* zetu zitakuwa za kulipua. Pia tuongeze bajeti kwenye *COSTECH* wafanye *research* za uhakika. Nalisema hilo leo nalirudia ni mara ya nne; elimu ni *research*, afya ni *research*, uvuvi ni *research* na kadhalika. Haya yote tunayozungumza humu

10 NOVEMBA, 2022

ndani bila kujikita kwenye *research* za uhakika na kutoa *facilities* za uhakika kwenye *research* itakuwa ni kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi mlimsikia Mheshimiwa Rais akizungumzia suala la *family planning*. Alizungumzia suala la *family planning* na kusema sasa twende na *family planning* tupunguze lile zoezi ili tusiwe tunaongezeka kwa mtindo ambao hautasaidia kuleta maendeleo. Alilisema hivyo kwa sababu gani? Tayari takwimu za *research* ndizo zilisaidia Mheshimiwa Rais akaona kwamba huko tunakokwenda ni kubaya. Kwa hiyo ushauri huo aliutoa kwa sababu ya ripoti hizo za *research*. Ndio maana nasema *research* ni muhimu katika kila nyanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kila Wizara hapa wana zile *basic research* yaani kila Wizara ina kaeneo ka *research* wana *basic research*, lakini niwaombe washirikiane na Vyuho Vikuu ili wafanye *research* za uhakika, ziwe *research effective*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nachangia kwenye eneo la kilimo. Narudia kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita kwamba anaendeleza ule mpango wa kuwapeleka Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wengine wa Wizara Japan katika kusoma ile *Program* ya *Local Government Reforms*. Sasa kwenye hiyo *program* wenzetu kule wanaangalia namna gani kila eneo linaweza likawa na jambo moja la kuwaletea uchumi wananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *program* ile inaitwa *OVOP, one village one product*, sisi tujipange kwenye *one district one product* au *one region one product*.

10 NOVEMBA, 2022

Mwekezaji au mfanyabiashara akija Tanzania akisema nataka asali nzuri unamwelekeza sehemu. Vile vile sio asali nzuri mwingine anasema nenda Lindi, nenda Singida, nenda Tabora hiyo haitawezekana. Kwa hiyo tukiwa na *program* ile tukai-*develop* hapa kwetu, tukai-*copy*, ndio italetu ufanisi na yale mafunzo yetu tunayokwenda huko yatakuwa yanaleta tumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mazao hapa wenzangu walishaongea, unakwenda mahali ujue kabisa hapa nakwenda kwa ajili ya kahawa, nakwenda mkoa huu kwa ajili ya alizeti, nakwenda mkoa huu kwa ajili ya mahindi, lakini sitapenda kuzungumza nakwenda mkoa huu kwa ajili ya tumbaku. Hilo nimemwambia Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, hilo hapana. Kwa hiyo tujipange hivyo, twende na ile *program* ili tusaidie. Wawawezeshe sasa, wamerudi kwenye mpango Mheshimiwa Waziri awawezeshe sasa tu-*practice* ile ili kwa kweli tuwe na zao moja, sio lazima zao la kupanda hata madini mbalimbali, mwekezaji au mfanyabiashara akija ajue nakwenda mahali fulani napata kitu fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, katika kufanya hivyo niombe katika Mpango, hivi ni lini wakulima hawa wataendelea kulima kwa jembe la mkono? Niombe Mheshimiwa Rais anapotafuta fedha hizi nyingi na zinapoingia katika Mawizara tunakuja hapa tunalalamika fedha nyingi zinapigwa. Hebu tujipange sasa hizo fedha zisipigwe, tuone kama tunaweza kufanya *pilot study* kwenye mikoa michache, vijiji vinunuliwe matrekta, kijiji kimoja matrekta matatu, tutakuwa tunafanya kitu cha maana. Tunataka uchumi wa mtu mmoja mmoja, lakini hili jembe la mkono Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa Mwigulu hatufiki mbali.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujaribu, hivi hatuwezi kila kijiji kikapata trekta tatu? Kwani trekta tatu ni bei gani? Waweke kwenye mpango kwani hawalielewi hili? Hebu waweke kwenye mpango jamani tubadilishe hiki kilimo. Yaani hii mipango tutaiongea lakini itakapokuja wakati wa utendaji kama mtindo ni ule ule wa jembe la mkono, nakwambieni tutakuwa na mipango lakini utekelezaji wake ni zero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kama nilivyosema, tuone kabisa kwamba sasa kwenye mpango huko zao la tumbaku Waziri asiliweke, kama wanataka kuendelea kulima tumbaku, wawachague wale wakulima wakubwa wanaofaidika, wa-*deal* na hao wakulima wakubwa, wakulima wadogo wa tumbaku hawapati faida yoyote, Mheshimiwa Bashe analijua hilo, hawapati faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale *verifiers* usipowapa pesa, usipowahonga, tumbaku yako kila siku itakuwa *grade* ya chini, sasa kuna faida gani? Wawawezeshe wakulima walime mazao yale yanayoweza kuwapa faida, mazao mbadala, tumbaku tuipige vita, tumbaku haiwasaidii wakulima wa chini.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe mzungumzaji taarifa, ni kweli faida inakuwa ndogo kwa sababu hata kwenye masoko kumekuwa na utaratibu wa kufanya *central market*

10 NOVEMBA, 2022

ambazo zinafanyika mjini badala ya masoko kufanyika kwa wakulima walioko kwenye maghala yao vijijini.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara unapokea taarifa hiyo?

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili na namwomba anisaidie tuendeleo na kampeni ya kuliondoa na kulipunguza kabisa hili zao la tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya ajiandae.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangaia katika Mpango huu wa Serikali. Mchango wangu utajikita katika maeneo matatu kama muda utanitoshia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze na suala ambalo Serikali yetu hasa ilani ilitoa kwamba inataka kufikia ajira milioni nane kwa ilani hii tunayoendelea nayo. Hata hivyo jambo hili linakuwa gumu sana kutekelezeka kwa sababu vyo vyetu vimejikita sana katika kuzalisha watu wa utawala, mambo ya kijamii lakini halijajikita katika kuzalisha watu wa *production*. Watu wa *production* ni watu ambao wamesoma mambo ya sayansi. Kwa sababu ukisema kilimo ni sayansi, kufuga ni sayansi, utawala tayari tuna watu wengi sana wa

10 NOVEMBA, 2022

kutosha. Watu wa uhasibu, leo taasisi kubwa kama hii ya Bunge inahitaji Wahasibu labda wawili au watatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli unapotaka kwenda kwenye *production*, kama unataka kufuga lazima uwe na watu wengi ambao wamesomea na wana uwezo. Ukitaka kulima ardhi hii ni kubwa na inahitaji watu wengi. Kwa hiyo, ningeshauri hivi vyuo vyetu vifike mahali viangalie *production* vinatoa watu wa aina gani katika vyuo vyao. Ukizingatia kwamba watu hawa wanakopeshwa mkopo na Serikali na inabidi walipe mkopo. Sasa kama ni watu ambao wanaweza kujjariri, ambao wanaweza kuzalisha ni rahisi kuwa-*trace* na kurudisha mikopo na watu wengine wakaendelea kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka huu mtindo wa *ku-copy*, sasa hivi ukiangalia *UDSM* na *UDOM* karibu *course* zote ni zile zile tu zinajirudia watu wa jamii, utawala na ndio nyingi. Kwa hiyo ningeomba mwelekeo wa vyuo vyetu uangalie kwamba unazalisha watu wa aina gani na hii itakuwa rahisi hata Serikali inapowakopesha fedha zile zirudi na uchumi wa nchi yetu kuweza kuchangamka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, lazima sasa niguse kwa mwajiri wangu ambaye ni wananchi wa Mkalama. Sasa hivi tunajenga barabara kutoka Manyara – Simiyu, barabara ya kimkakati kabisa. Barabara hii tunapojenga na tayari imetangazwa ni vizuri tukajenga katika mtazamo wa kibiashara pia ili Serikali iweze kukusanya mapato. Zipo baadhi ya barabara ndogo sana ambazo zikiwekwa pamoja na mradi huu ambao ni *feeder roads* zitasaidia sana kufanya barabara hii ichangamke kuleta mapato. Ikichukua barabara kutoka

10 NOVEMBA, 2022

Iguguno inayopita Mkalama kwenda kuunganisha na barabara hii kule Sibiti na ukichukua barabara inayotoka lyongero inakwenda kuunganisha na barabara hii kwenda kule Haidom, barabara hizi zinaunga barabara kubwa ya katikati ya nchi inayotoka Dar es Salaam mpaka Mwanza zinaunga na barabara hii ambayo itakuwa ni kubwa katika *corridor* upande wa kaskazini na huko ndiko kuna mbuga za wanyama na kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo utaona kabisa wananchi wanaotoka Nyanda za Juu Kusini watapita hapa katikati kwenye utalii wa ndani na kwenda kuchangamsha uchumi wetu kwenye mbuga za huku. Kwa hiyo utaona barabara hizi zitakuwa zimekaa kiuchumi zaidi na zitaleta faida kwa nchi yetu. Kwa hiyo ushauri wangu, kwa sababu sasa ujenzi wa barabara hii umeshatangazwa na unajengwa kwa *EPC+F*, basi na barabara hizi wataalam wetu waziunganishe katika barabara hii, hivi vipande viwili vidogo vya barabara nilivyovitaja, viwe kama *feeder road* ili barabara hii iwe na faida zaidi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nataka nisemee kwenye suala zima la mawasiliano. Mawasiliano ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. Kitu kinachonishangaza sana, kaka yangu Mheshimiwa Nape juzi ameleta hapa Muswada wa kulinda habari binafsi, tukampitishia Muswada mzuri kabisa, lakini nataka alete tena Muswada mwingine wa kuhusu kulinda haki zetu. Mashirika haya yamekuwa yakituibia, hivi ni kwa nini bando zina-*expire*? Simu ni ya kwangu, nimenunua bando kwa fedha yangu, halafu unanilazimisha nitumie kwa muda unaotaka wewe, hii ni kwa nini? *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni sheria, basi iletwe hapa tuibadishe, kwa sababu tunawaibia wananchi. Anatafuta fedha kwa jasho, ananunua simu, anataka awasiliane ananunua bando limsaidie, anaambiwa ndani ya siku saba limeisha. Hivi hii sheria ni ya nchi gani? Kama ni sheria tunaomba ije hapa, kwa sababu tunaibia hawa wananchi na tunaibiwa huku tunaona, kwa nini unipangie kutumia bando langu? Mimi si ndiyo najua umuhimu wa mawasiliano ndiyo maana nikanunua lile bando la wiki moja! Kama nimeamua kulitumia taratibu, wiki moja imeisha nimeweka akiba kwa nini wewe ulikate? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningekuomba sana kwa hili uwe mkali, utuongoze hili jambo la kuibia wananchi wa Tanzania lifikie mwisho...

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Francis Mtinga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba tu nimpe taarifa kaka yangu na Mbunge wangu wa Mkalama Ndugu Francis. Kwanza, si sawa kutoa tuhuma za jumla kwamba kuna wizi. Suala la bando nimesimama hapa mara kadhaa kulieleza. Bando ni huduma ya ziada ambayo ina masharti ya muda, ndio maana kuna bando la siku, la wiki, mwezi na kuendelea. Ukitaka lisiishe kwa muda upo utaratibu wa kutumia *main tariff* ambayo

10 NOVEMBA, 2022

ukiweka mpaka utakapoimaliza hata kama ukikaa nayo kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri, ukienda kwenye utaratibu wa kununua tiketi za kusafiria; kuna tiketi unainunua ya mwezi, unainunua tiketi ya wakati mmoja. Ukinunua ya mwezi ukasafiri mara moja, mwezi ukaisha, huwezi kwenda kudai kwamba siku 29 sikuitumia, kwa sababu uliwekwa kwenye mwezi, ndio utaratibu. Nadhani ni suala tu la uelewa, uelewa ukikaa sawa hili jambo halina matatizo hayo. Hofu yangu ni kwamba tukitumia Bunge kushutumu uwekezaji mkubwa kiasi hiki kwamba kuna wizi, nadhani tunakwenda mbali sana kwenda kuharibu huduma ya mawasiliano. Iko mifano mizuri na tukitaka tunaweza kuweka semina hapa tukaelekezana namna ya kufanya, lakini tusituhumu kwamba ni wizi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Nadhani Mheshimiwa Mbunge yeye amesema, hicho ulichosema ni utaratibu. Ni Sheria au ni utaratibu wa aina gani? Ndiyo alichokuwa anakisemea pale Mbunge, ili kama ni utaratibu ambao unaweza kubadilishwa nadhani ndio hoja yake. Kama Bunge linao uwezo wa kubadilisha, ndio ufafanuzi wako utueleze hapo. Bunge linao uwezo wa kubadilisha? Kama huo ni utaratibu je, uko kisheria au ni jambo ambalo haliwezekaniki? Kwa hiyo tujue ndiyo haliwezekaniki. Ndiyo ilikuwa hoja ya Mheshimiwa Mbunge pale.

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni utaratibu wa kawaida kabisa wa kibiashara, ndio maana bei ya bando ni ndogo ukilinganisha na *main tariff*. Hata unapopewa

10 NOVEMBA, 2022

yale masharti yake unapoenda kuchagua unaelekezwa kwamba hii unayoichagua itakwisha baada ya wiki moja. Ukitaka ambayo inaisha baada ya mwezi mmoja chukua kwa bei ya juu zaidi. Ni utaratibu wa kawaida wa kibiashara wala sio suala la sheria.

MWENYEKITI: Sawa, hilo limeeleweka. Sasa maadam umesimama, Mheshimiwa Mtinga muda wako unalindwa. Maadam umesimama kuna hawa ambao wanasema Bando MB moja, GB moja, halafu badala ya moja anatoa 800, huyo nae anaiba au yeye haibi na yeye ni utaratibu? *(Makofi)*

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali zuri sana. Imetokea kesi juzi na nadhani watu wengi mmeisikia imesambaa mtandaoni, nadhani ndiyo ambayo unai-refer labda na zingine za aina hiyo. Kilichotokea ni nini? Kumekuwa na kila baada ya miezi mitatu wanaruhusiwa watoa huduma kuleta mapendekezo ya mabadiliko ya hizi bando kwa sababu ni huduma wanazitoa wanaweza kuamua kupandisha kushusha kuongeza magroup, kilichotokea juzi wamepandisha baadhi ya vifurushi lakini kwenye bango lao wakawa hawaja badilisha kwamba wamepandisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikitokea mtumiaji huduma ameenda kununua kwa kutumia bango lilikuwa hailjabadilishwa sawasawa na ukienda kwenye kituo cha mafuta ukakuta kuna bei imeandikwa kabla hajabadilisha kumbe imeshatangazwa mabadiliko imeanza kuwa *effective* wakati kwenye bango haijabadilishwa ndiyo ikaleta malalamiko yaliyotokea.

10 NOVEMBA, 2022

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeiagiza TCRA kuwaita watoa huduma hawa ambao hawakufanya mabadiliko kwenye bango lao ili tuchukue hatua zinazostahiki, hivi tunavyoongea wanaendelea na utaratibu nao wakikamilisha hatua zilizochukuliwa zitatangazwa.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri na tuwashukuru TCRA kwa kuwa na huo utayari. Siyo wote lakini yako mazingira ambayo yanashawishi wananchi kwamba wanaibiwa, si wote lakini yako hayo mazingira. Sasa mazingira ni kama haya ukishasema mtu anapata one *gigabyte* basi apate one *gigabyte*, kama humpi hiyo *gigabyte* basi ulipaswa uwe umesema na kwa utaratibu kawaida kabisa ni kwamba umemuibia kwa sababu yeye ameangalia tangazo na akanunua kwa tangazo lako. Kwa hiyo, mimi sijui kwa sababu umesema mnaendelea kuangalia ili mchukue hatua hizo hatua ziwarejesheshe wananchi kile kilichoibwa. Mheshimiwa Musukuma ulikuwa umesimama.

T A A R I F A

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilitaka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba pamoja na maelezo yake mazuri aliyoeleza, anavyosema huu ni utaratibu wa kibiashara na biashara ni kitu cha kawaida kwamba unapopandisha bei unapotoka kwenye mstari watu wanalalamika, sasa wanapolalamika nani wa

10 NOVEMBA, 2022

kuwasaidia? ni sisi Wabunge. Maelezo ya Waziri ni mazuri lakini bado hayajajibu ile hoja ya Watanzania wengi hasa wasiokuwa na uelewa kama wa kwake kwamba kuna wizi wa siku na matumizi ya simu.

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Waziri utapewa dakika zako baadae kuchangia haya mengine utafafanua wakati huo, ngoja Mheshimiwa Mtinga amalizie mchango wake.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa taarifa hiyo. Mimi bado naona kwamba kama utaratibu ni huo bado Bunge lako linahaja ya kutunga Sheria kuwalinda wananchi kuhusuiana na suala zima la matumizi ya bando, kwa sababu hata TANESCO tunanunua umeme kwa *Tarif one* na huo umeme ukifika unapata *unit 75* unapofika mwisho wa Mwezi hujazimaliza zile *unit* zako zinabaki unaongeza zingine zinaendelea kukusaidia, hata ving'amuzi. Kwa hiyo, ninaomba bado kuna haja ya kuja hapa tutunge Sheria ya kuwalinda wananchi wetu na bando zao, akinunua bando atumie mpaka liishe kama sivyo hiyo huduma waitoe wasiiweke kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee na mchango wangu katika suala zima la kumuunga mkono Rais wetu. Mama yetu anao mpango mzuri wa kutaka wakina mama wapikie gesi safi, gesi asilia kwa sababu wanaumia sana na kupikia mkaa na kuni. Vilevile nchi inaisha kwa kukatwa miti kwa sababu ya mkaa. Nchi yetu tumebarikiwa tuna bomba la gesi linalotoka huko limefika Dar Es Salaam, lakini Bomba hili bado halijaenea katika nchi hii. Kwa hiyo, niombe katika mpango bomba hili litoke Dar es Salaam sasa lisambae katika nchi, lielekee

10 NOVEMBA, 2022

Mwanza, Kigoma, Kaskazini, Arusha na kusini huku ili wananchi tuweze kutumia gesi asilia kwenye majumba yetu. Teknolojia ya magari sasa hivi inatumika, Dar Es Salaam sasa hivi magari karibu yote ya *uber* wanatumia gesi asilia

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilo moja ya gesi inakwenda mara mbili ya lita ya petroli na bei ya kilo moja ni karibu 1500 na huku petroli ni 3000 na kitu. Kwa hiyo katika mpango bomba la gesi liende likasambae hata kwa kipenyo kidogo sio sawa na kipenyo kikubwa sana kilichotoka kule kusini ili lisambae kwenye nchi ili tuweze kutumia gesi na tumuunge mkono Mama yetu kwa kuhakikisha kwamba tunatumia gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili litachangamsha uchumi kwa sababu miti itapona na tabianchi itabadilika kuwa *positive*, mvua itaongezeka mabwawa yetu yatajaa maji. Kwa hiyo hili jambo lina faida mtambuka lina faida kubwa sana kusambaza bomba ambalo tayari tunalo. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri katika mpango wako fikiria suala la Bomba kwenda Mikoani. Kama Mama anatoa Bilioni 100 kila Mwezi kwenye ruzuku ya mafuta anao uwezo pia wa kutoa fedha kwa ajili ya kujenga bomba ambalo litatuokoa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka tumuunge Mkono Mama yetu katika uchumi kwa kusambaza bomba wananchi wa Tanzania wafaidi bomba hili wakiwa bado hai na vizazi vijavyo pia waje wafaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme hayo kwa uchungu kabisa kwamba yakitekelezeka naamini

10 NOVEMBA, 2022

Watanzania wengi watafurahi. Ahsante sana kwa nafasi hii.(Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Patrick Aloyce Ndekidemya atafuatiwa Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, ajiandae.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nami nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuwasilisha vizuri Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2023/2024. Nianze pia kwa kutambua juhudi za Serikali ambazo inafanya kwa kuhakikisha kwamba miradi mbalimbali inatekelezeka ikiwepo miradi michache tu ambayo nitaitaja:

Tunajenga barabara, tunaboresha viwanja vya ndege, tunaboresha ununuzi wa ndege, kuna shule tunajenga, maji, barabara za vijini, ya Mikoani vyote hivyo ni kazi nzuri ambayo Serikali yetu inafanya. Kwa hiyo, niipongeze sana Serikali na niombe waendeleo kukusanya fedha ili hii miradi iishe ikamilike kama tulivyopanga kwenye mpango wa 2022/2023 tupate heshima yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita kwenye sekta ya kilimo mifugo na uvuvi. Nianze kwa kuipongeza Serikali na Bunge hili lako Tukufu kwa kuongeza bajeti ya kilimo kutoka Shilingi Bilioni 294 mpaka Bilioni 954 na ile ya Wizara ya Mifugo kutoka shilingi bilioni 168 mpaka Shilingi Bilioni 268 ijapokuwa imeongezwa Haba na haba hujaza kibaba siyo mbaya sana.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali, huu ulikuwa ni uthubutu wa hali ya juu kabisa kuongeza hizi bajeti za hizi sekta mbili tuendeleo kuhakikisha kwamba wanapokea hizi pesa ili yale mafanikio ambayo tunategemea wakulima wetu wayaone kule yaweze kuwafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu kwenye mpango nitaanza na kuongelea suala la utafiti kwenye vituo vyetu vya utafiti wa kilimo, ngoja nianze na kilimo. Tumekuwa na mikutano mingi na watafiti wa *TARI* na pia tumetembelea vituo vya utafiti *TARI*, tulichokiona kule kunasikitisha, miundombinu ya hivi vituo vya utafiti iko taabani. Tanzania tuna vituo vya utafiti 17 ambavyo miundombinu ya ofisi haijaka vizuri, ukienda kwenye maabara ni *almost* hazipo kabisa, ukija kwenye nyumba za kulala za watumishi haziko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali angalau kwa *TARI* wamewatengea Shilingi Bilioni 39 kwenye mpango huu wa mwaka huu na mambo yanakwenda vizuri. Wameongeza kutoka Bilioni 11 mpaka Bilioni 39. Kwa hiyo tunaishukuru sana Serikali. Niombe kwenye huu mpango kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara kwamba bila utafiti hakuna mahali tutakapokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi zimefanikiwa Duniani kupitia utafiti. Kwa hiyo, tukiwaongezea kwenye huu mpango Watafiti wetu pesa ya kutosha ili waweze kufanya utafiti wa kuzalisha mbegu. Utafiti wa kubuni mbinu bora za kuongeza tija kwenye kilimo tutafika mahali ambapo na sisi tutanufaika na utafiti wetu. Kwa hiyo, kwenye huu mpango niombe ikiwezekana walikuwa

10 NOVEMBA, 2022

wanasema wakipata Shilingi Bilioni 75 watu wa *TARI* wangefika mahali ambapo watafanya kitu ambacho kinaonekana. Kwa hiyo niombe tufikirie kuwasaidia watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni kwenye mpango wa pembejeo. Tunaishukuru sana Serikali yetu ambayo imeshawekeza pesa karibu Shilingi Bilioni 100 kwenye pembejeo za ruzuku hasa ya mbolea. Tunaweza tukatoa mbolea kwa wakulima wetu lakini kama hujawapa mbegu na viuatilifu anaweza asizalishe akafikia pale tunapotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali kwenye huu mpango mpya wahakikishe kwamba tunaweka pesa ya kutosha ili tuwapatie wakulima wetu mbegu, mbolea na viuatilifu ili uzalishaji uweze kukamilika kwa sababu bila hivi vyote vitatu kwenda pamoja nafikiri hatutafika mahali pazuri na kama pesa haitoshi ya ruzuku ninapendekeza kwamba tuwe na Mfuko maalumu tuipatie Benki yetu ya kilimo pesa ya kutosha ili waweze kupatia wakulima wetu mikopo nafuu, waweze kununua hivi vitu ambavyo haviwezi kutoka kwenye ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa tatu kwenye kilimo ni Kilimo cha Umwagiliaji. Kama sote tunavyoona mabadiliko ya tabianchi yamesababisha shida kubwa sana na kuna upungufu wa chakula karibia dunia nzima. Kwa hiyo, sisi kama Taifa tuna bahati nzuri kwamba tuna maeneo mengi na maji ya kutosha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara ya Kilimo kwamba ina miradi karibia 36 ambayo ipo inaendelea wanajenga skimu mpya. Niwaombe katika

10 NOVEMBA, 2022

mpango huu tuhakikishe kwamba tunajenga miradi ya umwagiliaji kwenye maeneo ambayo kuna maji ya kutosha ili tuweze kunufaika na hiki kilimo cha umwagiliaji, kikubwa napendekeza pia kwenye huu mpango waongezewe pesa za umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la Nne ni kilimo cha bustani, hivi karibuni tumezindua Mpango wa Taifa wa Kilimo cha Bustani, niombe kilimo cha mboga mboga ndiyo kitu ambacho kinaweza kikalikwamua Taifa letu kwa sababu mboga mboga zina bei mahali pote. Kwa hiyo, niombe Serikali kwenye huu mpango wahakikishe wanafuatilia ule mpango ambao umezinduliwa, mpango wa Kitaifa ili tuweze kutekeleza pamoja na tuhakikishe kwamba wananchi wanazalisha mboga na matunda ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa nne ni kwenye sekta ya mifugo na uvuvi. Nitazungumzia pia suala la utafiti kwenye hii sekta ya mifugo na uvuvi. Pale mifugo shirika linalo-*deal* na utafiti pale linaitwa *TALIRI*, kwenye mwaka wa 2021 walipokea Shilingi Milioni 522.5. Hizi pesa ni ndogo sana kwa watafiti wa mifugo kwamba hii pesa Milioni 500 na tunategemea tupate kitu kikubwa kwa hawa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TAFIRI*, watafiti wa samaki walipokea Shilingi Bilioni 1.7 mwaka huohuo ambao nimeutaja, angalau siyo mbaya sana lakini wenzao wa *TARI* mwaka huohuo walipokea Shilingi Bilion 11. Nashauri kwenye mpango huu Serikali ihakikishe kwamba hizi taasisi za utafiti za mifugo na uvuvi zinapatiwa fedha za kutosha ili waweze kutekeleza azma yao ya kuzalisha nyama ya kutosha, waweze kuzalisha ngozi za kutosha, maziwa ya

10 NOVEMBA, 2022

kutosha, kuku wa *broiler* wa kutosha na samaki wa kutosha. Tusipofanya hivyo tutakuwa hatuwatendei haki na tutakuwa tunawalaumu bure tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kwenye hii sekta ya uvuvi ni meli ya kufanya utafiti. Tuseme ukweli hawa watu wana-*operate* katika hali ngumu sana. Meli ya kufanya utafiti hawajanunuliwa ilishaagizwa lakini mpaka sasa hivi haijapatikana. Ninaiomba Serikali tujitahidi angalau tuwapatie hawa watu meli moja ili waweze kufanya utafiti kwenye Bahari Kuu, kule nina hakika kuna fedha nyingi sana ambazo Taifa linaweza kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle Mheshimwa Bakari Hamadi Bakari, ajiandae.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi niweze kutoa maoni yangu katika mapendekezo ya mpango wetu wa mwaka mmoja. Moja kwa moja naunga mkono mapendekezo ya mpango pia naunga mkono maoni ya Kamati yangu ya Bajeti ambayo na mimi ni mmoja wa wanakamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimshukuru Mheshimiwa Rais, niishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutupatia tani 30 za mahindi Wilaya ya Meatu kwa ajili ya kukabiliiana na uhaba wa chakula. Wilaya ya Meatu tuna upungufu wa tani 19,000 hii

10 NOVEMBA, 2022

imesababishwa na ukame uliokuwepo wananchi hawakuweza kulima kwa kiasi kikubwa na waliolima mazao hayakuweza kuota na yaliyoota wengine hawakuweza hata kupalilia. Hivyo tuna upungufu mkubwa wa chakula na tunaomba Serikali iendelee kusaidia Wilaya ya Meatu pamoja na jirani zetu Mkoa wa Singida ambao wanatusaidia mahindi kwa kuleta mahindi yale yamekwisha katika Mkoa wao, Serikali iongeze speed ya kusaidia Wilaya ya Meatu. *(Makofi)*

Mhshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu kwa mipango yake mizuri na kwa kazi yake nzuri hasa katika matumizi ya zile Trilioni 1.3. kazi kubwa imefanyika. Pamoja na kazi kubwa iliyofanywa ya ujenzi wa miundombinu ya madarasa pia kazi kubwa imefanywa katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Miundombinu ya barabara imetengenezwa vizuri kwa ajili ya kuwawezesha watalii wetu ili *ku-facilitate* kazi za utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa, uwekezaji mkubwa umefanywa katika ununuzi wa mitambo ya kutengenezea barabara pamoja na ununuzi wa magari makubwa katika Wizara ya Maliasili Idara ya TANAPA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu na ushauri wangu, Wizara hii sitegemei uendeshaji wa mitambo hii utegemee asilimia 100 kutoka ruzuku ya Serikali. Mitambo hii iliyopelekwa ni mipya kwa sasa ina sifuri katika suala zima la uchakavu, niliomba mitambo hii ijiendeshe yenyewe kwa kufanya miradi mbalimbali si ya TANAPA peke yake lakini hata taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili ikiwemo TAWA. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu nilitaka sasa kuwena mpango Pamoja na mpiango mingine ya TANAPA na Maliasili kuwe na mitambo ya kuchimba malambo katika hifadhi zetu katika mapori ya akiba ili kuodoa suala la binadamu na wanyamapori kuchangia miundombinu iliyotengenezwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani katika Wilaya ya Meatu bwawa letu la Meatu tembo wapatao 15 zaidi ya mwezi mmoja waliweka kambi katika bwawa letu ambalo ni kilomita tatu kuja Mjini Mwanuhuzi. Kwa hiyo, kuwapunguzia wananchi huduma kulikuwa kuna uhaba mkubwa wa maji katika Mji wa Mwanuhuzi kutokana na tembo hao ambao 15 waliweka kambi lakini zaidi ya 15 walikuwa wanakuja na kuondoka. Kwa hiyo Serikali ijikite kuchimba malambo katika hifadhi ili wale Wanyama waendeleo kubakia kule kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wizara hiyo kupewa fedha ya uwekezaji huo nilitaka sasa fedha zile zitakazopangwa ziwekwe katika kuwekeza miradi mingine, katika Maliasili na Utalii kufikiria kuanzisha miradi itakayo ingiza mapato ujenzi wa mahoteli, tuna upungufu wa hoteli katika Mbuga zetu kutokana na uwingi wa watalii wanaokuja kutokana na Mama yetu kuutangaza utalii wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Halamga ya kufungua malango. Tuombe katika Wilaya ya Meatu tufunguliwe lango la kuingia katika Hifadhi ya Serengeti kwa sababu Wilaya ya Meatu Serengeti imo kwa kiasi kikubwa.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, niunge mkono maoni ya Kamati katika kipengele cha kilimo cha umwagiliaji na ujenzi wa mabwawa. Wizara ya Kilimo ina hekta Milioni 29 ambayo inaweza ikafanywa umwagiliaji lakini ni asilimia Mbili tu ambayo iko chini ya umwagiliaji ambayo ni hekta Laki Nane. Tukiangalia katika hekta Laki Nane hizo naamini kabisa kuna miundombinu ambayo ilishakufa kuna miradi ambayo ilitekelezwa lakini haijakamilika. Kwa Mfano miradi iliyotekelezwa na *DASP* katika miaka ya 2014 miradi ile haikukamilika lakini ilitumia Mabilioni ya Shilingi kwa mfano kutokana na fedha za Benki ya Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe miradi hiyo ya *DASP* iliyoanzishwa ya umwagiliaji ili iweze kukamilishwa iingizwe katika ile idadi kukabiliana na uhaba wa maji katika nchi yetu. Mfano Wilaya ya Meatu mradi ulitekelezwa kiasi kwa Bilioni 1.2 ambo ungeweza kuhudumia hekta 150 sawa na kaya 129 ambapo tungepunguza kabisa uhaba wa chakula, kwa sababu tulitegemea kulimwa mazao ya bustani, mahindi, mpunga na mambo mengine lakini pia wananchi wangeweza kujipatia kipato kwa kuuza ziada. Kwa hiyo, niombe miradi ya *DASP* ikamilishwe ambayo haijakamilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, pamoja na hayo nilitaka kuomba Wizara ya Maji na Wizara ya Kilimo ziweze kushirikiana kwa sababu kitengo cha umwagiliaji kiko katika Wizara ya Kilimo. Wizara ya kilimo haiwezi kufanya peke yake ikaweza kutekeleza miradi ya umwagiliaji. Kwa mfano, Wizara ya Kilimo inaweza ikachangia fedha zake katika miradi ya kutoa maji katika maziwa makuu kwa mfano ule mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya athari ya Tabianchi unaotekelezwa katika Mkoa wa Simiyu kuna *component* ya umwagiliaji, katika fedha za ufadhili

10 NOVEMBA, 2022

zinahitaji pia nchi yetu ichangie, basi zile fedha ambazo ziko katika Wizara ya Kilimo ziletwe katika mradi huo ili tuweze kutekeleza ule mradi mkubwa wa kukabiliana na athari ya mabadiliko ya Tabianchi hii katika Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuisaidie Meatu, Meatu ina uhaba mkubwa sana wa mvua kwa ajili ya binadamu na hata kilimo. Mimi ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, atafutatiwa na Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi ajiandae.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kuhusu mchango huu ambao ni maoni ya Mpango wa Bajeti ya Serikali. Kwanza niseme jambo mmoja, tangu juzi Wabunge wamejadili humu ndani mambo mbali mbali lakini mmoja kubwa ambalo Wabunge wengi tumejiuliza ndani ya Bunge lako Tukufu ni kwamba tunayo maji ya kutosha, tunayo ardhi ya kutosha, tunao watu, Wabunge wanasema, kwanini mambo hayaendi mbele? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, aliwahi kusema wakati fulani, na pengine hilo huwenda likawa ndilo jibu. Alisema kuna msemu Wakwere wanasema '*zilongwa mbali zitendwa mbali*'; yaani yanayosemwa na yanayokwenda kutekelezwa ni tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha ukusoma ni mpango mzuri

10 NOVEMBA, 2022

sana, na hata ukisoma takwimu ni takwimu nzuri sana; lakini utajiuliza ni kwa nini kila mwaka tukija hapa ndani tunarudia mambo yale yale ndiyo maana jibu lake likawa zilongwa mbali zitendwa mbali. Ukitazama michango ya Wabunge, wamechangia maeneo mazuri sana kwenye kuboresha mpango huu. Wametoa maoni mengi sana kwenye Bunge lako Tukufu, lakini unaweza kuja kushangaa tukija mwakani hapa, kwenye mpango wenyewe ukaona hakuna hata moja ambalo wenzetu wa Wizara wameyaweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe wenzangu Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Spika utuongoze Bunge lako, tulioyasema humu ndani ya Bunge, tunatamani kuyaona kwenye mpango wenyewe. Tunaolala na wagonjwa ni sisi, ndio tunaojua wanapoumwa. Sisi ni Wabunge tunajua shida za wananchi wetu, tuwaombe sana wataalam watusikilize, watusikilize na waamini kwamba tunayoyasema ndiyo matatizo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasa nianze kwenye kilimo, jambo la kilimo tangu wakati wa Mwalimu Nyerere, tumesema kilimo ni siasa, kilimo cha kufa na kupona na kadhalika, lakini miaka yote hii kilimo kimekuwa kinasuasua. Nitumie nafasi hii kwa mara ya kwanza kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ambaye yeye ameamua kuondoka kwenye kauli ya zilongwa mbali zitendwa mbali ameamua kufanya kwa vitendo kwa kuongeza bajeti ya kilimo kuanzia bilioni 294 hadi bilioni 959, zaidi ya zaidi ya mara tatu. Rais ana dhamira njema ameamua kufanya kwa vitendo, lakini nimwombe sana Waziri wa Kilimo na hili nasema na Bunge liweke Kumbukumbu. Tumemuongezea Waziri wa

10 NOVEMBA, 2022

Kilimo fedha kwa ajili ya mbolea, mbegu, ujuzi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nataka kuamini tutakuja mwakani hapa, tutakuwa na wakulima wengi ambao wamelima mazao yao lakini hakuna soko. Mwaka jana kabla ya kuongeza bajeti tulikuja hapa, tukaiomba Serikali itafute fedha za dharura kwenda kununua mahindi kwa wakulima. Namuomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, wameshauri Waheshimiwa Wabunge humu ndani, mpango mzuri unaokwenda nao, tusaidie kuweka mkakati wa kutafuta masoko kwa ajili ya mazao haya ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kule Lupembe wananchi wangu wamehamishwa sana kulima parachichi, tunavyozungumza wamelima parachichi wameuza zaidi ya miezi sita hawalipwi kwenye mazao yao, soko hakuna. Kwa hiyo naomba kabla hatujatengeneza *crisis* ya soko tujipange mapema, tuandae soko, wananchi wakulima mahindi au mazao watakwenda kuuza wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Tusaidie kutuondolea watu wababishaji na wafanyabiashara uchwara kwenye kilimo. Sisi Lupembe kwa mfano tunalo zao la chai, zao ambalo ni kubwa sana kwenye nchi hii. Linaingiza fedha za kigeni na lina uwezo wa kutoa ajira nyingi sana kwa wananchi wetu. Linaweza kutoa ajira kwa mkulima mwenyewe kwa mzalishaji, watu wenye magari, wasafirishaji na kadhalika. Lakini zaidi ya miaka 20 wananchi wa zao la chai Lupembe wamezidi kuwa

10 NOVEMBA, 2022

maskini, wanalia na Serikali kila siku wanaomba kiwanda chao kirudi kifanye kazi sababu hakifanyi kazi. Tunaongea habari ya ajira hapa, mtapataje ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, wananchi wa Lupembe wamelia kilio kama mamba majini machozi yao yanakwenda na maji. Naomba wapatie matumaini wananchi wangu wa Lupembe, kile kiwanda cha Lupembe *Tea factory* Kirudishwe kifanye kazi na mwekezaji aliopo pale tuondolee kama ni mzigo, atoke pale, wananchi wangu wapate ajira na Serikali ipate fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni kuhusu...

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Edwin Ennoy Swalle kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

T A A R I F A

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa tu taarifa Mheshimiwa Mbunge wa Lupembe na wananchi wake, kwamba Serikali imeshachukua hatua dhidi ya muwekezaji wa kiwanda cha *Lupembe Tea Company Dhow Merchantile*, na sasa Bodi ya Chai imeshamuandikia *notice* ya kumfutia leseni kwa sababu makubaliano yote aliyoingia na Serikali ameamua kutokuyafuata. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Swalle, unaipokea taarifa hiyo.

10 NOVEMBA, 2022

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili kwa niaba ya Wananchi wa Lupembe. Ninachoomba kauli hii ya Mheshimiwa Waziri isiwe zilongwa mbali zitendwa mbali. Nakushukuru sana Mheshimiwa Bashe kwa jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni kuhusu jambo la mazingira. Nimesoma kwenye mpango wa Serikali, jambo la mazingira limesemwa kama jambo la mzaha hivi. Jambo la mazingira; naishauri Serikali tusitegemee fedha za wahisani tu, tuanzishe mpango maalum angalau kwenye halmashauri zetu waanze kutenga fedha kwa ajili ya kutunza vyanzo vya maji. Hata hapa Dodoma hali ya hewa imekuwa ikibadilika siku hadi siku, na wananchi yetu wanaendelea kuongezeka, tusipoweka mkakati wa muda mrefu wa kutunza mazingira, wakutunza maji, suluhu ya muda mfupi ya kuhamisha wananchi kwenye mabonde haiwezi kusaidia. Suluhu ya kudumu ni kutunza mazingira, tuwashirikishe wananchi wapande miti, watunze vyanzo vya maji wawe sehemu ya kuhifadhi mazingira yetu. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumesaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajenga Bwawa la Mwalimu Nyerere pale leo, linategemea maji, Mikoa ya Kusini ndio mwanzo wa maji haya. Tumeingiza trilioni sita pale lakini mpango wa Serikali wa kuhifadhi vyanzo vya maji kwa kutumia fedha za ndani kwenye halmashauri upo wapi? Juzi pale kwangu Mtwango wananchi wangu wamelima kwenye maeneo ya mabonde, wamefyekewa mazao yote pale, lakini kufyeka mazao haiwezi kuwa suluhu ya kuhifadhi maji.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuwa na mpango wa Serikali wa kukwamua utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji. Napendekeza kama itakuwa jambo jema, Serikali ikiona inafaa, waziagize halmashauri, kwa kuwa mmeagiza kutoa asilimia kumi kwa ajili ya wanawake, vijana na wenye ulemavu, agizeni halmashauri watenge hata asilimia mbili kwa ajili ya fedha za kuhifadhi mazingira na kutunza vyanzo vya maji.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar atafuatiwa na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, naona muda wetu utakuwa umeishia kwa huyo. Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar.

MHE. BAKAR HAMAD BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, kwa zawadi ya uhai na uzima na kuweza kuniwezesha kusimama katika Bunge lako tukufu asubuhi hii. Pia, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, lakini pia nikupongeze kwa namna ambavyo unaendelea kuliheshimisha Bunge letu ndani na nje ya nchi yetu.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anaendelea kupambana na kutatua changamoto za Watanzania.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najjuliza hivi hali ingekuwaje kama Mama Samia asingekubali kuweka na kutoa zile

10 NOVEMBA, 2022

bilioni 100 kila mwezi ambazo zinaenda kutatua na kupunguza changamoto ya mafuta. Najjuliza ingekuwaje kwa wakulima wetu kama Mama Samia asingekubali kuzitoa zile bilioni 150 kwa ajili ya kupunguza changamoto ya bei ya mbolea na bei ya mbegu bora. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia huwa najjuliza, hivi bei ya unga na mafuta ya kula ingekuwaje kama kodi za bidhaa hizi pamoja na tozo zisingeweza kuondolewa na kuweza kuwawezesha wananchi kuweza kupata bei nafuu angalau kutokana na uchumi ambao kwa sasa hivi unaendelea duniani. Baada ya kujuliza haya yote, niwaombe sana Watanzania tuendeleo kumuunga Mama Samia mkono, tuendeleo kumuomba dua ili aweze kuyatekeleza haya ambayo yanapangwa kwa umakini zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango huu ambao tunaenda kuujadili pamoja na bajeti ya mwaka 2023/2024, mimi nitatoa mapendekezo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezwa kwamba kuna mwenendo wa sekta za kibenki, kwamba benki sasa hivi zimeanza kupata faida kubwa kupitia *return on equity* pamoja na *return on asset*. Hatuwezi kujisifia kwa kuwapa benki hizi kupata faida pekee yao. Kwa sababu ndani ya benki hizi zisingekuwepo kama si wawekezaji. Bado *interval* na *difference* kubwa ipo kwenye wawekezaji pamoja na benki hizi. Watu ambao wanawekeza fedha zao, fedha wanayoipata kama faida ni ndogo kulinganisha na pesa wanayoipata benki kama faida. Bado *interest cost* ambayo waomba mikopo wanaichukua, wanaomba na kupewa ni *interest* kubwa

10 NOVEMBA, 2022

sana hadi sasa hivi, lakini ukiangalia wale wanaowekeza fedha zao ile *interest income* wanayoipata ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa hali hii utakuta kwamba benki zinatengeneza faida kubwa lakini wale wanaowekeza bado pesa wanazozipata na *income* wanayoipata ni ndogo sana. Kwa hiyo, hatuwezi kujisifia kwa jambo hili. Mimi niombe muongozo wa mpango na tutakapokwenda kutengeneza mpango basi angalau sasa tushushe riba ya mikopo lakini pia tuongeze ile *interest income* ambayo inapatikana kwa wawekezaji wanaowekeza kwenye benki zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge la Bajeti nilichangia kuhusiana na kuwepo kwa *Islamic banking* bado naendelea. Kwenye muongozo huu wa mpango ambao tunaenda kuuandaa pamoja na bajeti inayokuja naendelea kulisisitiza jambo hili. Kwa sababu kipindi kile cha bajeti halikuweza kutekelezeka lakini naamini kwa sababu tunaenda kutengeneza mwongozo, tunaenda kutengeneza mpango wa bajeti lakini pia tunaenda kutayarisha bajeti ijayo, naamini jambo hili Mheshimiwa Waziri kutokana na umuhimu wake unaweza kulichukua na kuweza kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametuambia hapa kwamba mikopo chechefu imetoka kuanzia asilimia 9.3 mpaka sasa hivi ni asilimia 7.8. Mimi nipongeze kwamba inapungua lakini bado hiki kiwango ni kikubwa na ni kikubwa kwa sababu ile ambayo mwanzo niliizungumza, kwamba riba ya mikopo ni kubwa sana, lakini *Islamic banking* ndiyo ambayo inaenda kutatua changamoto hizi. Mifumo hii ya *Islamic banking* ipo hapa nchini tangia

10 NOVEMBA, 2022

2008 lakini tangu kipindi chote hicho inatumika kienyeji. Bado hakuna sheria, bado hakuna miongozo, bado hakuna kanuni ambazo zinaiongoza na kuisimamia *Islamic banking* ndani ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana Serikali, ilichukue jambo hili, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuweka kile kipengele kwenye ile *financing act* ya kuondoa VAT kwenye mikopo ya mrabaha ambayo ni *Islamic product*. Kuondoa kipengele kile kuanzia mwaka huu 2022 lakini bado tunatakiwa tuwe na sheria ambayo inaongoza namna bora ya kuendesha hizi huduma za mikopo ya kiislamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichangie jambo moja, nakuomba...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. BAKAR HAMAD BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nikachangia Mapendekezo ya Mpango huu wa Taifa wa Mwaka 2023/2024. Mpango huu ni wa tatu katika mpango wa miaka mitano wa 2022 mpaka 2025/2026 na mpango

10 NOVEMBA, 2022

wetu huu unadhima ya kukuza uchumi shirikishi na uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunalenga kukuza uchumi wa viwanda na uchumi shirikishi tunategemea mpango wetu huu ungeangalia zaidi *catalyst* (vichachua uchumi). Vichachua uchumi vyetu hivi ni viwanda ni nishati ni usafiri na usafirishaji ni muhimu sana. Toka tumesema Tanzania ya viwanda bado hatujafanya vizuri kwa viwanda. Viwanda ni kichachua uchumi kwa wazalishaji wote; kwa wakulima kwa wafugaji na hata kwa wachimba madini. Wakiwa na uhakika kwamba viwanda vipo pale kwa ajili ya kusindika, uzalishaji utaongezeka kwa sababu ya uhakika wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini viwanda ndivyo vingenda ku-solve changamoto ya aijira ya vijana tunayoisema kila siku. Vile vile, viwanda hivi ndio vingesaidia kuongeza kipato kwa mkulima kwa kuongeza mnyororo wa thamani. Wenzangu wamesema, tunazalisha na tunauza malighafi kwa wenzetu. Tunazalisha korosho, pamba, mahindi vinaenda kama malighafi, tunaenda kujenga viwanda vya wenzetu wanasindika na sisi ndio walaji wanaturudishia. Sasa tubadilike na sisi tukatafute masoko ya vitu ambavyo tayari tumeshavi-process kwenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishati ya umeme ni muhimu sana kama kichochezi cha uchumi katika Taifa letu. Niwapongeze tu Wizara tu kwamba wameweza kufikia vijiji 9,160 kati ya vijiji 12,400 na kitu. Umeme ni kichochea uchumi muhimu sana, ni haki ya kila Mtanzania kupata nishati ya umeme. Umeme ambao tayari umekwisha kupelekwa unaishia katika *center* za vijiji

10 NOVEMBA, 2022

ambapo unapaswa umeme kufika kwenye vitongoji kama ilivyo dhima yetu ili kila mtu a-enjoy kuwa na umeme katika eneo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme unatoa ajira kwa vijana walioko vijijini watatengeneza visaluni vyao watukuwa na viwanda vidogo vidogo vya *welding* wengine watamwagilia kwa kutumia *pump*. Vile vile ungepunguza hii *rural-urban migration*, kwa sababu vijana wanaomaliza chuo kikuu ukawapeleka kwenye vijiji ambavyo havina umeme wasingeweza kukaa huko. Umeme tunahitaji wa kuaminika, unajenga fursa ya wawekezaji nikivutio kwa wawekezaji kuja kama kuna umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani mpango huu sasa utuambie, pengine uhakika wa umeme, tungeweza kuupata baada ya kukamilisha mradi mkubwa huu wa Julius Nyerere ambao tulitarijia kupata *mega watts* 2,115. Mradi huu umeanza tangu Disemba 2018 nawapongeza kwamba tumefikia sehemu nzuri asilimia 77 lakini tumekwisha kuwekeza 1.2 trilioni. Sasa ili weze kutoa *output* tunakila budi kuona kwamba mpango ukoje na mpango kazi ukoje, kwamba katika mpango unaokuja, tukamilishe ili tuweze kupata umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafirishaji ni changamoto kubwa sana. Usafirishaji huu ndiyo sababu kina mama zangu kule wanalalamika bei kubwa ya vifaa wanavyovitumia, bei kubwa ya pembejeo, kwa sababu barabara na vivuko ni ngumu. Nategemea mpango huu uwekeze vya kutosha kwa *TARURA* na *TANROAD* ili barabara zetu na vivuko vipitike mwaka mzima.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni shida sana, wakulima wamezalisha kule, kuja kuleta mazao yao mjini ni kazi kubwa na yanaharibika mwengine ni *perishable foods*, zinakaa pengine kwenye usafirishaji siku nzima au siku ngapi baada ya magari kukwama, unakuta kwamba uharibifu wa mazao ni mkubwa sana. Kwa hiyo, tuangalie hizi *pillars* katika mpango wetu huu. Kwamba lazima tuboreshe hizi viashiria ili kwamba tuweze kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpango huu nategemea pia utaendelea kuwekeza katika sekta za kiuchumi ambayo ni kilimo, mifugo, maliasili pamoja na madini. Mimi nawapongeza sana kwamba tumeshafanya vizuri kwa kuongeza bajeti iliyopita, tumeongeza bajeti zaidi ya mara tatu na tumeanza kuona matokeo makubwa. Sasa ninafikiri uwekezaji huu lazima tuone ni maeneo gani hasa tutawekeza kwenye kilimo. Sehemu ambayo ina - *risk* kidogo na sehemu ambayo tukiwekeza miradi mikubwa, tukawekeza fedha nyingi itaweza kurudisha kwa mapema, yaani *pay back period* iwe ndogo. Kwa mfano, naipongeza Wizara kwa mpango wake, sasa hivi tunatakiwa tuhamie kwenye uwekezaji wa mashamba makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Wizara imekwisha kupata ekari 183,000 hapa Chamwino. Mimi nawapongeza kwa sababu kuwekeza katika mashamba makubwa ya pamoja (*block farming*) ina faida kubwa kwa sababu ni mashamba yapo pamoja uzalishaji utafanyika kwa gharama ndogo, itakuwa *economical of scale* lakini rahisi kusambaza teknolojia. Vile vile sasa kuweza kupata soko, mazao yanayotakiwa kwa ile *quality*. Kwa mfano shamba lilipo hapa kama

10 NOVEMBA, 2022

tunawapata *assignments* watazalisha soya itaenda kuzalisha ile soya ambayo tayari tuna soko lake nje. Basi jitihada hizi zifanyike kwa zone. Kila zone agro-zone, kwa mfano hata Manyara tungeweza kupata mashamba Kiteto, basi yapatikane mashamba yaangaliwe hali ya udongo hata tuka - *assign* pengine ikazalisha hata mahindi ya njano ambayo tayari tunasoko Misri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mpango huu ni mzuri nawapongeza. Kwamba hatuna *risks* zozote za kuwekeza katika kilimo kama hicho, na kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji ambacho *risks* zake ni ndogo. Fursa ni nyingi kwenye kilimo, tumeona kwamba maeneo yanoyofaa kwa kilimo ni zaidi ya hekta milioni 44 na ambazo tumeweza kulima asilimia 38 mpaka 40. Kwa hiyo zaidi ya asilimia 60 ya eneo linalofaa kwa kilimo bado halijatumika. Kwa hiyo, bado tunaweza kuweka wawekezaji ambao unalima na ambao hauna *risks* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikifikiria kwamba tungeweza kuwekeza pia kwenye mifugo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia ahsante sana. Tungeweza kuweka kwenye *ranch* zetu kule tukanenepesha mifugo au tukazalisha malisho ya mifugo kwa matumizi ya ndani na nje tungeweza pia kufanya vizuri. Nakushuru sana, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mchana nitawataja baadhi ya wachangiaji ambao

10 NOVEMBA, 2022

tutaanza nao; Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hassunga, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga na Mheshimiwa Nagenjwa Livingstone Kaboyoka. Wengine tutaendelea kuwataja kadri muda utakavyokwenda.

Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:
Bunge linarudia.

(Bunge Lilirejea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nadhani mmeshamuona hapo Kaimu Mkuu wa shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo kwa hivyo, Mheshimiwa Mkuchika anashika nafasi hiyo.

Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11 kamili, jioni leo.

(Saa 7.30 Mchana Bunge Lilisitishwa Hadi Saa 11:00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

SPIKA: Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

10 NOVEMBA, 2022

pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate atafuatia, na Mheshimiwa Saashishi Elinikyo Mafuwe ajiandae.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu katika mwelekeo wa mpango wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Pia naipongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuja na mwongozo huu wa Mpango na Bajeti ambao wameileta mbele yetu. Tatu, naipongeza Kamati ya Bajeti kwa namna walivyoichambua na kuleta maoni yao hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wetu lazima ujielekeze katika kujibu mambo ya msingi yanayotuhusu. Ninafurahi kuona kwamba mpango huu umeandaliwa vizuri. Mwelekeo wa mpango huu ni mzuri na unatupeleka kule tunakotaka. Yapo matatizo ya msingi ambayo sisi sote tunahusika na lazima tutafute mwelekeo wa namna ya kuyatatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni umasikini mkubwa wa wananchi katika utajiri ulio mwingi

10 NOVEMBA, 2022

katika nchi yetu. Nchi yetu ni moja ya nchi tajiri sana, lakini watu wake ni masikini. Kwa hiyo, hili ni lazima mwelekeo wa mpango ukajibu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni ukosefu na upungufu wa ajira kwa vijana wetu; na la tatu, ni mchango mdogo wa sekta za uzalishaji kwenye pato la Taifa. Jambo la nne, ni tija ndogo katika maeneo mbalimbali; na la tano ni ukuaji mdogo wa sekta ya viwanda na mambo mengine yote. Haya mambo matano ni msingi mkubwa wa utayarishaji wa mpango. Nami naamini kwamba mpango huu unatupeleka katika kujibu na kutafuta ufumbuzi wa haya ambayo yanaikabili nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2000-2025, ina vipaumbele vitano. Moja ya kipaumbele ni kwamba tunataka kuboresha hali ya maisha ya Watanzania. Sasa hivi maisha ya Watanzania katika uhalisia, hali ni mbaya. Tunataka kuwepo kwa mazingira ya amani, usalama na umoja, na hili tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa; tunataka kujenga utawala bora; tunataka kuwepo kwa jamii iliyoelimika na inayofundishika; na tunataka kujenga uchumi imara unaoweza kukabiliana na ushindani wa nchi jirani na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia dira yetu inavyosema, mipango yetu, vipaumbele vyetu, Sera na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, vyote vinashabihiana. Vinatulazimisha tukae chini tuweze kutatua haya matatizo ya wananchi. Sasa hali ilivyo sasa hivi, tunazo takwimu nyingi; tunayo nchi yetu ambayo imebarikiwa kuwa na rasilimali za kila namna, lakini tunazunguka

10 NOVEMBA, 2022

katika mzunguko wa umasikini (*poverty cycle*), tunazunguka mle. Sasa hapa lazima tujikite kuona tunatokaje katika huu mzunguko ili twende kwenye eneo lingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mipango yetu na mambo yote ambayo tumekuwa tukiyafanya, bado tunazunguka. Sasa hivi kuna mjadala mkubwa kwamba nchi yetu ilikuwa imefika kipato cha kati, sasa tumerudi kipato cha chini, lakini sisi kazi yetu ni kuhakikisha kwamba tunatoka hapo tunaenda mpaka kwenye kipato cha juu. Sasa yapo mambo ambayo mimi ningependekeza kwamba tuyaangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumependekeza kwa muda mrefu na bado halijafanyiwa kazi. Kwanza, ni uwepo wa Tume ya Mipango pamoja na Baraza la Tija.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hasunga, Mheshimiwa Waziri amesimama. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongezae Mheshimiwa Mbunge kwa mchango mzuri. Nimeona ame-refer hili jambo lililosemwa juzi kwamba Tanzania tumeshuka kwenda kwenye kipato cha chini, pamoja na kwamba nimejiandaa kuja kulijibu, lakini niliona ili kumsaidia atiririke vizuri, ni kwamba Tanzania haijashuka kwenda kwenye kipato cha chini na taarifa zilizotolewa na mchangiaji, Mbunge wa Musoma Vijijini siyo sahihi, na nukuu aliyonukuu na yenyewe haikuwa sahihi. Nadhani nitatolea zaidi ufafanuzi nitakapokuwa na-*wind-up*.

10 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hasunga, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea, kwa sababu sina tatizo kabisa katika huo mjadala unaoendelea. Naipokea kabisa kwa sababu tunatakiwa tuwe na takwimu sahihi, na ndiyo msingi wa kupendekeza kwamba tuwe na Tume ya Mipango itakayokuwa na uwezo wa kuchambua hali ya maisha, uchumi wa nchi yetu na kutupa takwimu sahihi. Ie Tume ya Mipango itapanua wigo, itafanya watu wote waweze kushirikishwa wataalam mbalimbali, waweze pia kujadili watupe takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Waziri hii itatusaidia sana kuwepo kwa Tume ya Mipango lakini pia na Baraza la Tija ambalo litasimamia kupanua tija katika uzalishaji, tija katika viwanda vyetu na tija katika maeneo mbalimbali. Hili ni suala ambalo nafikiri ni la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tumeona nchi yetu iko *strategically located*, na ndiyo maana sasa hivi tunazo bandari ambayo tunafikiri zinaweza kuhudumia nchi jirani. Sasa hivi kuna mjadala unaoendelea, watu wengine wanasema tujenge Bandari ya Bagamoyo na wengine wanakataa. Mimi nafikiri Bandari ya Bagamoyo ni *inevitable*, lazima tujenge, na Bandari ya Dar es Salaam iendelee, ya Mtwara iendelee na bandari nyingine zitakazowezezana zijengwe. Kwa sababu lengo la hizi bandari ni kuhudumia, na tunataka zile nchi ambazo hazina uwezo wa ku-access ziweze kuhudumiwa. (Makofi)

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye hili lazima tuweke nguvu. Kwa hiyo, nategemea mpango huu utakapokuja, utakuja na namna ya kuijenga hii Bandari ya Bagamoyo, lakini tusingahau na pale Bandari Kavu Mpemba, Tunduma kwa sababu pale ndiyo lango la SADC. Pale ndiyo nchi za Zambia, Malawi na nchi zote zitakuja kuchukulia mizigo pale. Kwa hiyo, tukijenga Bandari ya Bagamoyo, tunajenga Bandari Kavu pale Tunduma-Mpemba, tutakuwa tayari tumeitendea haki nchi hii. Tutaenda kujibu matatizo haya ya msingi ambayo nimesema yapo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo napenda kupendekeza, ni katika upande wa *allocation* ya *resources*. Mheshimiwa Waziri atakapokuja na bajeti, nimeona mwongozo, nimeusoma, lakini nadhani, ili tuondoke katika mzunguko wa umasikini ili tutoke pale, uwekezaji tuje na *formula* ya namna ya kuwekeza zile rasilimali zetu. *Allocation* ya *resources* zile za maendeleo, tuje na *formula*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza napendekeza, zaidi ya asilimia 30 au 40 ielekezwe kwenye sekta za uzalishaji. Kwa sababu tukielekeza kwenye uzalishaji, huko ndiyo wananchi wengi wapo; tutatatua tatizo la ajira, umasikini na tutahakikisha uzalishaji malighafi zinapatikana na ndiyo viwanda sasa vitaweza kujengwa, tutapata malighafi. Huwezi kufanya hivyo kama hilo halitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 30 iende kwenye huduma za jamii na asilimia 30 nyingine iende kwenye huduma za biashara na miundombinu. Hiyo *formula* inaweza ikatusaidia kutoka. Tukiwekeza kwenye huduma za jamii bila kuwekeza kwenye uzalishaji, tutakuwa

10 NOVEMBA, 2022

tunazunguka kwenye *poverty line*, hatutatoka kule kwenye yale maeneo ambayo mimi ningependekeza tutoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, kujenga viwanda na kuanzisha mfuko wa kuchochea viwanda. Hatuwezi kujenga viwanda kwa kupiga kelele. Hatuwezi kujenga viwanda kwa kusema tunahamasisha viwanda, lazima tutenge fedha, tujenge viwanda, halafu tutafute waendeshaji wa hivyo viwanda. Yale mazingira yawe yameshatengenezwa, tutakuwa tayari tumeteteleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mengi, lakini mengine tutayachangia, nashukuru sana kwa kupata hii nafasi na ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, ajiandae.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii, kuchangia Mpango wa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutengeneza mpango ambao unaendana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025. Pamoja na kufuata ilani, lakini kwa mpango wetu huu nimenifurahishwa mno kitendo cha kuwepo miradi ya Liganga na Mchuchuma pamoja na reli ya Mtwara, Mbamba Bay.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza suala la Bandari ya Mtwara, tumefanya uwekezaji mzuri, lakini bado hatuna mipango, namna ya kuitumia Bandari ya Mtwara. Njia pekee ya kuitumia hii ni kutekeleza miradi miwili ya Liganga na Mchuchuma sambamba na reli ya kutoka Mbamba Bay kwenda Mtwara pamoja na njiapanda zake za Mchuchuma na Liganga. Tukitekeleza miradi hii, Bandari ya Mtwara itatumika ipasavyo na itaweza kuleta uchumi na kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutekeleza miradi hii, kwa sasa hivi kule Ngaka kuna makaa ya mawe ambayo yanaenda Mtwara karibu kila siku zaidi ya magari 300 mpaka 400 na mengine yanapita hapa hapa Dodoma kwenda Nairobi, Burundi na Arusha. Ni kwa sababu y barabara ile imekuwa nzuri, na ni ya lami. Kama tungeweza kujenga Reli ya Mtwara -Mbamba Bay - Liganga na Mchuchuma nadhani ingekuwa rahisi zaidi na mzigo mwingi ungeweza kutumia Bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wizara watakapokuja na mpango kazi huu ambao wameuzungumza, isiwe wimbo wa kila siku kwamba kila mwaka tunasema tutajenga, tutatekeleza Mradi wa Liganga na Mchuchuma, tutatekeleza kwa PPP, suala la ujenzi wa reli ya Kusini, hili jambo litakuwa halina maana. Hili jambo huwezi kulitenganisha; utatekeleza Mradi wa Liganga na Mchuchuma, hakuna namna ya kusafirisha chuma. Njia sahihi na rahisi ni ya kutumia reli peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa tutaanza mapema, tunatakiwa lazima tujenge barabara inayounganisha Mkiu kwenda Madaba ambayo magari yataenda moja kwa moja mpaka kufika Mtwara. Njia hizi bila kufanya,

10 NOVEMBA, 2022

kwa kweli hali ya miradi hii, hata wawekezaji wanapokuja, moja ya changamoto ya Liganga na Mchuchuma kwa wawekezaji wa ndani ni hali ya mahali ilipo na usafiri wa kwenda mahali pale. Shahidi atakuwa ni Mbunge wa Ludewa; barabara yao, sisi tumefika pale, siyo nzuri na siyo rafiki kwa kuweza kuendesha ule mradi. Nadhani wakati umefika, pamoja na kutekeleza huu mradi, basi tutengeneze huu mradi pacha ambao ni wa kutengeneza reli ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, nitazungumzia mpango na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 ambayo ilieleza kwamba, tutatengeneza barabara kwa kiwango cha lami kutoka Mtwaro - Pachani Nalasi kwenda Tunduru Mjini. Eneo hili kwa kweli lina vijiji 77. Vijiji 30 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, vijiji 47 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo. Ni maeneo ambayo ni mazuri, yana uchumi mkubwa wa korosho, ufuta, mbaazi pamoja na mahindi. Kwa hiyo tunaomba kwenye mpango ujao, na sasa hivi ni mwaka wa tatu huu, hakuna dalili yoyote ya kuonesha sehemu hii itatengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwamba kila mwaka inatoa siyo chini ya Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kutengeneza barabara ile kwa kiwango cha changarawe, lakini kwa sababu ya mvua nyingi zinazonyesha katika maeneo yale, kila mwaka barabara ile inakuwa inatengenezwa na haina mafanikio kwa sababu ya hali ya milima na maeneo korofi yanasababisha wananchi kuweza kushindwa kupeleka mazao yao sokoni ili waweze kupata tija.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali kwenye mpango ujao waone namna angalau katika kilometa zile 300 waanze kupunguza maeneo yale korofi, kuyatengea bajeti ili barabara ile iweze kutekelezeka na watu waweze kupunguza kero za usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, suala la barabara kutoka Songea - Njombe mpaka Makambako, hili jambo ni la muda mrefu, barabara imechoka. Kama nilivyozungumza mwanzo, inapitisha malori makubwa ya makaa ya mawe kutoka Ngaka. Ie barabara ina mzigo mkubwa, ni ya muda mrefu, imekamilika mwaka 1984, mpaka leo ile barabara kwa kweli hali ni mbaya. Ina mashimo, ukienda ovyo unaweza ukakuta undingia korongoni kwa sababu ya makorongo ambayo yapo kwenye barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye mpango huu, tunapofikiria kutengeneza Liganga na Mchuchuma, basi barabara hii itengewe fedha ili ijengwe upya, siyo kuweka viraka kama wanavyofanya sasa kwa sababu haina manufaa na inachelewesha mizigo ya watu kufika sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo na Mheshimiwa Jackson Gidion Kiswaga, ajiandae.

10 NOVEMBA, 2022

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Mapendekezo ya Mapendekezo ya Mpango ulioletwa hapa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nami nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa maandalizi mazuri yaliyoanza na uwasilishwaji wake mzuri. Ila naomba nirejee jambo ambalo nimewahi kusema humu ndani. Sioni tuna shida gani ya kukubali kupokea ushauri mpya. Mipango hii tunayoendelea nayo na utaratibu tunaoutumia wa kuandaa kwa kipindi cha miaka mitano, tunaandaa mwaka mmoja mmoja, hatuwezi kufikiria kusogea mbele zaidi? Nilishauri hapa tuwe na mipango ya miaka 50, itakuwa na tija ili vitu vyetu tunavyovipanga, vikamilike kwa ukamilifu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa dhima yetu inayotuongoza inasema, kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya Taifa. Sasa kama tunazungumza viwanda, hii ni *process* ya muda mrefu. Naomba Waziri anapokuja, hizi dhima zilizopita huko nyuma, angalau arejee basi kutupa tathmini, walifikia malengo kwa kiwango gani? Ili michango hii tunayoitoa hapa, iwe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalisema kwa utangulizi tu. Tunapotoa mawazo hapa, wakubali kupokea vitu vipya; na hili litatuondoa kwenye hii hali ya watumishi kufanya kazi kwa mazoea. Wakiambiwa nendeni mkaandae mpango, wanarudi kwenye *laptop* zao, wanabadilisha mwaka na *figure* pale, wanatuletea. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Mheshimiwa Waziri, hebu wakati unapokuja mwaka mwingine, fikirieni namna ya kutuletea mpango wa kutumia watu wetu wenye akili. *Mindset* za watu tuone, wote tuna akili ndiyo, lakini wapo watu wenye uwezo mkubwa kuliko sisi. Hata huko kwenye Wizara zenu mna watu ambao wana uwezo mkubwa lakini bahati mbaya hatuwatumii kwa sababu hatuna mpango wa kuwatumia hawa watu. Sasa shida tuliyokuwa nayo ndiyo hii tunayokutana na watu ambao kazi yao ni kujaza maboma, yaani yuko pale Wizarani, anatuma taarifa ana-*edit*, anatuletea. Tuwape watu uwezo wa kufikiri waje na vitu vipya, kama hivi ambavyo nasema tuwe na mipango ambayo itatekelezwa kwa kipindi cha miaka 50, miaka 100 na kuendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze kwa namna ambavyo kwa kweli Wizara ya Kilimo imepokea mawazo yetu na imeanza kufanya kazi. Nimefurahi kuona kwenye mpango huu tumeanza mashamba maalum kwa ajili ya kulima mbegu zetu, nipongeze sana. Nimpongeze pia Waziri wa Kilimo, kwa kweli kwa hili anatupa heshima sana. Wametenga hekta 853 na mchakato uko kwenye tathmini. Sasa nikawa najiuliza, ina maana tangu tumepata uhuru ndio tunaanza kutengeneza mashamba yetu ya mbegu? Basi kwa kuwa tumeanza, niombe sana Mheshimiwa Waziri kwa kweli aongeze *speed* ili tuwe na mbegu sahihi za kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishauri Bunge lililopita kwamba, hili suala la mbegu lichukuliwe kama suala la kiusalama kwa sababu, bila mbegu sahihi hatuwezi kufanya kilimo kilicho sahihi na bila kilimo hatuwezi

10 NOVEMBA, 2022

kuongeza uchumi wetu, kwa sababu unapoongeza uzalishaji ndio unakuza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho kimenishangaza ni kwamba wameanzisha mashamba hizi *block farming* hapa Dodoma, lakini wameweka changamoto kwamba mashamba yametengwa lakini hakuna maji. Sasa niombe Waziri atakapokuja kuhitimisha atueleze kwamba katika hayo mashamba kuna maji ya uhakika, tuweze kupata kauli yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo pia wamefanya vizuri na ningependa kuchangia. Kwenye umwagiliaji wametenga fedha na kule Hai tunashukuru tumepata miradi mingi ya umwagiliaji. Sasa naendelea kumwomba Mheshimiwa Waziri atazame na pale Metrom tukipata ile tutafanya kazi kubwa sana ya kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni sambamba na masoko, tumeshaanza vizuri sana kuimarisha kilimo na tumewekeza huko. Hali ya masoko ikoje? sisi pale Hai na soko la Kwa Sadala limeshakuwa sasa ni kila siku nazungumza. Soko hili la Kwa sadala jamani sio tu la Hai, hili litahudumia kanda yote ya kaskazini na ni kama soko la kimataifa. Nilisema hapa ramani tuliyotengeneza siyo ya kawaida tumeweka vitu vingi humo ndani, kuna *sorting industry*, humo ndani kuna *grading*, kuna kufungasha. Hebu watutengenezee hela watuletee ili soko lile liweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri uwanja wa ndege ule wameshaukubali uwe wa kimkakati wa kilimo. Wameshatuletea fedha za kujenga *common use facility*

10 NOVEMBA, 2022

pale. Kwa hiyo hili soko likijengwa litatusaidia sana kwenda sambamba na hiki ambacho tunakifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme jambo moja kabla muda haujaisha. Sisi Mlima Kilimanjaro pale ni chanzo cha mapato. Mapato yale yanakusanywa kupitia Serikali Kuu lakini sisi tulioko pale, kama ilivyo maeneo mengine, watu walioko migodini humo wanakusanya *service levy*, lakini sisi pale hatupati. Niombe sana kwenye eneo hili la mipango Waziri atakapokuja hapa atuambie, kama ambavyo maeneo mengine wananufaika na sisi tunataka tupate walau *service levy* kutokana na Mlima Kilimanjaro. Hili naomba sana sana Mheshimiwa Waziri atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo natamani niseme hapa ni kuhusiana na *NIDA*. Kwenye taarifa *NIDA* ili waweze kutoa vitambulisho vya utaiifa kwa wananchi wetu, wanahitaji bilioni 42.5 ambayo haijapelekwa. Sasa hapa tunapanga mipango mingi na tunatoa maelekezo mengi, mpaka tumesema ile asilimia 10 inayoenda kukopwa na vikundi, wale wanaoingia wanatakiwa wawe na *NIDA*. Sasa najiuliza, kama hawa hawana fedha hizi za kuweza kutengeneza vitambulisho, hali itakuwaje kwa wale wanaoenda kukopa? Hiki ni kikwazo. Kwa hiyo niombe sana hizi fedha zitafutwe na *NIDA* wapewe ili Watanzania wote waweze kuwa na vitambulisho vya Utaifa na waweze kupata huduma kama ambavyo tumezungumza hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linafanana na hili ambalo nilikuwa nazungumza hapa, ni la kuanzisha Tume ya Mipango ya Taifa. Tunapozungumza hapa naona Wabunge wengi

10 NOVEMBA, 2022

wamechangia, tuanze taasisi hii lakini kuwe na watu wenye uwezo, hili ni muhimu sana. Tumekuwa na mazoea tunaanzisha taasisi tunapeana, hapa twende na watu wenye uwezo ili watusaidie yaani kwa maana wenye akili sio tu wenye vyeo ndio namaanisha namna hiyo. Kwa sababu wengi kwenye utumishi wamo lakini wenye akili hawapati nafasi. Shida kwenye taasisi hizi mtu mwenye uwezo anafichwa chini chini. Ninyi ni mashahidi angalieni hata kwenye...

MHE. JANEJELLY J. NTANTE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Inatokea wapi? Sawa, Mheshimiwa Janejelly Ntante.

MHE. JANEJELLY J. NTANTE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji kwamba Serikali haiajiri watu wasiyo na akili. Watumishi wote wa Serikali wana akili sawasawa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, unapokea taarifa hiyo?

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa ya mama yangu wala sina tatizo. Ninachokisema mimi, wote tuna akili siyo tu watumishi wa umma hata sisi wote tuna akili ila tupishana uwezo, ndio ninachokisema. Sasa wale wenye uwezo wapewe nafasi ya kutumika na ukitaka hapa Mawaziri hapa waite Wakurugenzi wao, Wakuu wa Idara, wawanyanganye simu, halafu wawape *laptop* mpya, waqambie tutengeneze mpango waone tutakachokipata. *(Kicheko)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijana wako kule wadogo ambao hawaonekani kwenye vyeo vyao, ndio wanaofanya kazi, hawa wana vyeo ndio, lakini uwezo wa kueleza humu hawana. Si huwa wanaingia kwenye Kamati, unauliza swali anauliza dogo unasemaje? Ndio anatoa majibu. Sasa tuwape madogo wakalie viti wafanye kazi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Haya ahsante sana, muda wako umeisha.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge ili watu pamoja na watumishi wasije kuwa hawajamwelewa vizuri Mheshimiwa Mbunge, maana isije ikapeleka ujumbe siyo. Hoja ya msingi ni kwamba watu washirikishwe ndio hoja. Kwa hiyo ukishirikisha wengi unapata mawazo mengi zaidi.

Ni sawa na hapa Bungeni, ambavyo Mheshimiwa Waziri unapata mawazo kutoka kwa Wabunge. Mwingine atachangia kilimo, mwingine atachangia hoja hii, kwa hiyo ni hivyo hivyo kwamba, hata Serikalini washirikishwe hata hao wa chini wanaweza kuwa na mawazo fulani, lakini haina hiyo sura ya kwamba pengine Mkurugenzi pale yeye ndio hana ajualo, analijua wa huku chini, hapana. Mkurugenzi ashirikishe wale walioko huku chini

10 NOVEMBA, 2022

na sio kwamba yeye pengine ana mapungufu yoyote. Kwa hiyo hilo likae vizuri na Mheshimiwa Mbunge mwakilishi na yeye awe na amani tele. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo atafuatiwa na Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi ajiandae.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipatia fursa ya kuchangia kidogo kwenye hoja ambayo iko mbele yetu. Napenda kuwapongeza Wizara ya Fedha kwa kazi hii nzuri waliyotuletea hapa na ambayo tunaijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Hasunga anasema hapa nilikuwa nasoma kitabu kimoja, kimeandikwa na *Professor Keith Penny, Professor of psychology and neuroscience*. Kwenye hicho kitabu kuna sentensi moja inasema "*it takes money to make money*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunachangia Kamati zetu zile tatu, kulikuwepo tatizo kubwa ambalo tulibainisha. Mashirika yetu mengi yanaendeshwa chini ya mtaji wake, yanahitaji mtaji. Kulingana na hiyo *quote* ambayo nimeisema, bila kuwekeza kwenye mashirika yetu ya umma tusitegemee miujiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kidogo kwenye kilimo, kwa sababu watu wengi miongoni mwa watu wangu wa Muleba ni wakulima na kama tunavyofahamu zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wamejikita kwenye kilimo.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tatizo tulilionalo kama nchi, wasemaji wengi wamesema, tunalo tatizo na lazima tutafute tumejikwaa wapi ili tuweze kutoka pale. Nikiangalia mfumo wetu wa Taifa tumejifunga kwenye kanuni na sheria zetu ambazo nyingi zinatukwaza. Kule kwetu Mheshimiwa Bashe anafahamu nitemwona pale, kila ikifika mwezi Julai lazima nimwone Mheshimiwa Bashe. Sisi ni wakulima wa kahawa, lakini ikifika mwezi Julai, Agosti tuna *task force* nyingi kuliko *think tanks* za kutuletea suluhu ya matatizo yetu. Tutaunda *task forces* tunaanza kukimbizana na wakulima wadogo wadogo wenye gunia moja, debe mbili eti magendo, tunawakwaza wakulima na wengi wanakata tamaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko kwetu watu wengi walingoa mibuni na tunayo Sheria ya Kahawa, inasema eti kahawa ni mali ya Serikali. Kati ya sheria mbovu na hiyo ni moja ya sheria mbovu. Mheshimiwa Bashe wakati tunaongea pale alisema anataka *free market*, sasa inapokuja *free market*, *let make it a free market for every crop for every business*, tufungue soko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo taasisi za udhibiti, tunayo taasisi ya *Fair Competition* katika nchi hii, tuiachie ifanye kazi yake. Wakati mwingine tunakimbizana na hawa watu wadogo wadogo hawa, ukiangalia wakulima wa kahawa kwa mfano Kagera, zaidi ya asilimia 90 ni wakulima wadogo wadogo ambao baada ya kuvuna mazao yao tunaanza kukimbizana nao. Hayo mazao wanayapeleka wapi? kama kule wanakoyapeleka kuna soko zuri, bei nzuri, kwa nini tusije na utaratibu mzuri tukawawekea utaratibu mzuri wakauze kule tukakusanye kodi sisi kama Watanzania? Kuna tatizo gani kwenye hilo? Tuachane na mfumo wa ku-*paralyze* soko kwa

10 NOVEMBA, 2022

kuwafungia wakulima kana kwamba ni wezi, kana kwamba ni *smugglers*, kana kwamba yaani hawana; mazao wamezalisha wenyewe lakini tunapambana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye uvuvi, tatizo ni lilelile. Ukiangalia tozo za sekta ya uvuvi na ukizilinganisha na nchi nyingine, ndio maana ukiangalia nchi jirani Uganda, Kenya wanafanya vizuri kwenye uvuvi. Sisi wenye sehemu kubwa ya ziwa tunapata mapato kidogo kwa sababu ya tozo tulizonazo. Huu siyo muujiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye tozo tulizonazo kwa mfano *fillet*, Tanzania ile viwango vya tozo kwa kilo tunatoza shilingi 552, wenzetu Uganda wanatoza shilingi 115, Kenya shilingi 34.51 hizi ni hela za Kitanzania. mabondo sisi tunachaji shilingi 7,500, wenzetu Uganda shilingi 460, Kenya shilingi 34. Vichwa vya samaki sisi tuna-charge shilingi 46, wenzetu Uganda shilingi 115, Kenya shilingi 34, ndio maana tunakula vichwa hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni mtu gani ambaye ataingia kwenye ziwa akuletee wewe mazao ya uvuvi badala ya kuyapeleka kule ambako tozo na tozo nyingine ziko *much more user friendly*. Sisi kwetu tozo ziko juu sana, tuangalie haya mambo Mheshimiwa Waziri wa Fedha tunapokuja kutengeneza hizi. Tunavutiaje haya mazao kwetu? Ndio maana Uganda tunavyoongea wana viwanda 20, sisi tuna viwanda nane, Kenya wana viwanda vitano, lakini ukiangalia ziwa tunalolimiliki sisi ni zaidi ya asilimia 50, liko kwa upande wetu. Hata ukiangalia mauzo ya nje, tunavyoongea leo, Uganda wanafanya vizuri zaidi kuliko sisi na nchi ya pili baada ya Nigeria, lakini sisi tuko wapi kwa sababu ya mifumo

10 NOVEMBA, 2022

tuliyojiwekea ya sheria, kanuni, tumejifungia kiasi kwamba tunajitengeneza umaskini sisi wenyewe kwa kujua au kutokujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana Mheshimiwa Hasunga alikuwa anasema *we are living in the cycle poverty* na hii tumeitengeneza sisi wenyewe kwa kanuni zetu, sheria zetu. Tukae chini tuangalie ni wapi kanuni zetu zinatufunga, ni wapi sheria zetu sio nzuri, ni wapi *competitive advantage* tunaweza tukaitumia tukijilinganisha na mataifa jirani, tusijifungie ndani, tukadhani sisi ni kisiwa, sisi tunafanya biashara peke yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga hoja mkono. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu ajiandae.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye mapendekezo ya Mpango wa Bajeti. Nina mambo machache ambayo nataka nichangie. Kwanza ni kwenye kilimo, kwanza nimshukuru sana Waziri kwa mikakati yake ambayo ameanza kuifanya kuhakikisha kwamba kilimo kinakuwa na nafasi katika nchi hii, lakini kuna mambo ambayo tunahitaji kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012 nilipata nafasi ya kualikwa Ubalizi wa Marekani alikuwa amekuja, aliyekuwa *US Administrator wa USAID* alikuwa anaitwa

10 NOVEMBA, 2022

Rajiv Shah na yeye alikuwa na mpango wa kutaka Tanzania iweze kulima zaidi kwa kupitia taasisi moja ambayo tuliianzisha wanaita ile korido ya Kusini. Alitaka tuwe na benki ya ardhi ambapo yeye anaweza akaleta wawekezaji kutoka Marekani waje walime katika eneo kubwa. Akaonesha masikitiko yake, kwamba tangu aanze ku-support mambo ya kilimo, haoni hatua ambayo imeendelea, kwa hiyo alikuwa na mpango wa kujiondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu ni nini? kwa kuwa tunasema kwamba Tanzania ina asilimia zaidi 60 ya ardhi ambayo inaweza kulimika, tunaweza tukafanya mapinduzi makubwa sana kwenye ardhi, kwa kufanya nini? Lazima Serikali iwe na benki kubwa ya ardhi ambayo imeisajili na iko mikononi mwake. Mwekezaji mkubwa anapokuja hapa anataka kuwekeza tumwonyeshe kwamba tuna benki ya ardhi iko Morogoro tuna hekta 500,000, tuna hekta 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua wawekezaji wakubwa kutoka katika mataifa makubwa hawawezi kuja kuchukua heka 1,000 heka 2,000. Tuone katika mipango yetu ya baadaye, tutakuja kufanya nini katika hilo eneo. Maana vinginevyo tutakuwa na ardhi kubwa, lakini hatuwezi kufaidika nayo. Tuwe na mipango ya muda mrefu ya kuwa na Benki ya Ardhi ambayo tutaweza kuvutia wawekezaji kirahisi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kwenye kilimo, kwamba tunafahamu mabadiliko yanayoendelea ya hali ya hewa, mvua zimepungua sana. Naomba Serikali isichelewe, tuwe na mpango endelevu wa muda mrefu. Sehemu nyingi za nchi hii zina mabonde mengi mazuri. Tunaweza tukatengeneza haya mabanio kwa bei

10 NOVEMBA, 2022

ndogo sana. Huhitaji kufikiria mradi wa bilioni 10, 20 au 30, unaweza kutengeneza banio kwa bilioni moja na nusu, unafunga upande huu, upande huu, kwenye mkondo wa maji unatengeneza mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa na mabanio mengi katika nchi hii, tutaokoa majanga mengi ambayo yanatokana na wananchi kukosa mahali pa kulima na sasa hivi wananchi wengi wanakimbilia kwenye vyanzo vya maji kwa sababu hawana maji, sasa utafanya nini? Ni lazima wakimbilie tu huko, lakini kama tutatengeneza mabanio mengi, kwa mfano Mkoa wa Iringa *of course* na mikoa mingine yako maeneo mengi ya namna hiyo. Serikali isichelewe kwenye huo mkakati, vinginevyo itafika mahali tutaanza kulia wakati tutakuwa tumeshachelewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nione liwe kwenye mpango wa muda mrefu ni namna gani tutaendelea kuboresha mawasiliano vijijini? Unajua biashara nyingi na mifumo mingi sasa hivi ya kibiashara huwezi kuitenganisha na mawasiliano. Mwaka 2012 wakati nasimamia idara ya M-pesa nilipata nafasi ya kuanzisha kitengo cha M-commerce. Sasa kwenye M-commerce kwa maana ya mtandao biashara tuliingiza afya, kilimo na kwenye afya tulitaka kwamba tusajili vituo vyote vya afya, tusajili zahanati zote ambapo kwa kutumia M-commerce, biashara mtandao tulikuwa na uwezo wa kutoa taarifa kutoka katika vituo mbalimbali kusema hapa unaweza kupata dawa hii, dawa hii na mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye M-commerce tulikuwa na uwezo kwenye kilimo wa kujua hali ya hewa

10 NOVEMBA, 2022

ya kuweza kujua ni aina gani ya mbegu, wapi upande nini, ardhi inapatikana wapi, msimu wa kulima na mambo kama hayo. Yote hayo yanafanyika kwa njia mtandao, ndio maana ni muhimu sana kuwa na mipango ya baadaye ya kuboresha mitandao ya simu vijijini kwa sababu ni njia ya uchumi na ya kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyoona sasa hivi ni njia rahisi sana kukusanya mapato kwa kutumia mitandao ya simu. Sasa kama hatujaweza kupeleka mawasiliano huko tutafanyeje? Kwani eneo lingine muhimu sana la kukuza biashara na uchumi wa nchi yetu. Hilo nalo katika mipango yetu ya baadaye hilo tuliweke na tuone tutafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye mazingira sio jambo la kuchezea. Tumekuwa tukisema mara nyingi hapa tulinde mazingira, lakini ukipita katika milima mikubwa hata kama Kitonga pale unakuta moshi unafuka katikati ya mlima. Sasa unajiuliza ni hatua gani kama Serikali tunachukua? Sasa kama moshi unafuka pale maana yake kuna watu wanachoma mikaa, sasa hili ni jambo la hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mikaa mingi sana inatoka katika nchi hii inaenda kuuzwa Burundi, Kenya na misitu yetu inazidi kuharibika. Sasa kwenye hili eneo la utunzaji wa mazingira kwa kweli kuna hao watu wa hizi kampuni ambazo zinajihusisha na kutunza mazingira wanasema miradi ya kuhifadhi mazingira pamoja na bioanuwai. Kwa hiyo kwamba ziko fedha nyingi sana ambazo tunaweza tukazivutia kwa kuziingiza halmashauri zetu, zikatengeneza maandiko mengi, tukahifadhi mazingira, tukapata fedha, tukafanya maendeleo

10 NOVEMBA, 2022

kwenye vijiji vyetu, lakini bado tumetunza mazingira *at the same time* tumepata pesa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda wangu umekwisha, naunga mkono hoja, mambo ni mengi lakini nitachangia kwa njia nyingine, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Hiyo uliyosema hiyo hiyo haijaingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, ulikuwa na maana ya *bioanuwai* ama kitu gani?

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, inaitwa *bio.....* hiyo hiyo. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Haya ni *bioanuwai*, ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka ajiandae.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nijielekeze kwenye umuhimu wa kukuza Pato la Taifa letu. Kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu wa Makazi ya mwaka 2022 inatanabaisha kwamba idadi ya watu nchini ni takribani milioni 61.7 vilevile inaendelea kusema wastani wa ukuaji wa watu Tanzania kwa mwaka ni wastani wa asilimia 3.2. Nimejielekeza kwenye mpango huu pia unaelekeza kwamba uchumi wetu unakua kwa wastani wa asilimia 5.4. Kwa hiyo,

10 NOVEMBA, 2022

ongezeko la watu lina mahusiano ya moja kwa moja na Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *actual growth* ya Pato la Taifa letu, ukuaji halisi wa uchumi wa Pato la Taifa letu siyo 5.4 ni 2.2 kwa sasa. Unawezaje kupata *actual growth* kwa maana ya wastani halisi? Unachukua wastani wa Pato la Taifa ambalo ni 5.4 unatoa wastani wa ukuaji wa watu ambao ni 3.2. Kwa hiyo wastani halisi kwa sasa nchini wa ukuaji wa Pato la Taifa ni asilimia 2.2 ambacho kile kimebaki baada ya *ku-minus and I stand to be corrected*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiribu kueleza tunawezaje kutoka hapa? Tuna kila sababu ya kuongeza bidii kwenye vichochea Pato la Taifa, walau tufike kwenye asilimia nane au kumi. Nilikuwa najaribu kuwaza kwa sauti kama sasa hivi wastani wa ukuaji wa watu ni asilimia 3.2; je miaka hamsini ijayo Tanzania itakua ya aina gani? Tumejipangaje kama Taifa kwa idadi ya vizazi hivyo vijavyo? Bado kuna changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nijielekeze kwenye maeneo ambayo tukiwekeza tunaweza kufikia asilimia nane mpaka kumi ya ukuaji wa Pato letu la Taifa. Jambo la kwanza ni utafiti. Utafiti kwenye kilimo, utafiti kwenye viwanda, utafiti kwenye madini, utafiti kwenye masoko na biashara, hali kadhalika na utafiti kwenye mazao ya mifugo ya samaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najjuliza pia maswali kuna Chuo kama *SUA* hivi hatuwezi kubadilisha mfumo wa elimu tukaondokana na tafiti au *academic research* kwamba ili mtu apate *Degree* lazima awe amefanya *thesis* amefanya *research* fulani lakini ile

10 NOVEMBA, 2022

inaenda kukaa kwenye kabati tu. Sasa hatuwezi kuwekeza kwenye Vyuho Vikuuu tukapata tafiti ambazo ni *practical* mbona Madaktari wanaweza? Kwa Madaktari wanafanya, Daktari Bingwa wa Moyo anakwenda kufanya tafiti lakini ni *practical* kwa nini watu wa kilimo wasifanye? Kwamba zao fulani linaweza linaweza likastawi sehemu fulani, ardhi fulani na ikiwezekana na bahati mbaya nilikuwa naona kengele ngoja niende haraka haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona jitihada za Mheshimiwa Rais, ameenda China tumepata Soko la Parachichi sasa najiuliza maswali tumejiandaaje kukata hiyo *market* ya parachichi? Kwenye suala la kilimo, tunaona jitihada za sekta ya kilimo lakini tunawekeza nguvu hizi kwenye biashara ya kilimo kimkakati? Kwa mfano, Bonde la Mto Kilombero kuna Bonde la Hifadhi lakini kuna Bonde linalofaa kwa kilimo. Je, tumejifikiriaje kuweka Miradi ya Umwagiliaji? Kwenye Bonde la Mto Kilombero? Tuna mikakati gani ya kuwekeza eneo hilo? Sasa hayo ni mambo ya kuangalia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nilikuwa nashanga sana leo hii korosho inalimwa Dodoma, Mwanza kila sehemu korosho tu jamani hii korosho inatija gani kwa nchi hii? Tuache Mtwara, walime korosho na sisi watu Mlimba, tuwe na zao maalum la mpunga tuzalishe mchele, lakini navyozungumzia viwanda, nazungumzia viwanda kwa maana siyo vile viwanda vya tunasema viwanda vikubwa nazungumzia *agro-base industry* ni viwanda vinavyochakata malighafi kuwa bidhaa hiyo ndiyo hoja yangu ya msingi. Tukiwekeza kwenye viwanda maana yake vijana watapata ajira lakini pia tutaongeza Pato la Kigeni.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia Urari wa biashara nchini kwenye *East Africa* tunafanya vizuri na *SADC Countries*, lakini huko Duniani tuko mbali mno kwenye urari wa biashara ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, tunayo kazi ya kufanya ili tuweze ku-*capture* hiyo *market*. Pia kuna urari wa malipo tunasema *balance of payment* bado tunakwenda kwenye hasi *unfavorable balance of payment* kama Taifa. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri yupo hapa uchumi, Waziri wa Fedha atusaidie kwenye eneo hili, mipango hii tunayosema sisi basi ichukuliwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende mwisho kwenye sekta ya ardhi. Nilikuwa nafuatilia sensa ya watu na makazi idadi ya majengo ni 13,907,951. Idadi kwa maana ya wakati kuna mapitio ya bajeti idadi ya viwanja vilivyopimwa ni Millioni Sita, idadi ya Hati Miliki nchini ni Milioni Mbili. Kwa hiyo kama idadi ya majengo yako Milioni 13 kuna idadi ya watu wenye majengo ambao hawajapimiwa zaidi ya Milioni Saba. Sasa hiyo ni sekta ya sehemu nyingine, pia kuna idadi ukitoa Milioni Mbili watu wenye Hati Miliki maana yake kuna idadi ya Million 11 ya Watanzania hawalipi kodi ya ardhi. Sasa hili eneo ni fursa kwetu nampongeza sana Waziri wa Ardhi anatatua migogoro kwa kutumia hii kliniki, nimeona juzi pale Kibaigwa. Mama anafanya kazi nzuri, kama kutatua migogoro kwa kutumia kliniki na nikuombe Mheshimiwa Waziri, kliniki hii ifanyike na kule Morogoro, isifanyike tu Dodoma. Kliniki endelevu tembezi inasaidia kutatua migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto tuliyonayo ukiangalia ardhi, nikuombe dakika moja tu nimalizie, samahani ahsante. Tusitazame sekta ya ardhi kama migogoro, migogoro ni matokeo ya kutokufanya vizuri

10 NOVEMBA, 2022

kwa sekta. Kwa hiyo, tukijielekeza kwenye mipango bora ya matumizi ya ardhi hakika Taifa letu litaenda kutatua migogoro yote ya ardhi. Baada ya kusema hayo, ahsante sana na Mungu akubariki sana (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, atafuatia na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka ajiandae.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi nichangie huu mpango wetu, Mpango wa Tatu wa maendeleo katika nchi yetu. Pamoja na muda nisiache kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na kuendelea kumpa moyo mkubwa kabisa kwamba kazi anayoendelea kuifanya kwenye nchi haina mfano na tunaendelea kumuomba kwa Mungu aendelee kumpa afya njema ili Watanzania waweze kuendelea kuona matunda yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitasema jambo moja tu ambalo Serikali imeanza kulifanyiakazi lakini naona hatuendi nalo kwa speed nalo ni eneo la usimamizi wa maafa nchini. Nikitambua tayari Kifungu cha 35 cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 kinaeleza wazi juu ya kuanzishwa kwa Mfuko huu, lakini ukweli Serikali hapa kupitia Kamati ya Kudumu ya Sheria na Katiba Mwezi Februari 14, 2022, Kamati iliwasilisha hapa juu ya Mapendekezo ya Muswada wa Sheria kwenye jambo hili. Septemba mwaka huu 2022 Waziri Kaka yangu Simbachawene naye aliwasilisha Muswada wa Sheria wa Usimamizi wa Maafa Nchini, ni jambo jema sana.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba bado Mfuko huu aujaanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti. Lazama tukubaliane inawezekana umuhimu wenzetu hawajaujua bado. Kwa nini tunahitaji kuharakisha mfuko huu kupatikana? Niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge, juu ya majanga mengi nchi ambayo tumewahi kuyapata katika kipindi cha miaka kadhaa. Mwaka 1996 Tarehe 21, Mei, tulipata maafa makubwa kupitia *MV Bukoba*, wananchi wanajua. Ni kweli kupitia taarifa ya Jaji Robert Kisanga tuliweza kupoteza wananchi wetu, watoto wetu, wazee wetu 391 dhidi ya waliokolewa 114 tu, unaweza ukaona hili ni janga!

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu ni juzi tu *MV Spice* tarehe 10 Septemba 2011, zaidi ya maiti zilipatikana 243 lakini waliokutwa hai ni 900 tulipoteza hawakupatikana kabisa zaidi ya 1,370 hata kupatikana. Niwakumbushe tena kwa haraka kupitia maji tu Bahari na Maziwa ajali kubwa ya *MV Skagit* mwaka 2012 wananchi zaidi ya 222 walipoteza maisha, kuna *MV Julius* mwaka 2017 pia *MV Nyerere* mwaka 2018 ambayo ilikuwa inatokea Bungarara kuelekea kwenye Kisiwa cha Ukara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya majanga ni makubwa kama nchi. Tumepoteza ndugu zetu wengi, nini maana ya Mfuko huu? Mfuko huu utatusaidia pale ambapo haya majanga ambayo yameendelea nimeyataja ikijumuishwa hata hiyo ya juzi ya ndege, tungeweza sasa hapa kuona fedha za haraka za dharura ambazo zingeweza kusaidia hata kupeleka Jeshi letu la Navy la Uokoaji, katika maeneo ya kimkakati na tukaweza kuwawezesha kupitia Mfuko huo. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile moto. Masoko yetu mengi, Soko la Kariakoo tumeliharabati kwa Billion 32, Mheshimiwa Waziri Mkuu alienda pale kukarabati tu, Soko la Mwanjelwa - Mbeya, Soko la Ilala kwa Naibu Spika lakini hata Mwenge zaidi ya bilioni 50. Madhara yake ni nini kama hatuna Mfuko huu? Madhara yake mpango wa kama huu na bajeti zetu tunazoziweka kila mwaka zinaenda kuharibiwa, maana yake yale tunayotarajia kuyafanya *activities* zinazotakiwa kufanywa haziwezi kufanyika. Kwa sababu dharura imekuja hatujajipanga nayo tunaenda kuchukua hela maana yake ni *activities* nyingine zinaweza zisifanyike. Kwa hiyo, ni maombi yangu sana Mfuko huu ninajua nia na dhamira ya Serikali ndiyo maana tumeanza na sheria basi tuelekee kwa sababu ndiyo nia yake kwenda kuanzisha Mfuko huu tukaanzishe haraka ili tuweze kufika sehemu salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mengi watu wanayajua. Mlima Kilimanjaro zaidi ya siku 15 tumeshindwa kuuzima hata ule moto ni hatari, haya madhara yake ni makubwa karibu hata manne, moja ni uchumi wa nchi yetu lakini la pili ni mapato watalii hawawezi kuja leo kwa haraka lakini vilevile ina-*distort* hata ile *goodwill* ambayo tunayo kama nchi ndani ya vivutio vyetu hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ajali hizi zinawapa umaskini watu wetu. Amezungumza *role model* wangu, Mheshimiwa Kaka yangu pale Mheshimiwa Hasunga, kwamba ni ukweli mpango wetu unazungumzia juu ya dhima ya kuona maendeleo ya watu wetu. Sasa kama watu wetu wanakufa na hatuna mipango ya dharura kutengeneza Mfuko wao hili dakika ikifikia pale tunachukua.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka, leo tunafanya nini kwa sasabu hatuna mfuko huu? Tunaenda Fungu 21 tunachukua hela pale haiwezekani, hatujawahi kuukuta ule Mfuko lile Fungu 21 lina hela muda wote. Kwa hiyo, ni vizuri na ni muhimu sana tufike sehemu tuone umuhimu wa Mfuko huu.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa kengele ya pili imeishagonga.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda ajiandae.

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Mpango huu wa Bajeti wa Mwaka ujao wa Fedha kama ulivyowasilishwa na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa ambayo imeletwa hapa ya mpango tumeona ukuaji wa uchumi katika kipindi cha Januari mpaka Juni 2022. Tumeona uchumi wetu umekua kwa asilimia 5.2 katika nusu mwaka hii na kuna sekta ambazo zimeongoza katika ukuwaji huu ni sekta ya maji safi na maji taka ambayo imekua kwa asiliamia 10.7, bima asilimia 10, umeme asilimia 8.5,

10 NOVEMBA, 2022

madini na mawe asilimia 7.1 na nyinginezo. Ukuaji huu kwa robo hii umekwenda vizuri lakini ukuaji huu hauendani sambamba na mfumuko wa bei ulivyo. Tunaona kipindi cha Agosti, 2022 mfumuko wa bei kwenye upande wa vyakula na vinywaji ilikuwa ni asilimia 7.8 ambapo hii ni ongezeko kubwa, ambapo kipindi cha Agosti mwaka uliopita mfumuko wa bei ulikuwa 3.6 kwa hiyo, mfumuko wa bei umekwenda mara mbili zaidi ya hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachotaka kusema ni nini? Nikwamba uchumi wetu unakua lakini auendi sambamba na mfumuko wa bei, kitu ambacho ni hatarishi sana kwenye uchumu wa nchi yetu. Nikiangalia kwenye mpango hapa hakuna namna yeyote ile yakuweza kukabili mfumuko huu wa bei. Tunaacha tu *nature* iweze ku-*take place* kitu ambacho ni kibaya, niombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, uangalie wewe pamoja na Wachumi wa kwako ambao amekuzunguka, namna ambavyo tuwe na mipango endelevu ya kuhakikisha kwamba mfumuko wa bei huu tunaenda kwenda kuutatua kwakuwa na mipango ya muda mfupi na mipango ya muda mrefu, bila hivyo tutakuwa hatuwezi kufika kule tunakotaka kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango huu wa Bajeti, tumeona kwenye msimu wa 2021/2022 uzalishaji wa chakula ulikuwa tani milioni 17.4 na kwenye mpango huu wa bajeti wamekadiria mahitaji ya chakula ya kwetu sisi hapa ni tani milioni 15. Hata hivyo hawajaonesha namna ambavyo uzalishaji wa kwetu sisi utakavyokuwa. Sasa tuna mipango mingi ambayo inakwenda, tunawekeza kwenye kilimo lakini hatuna mpango wa kuonesha kwamba uwekezaji wetu huu utazalishia kiasi

10 NOVEMBA, 2022

gani? Kitu ambacho kwenye uendeshaji wa uchumi wa kwetu tunakuwa tunakwenda kwa sababu tu tulitakiwa twende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri tu Wizara fedha, pamoja na Wizara ya Kilimo, muweze kukaa muwe na mipango kuonyesha kwamba kiasi ambacho tunakwenda kuwekeza kwenye upande wa kilimo tunategemea uzalishaji wetu utakua kiasi hiki na matumizi yetu yatakuwa kiasi hiki na hii ziada itatuwezesha sasa kuweza kuuza nje, kama mnavyojua, fedha nyingi ambazo tumeweza kuwekeza kwenye bajeti ambayo imepita tunaimani utekelezaji kwenye kilimo ukienda vizuri uzalishaji utakua zaidi na ukikua zaidi hii ni fursa kwetu kwa hizi bidhaa zetu za mazao kwenda kuuza nje ya nchi na tukaweza kupata fedha za kutosha na badae uchumi wetu ukakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri tukifanye kilimo chetu hiki kuwa cha kibiashara. Tumekuwa tunakizungumza kwa nadharia kwamba tunawekeza kwenye kilimo lakini tunaenda kufanya kilimo hiki kwa mazao ya kuweza kujikimu. Tutoke hapa tulipo twende kwenye mazao ya kibiashara ili haya tunayoyasema yaweza kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze pia kwenye upande wa Miundombinu. Naona hapa kwenye bajeti na kwenye mpango huu wa bajeti kuna mambo makubwa yameelekezwa kwenye miundombinu. Nichukulie mfano kwenye SGR tunajenga hapa, tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kujenga na mambo yanaendelea vizuri lakini bado hatujawa na mpango endelevu kuweza kuhakikisha

10 NOVEMBA, 2022

kwamba reli hii itaweza kuwa na tija kwetu sisi. Leo tunajenga reli hii kwenda Mwanza, kule Mwanza hakuna mzigo wa kututoa Dar es Salaam kutupeleka Mwanza, sasa hivi hapa ili reli iweze kutulipa, iweze kulipa tunapoweza kusafirisha mizigo mingi na ya kutosha na mizigo pekekee ambayo inaweza kututosheleza na uchumi wetu kuweza kukua ni kututoa Dar es salaam kwenda Kigoma na baadae *DRC* ndiyo inachukua mzigo wa asilimia Sabini ya unaopita Bandari ya Dar es salaam lakini sisi tumeelekeza reli yetu kwenda Mwanza kusafirisaha abiria badala ya kupeleka Kigoma ambapo tutapeleka kule mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Serikali iweze kupitia upya ione namna nzuri zaidi reli hii sasa tuwekeze nguvu ambayo itapeleka mizigo hii na badae itaweza kutusaidia. Hii ni reli ya kati lakini pia kwenye mpango tuone namna ambavyo tunaweza tukaiboresha reli yetu ya *TAZARA*. Reli ya *TAZARA* siyo kuboresha tu miundombinu peke yake. Reli hii tuone namna ambavyo, namna ya uwanzishwaji wake, namna uendeshwaji wake baina ya hizi nchi mbili. Tukiweza kutatua hili ndivyo ambavyo baadae tutaenda kwenye miundombinu na baadae tuone namna ambavyo itaweza kutusaidia. Kuna mizigo mingi inatoka hapa inaenda Zambia, kuna mizigo mingi inatoka Zambia shaba inatoka kule inakuja Dar-es-Salaam leo hii awatumia *TAZARA* wanatumia barabara, barabara hizo wanazotumia zinaishia kwenda kuharibu barabara zetu kwa malori haya na sisi tunakuwa hatunufaiki wakati reli tunayo na kusudi kubwa la reli lilikuwa kuhakikisha kwamba miundombinu hii inakua vizuri zaidi *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda wenyewe siyo rafiki. Nitakuandikia kwa maandishi ili niweze kuleta mchango wangu. Ahsante sana

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda na Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe ajiandae.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii yakuchangia katika mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kuweza kuajiri watumishi wa TRA. Kamati yangu imekuwa ikipigia kelele sana ufanisi wa kazi wa TRA na tuliona kwenye ripoti yetu tuliyoleta, jinsi ambavyo kumekuwa na shida katika kukusanya kodi. Kwa hiyo, unakuta kwamba madai yanaongezeka kutoka trilioni 3.9 mpaka trilioni 7.5 ambayo ilikuwa kama asilimia 95 ya madeni ambayo hayakukusanywa kwa mwaka wa 2020/2021. Najua kwamba Taifa letu linategemea sana kodi na kama hazikukusanywa na hata hii Mipango tunayoongelea haiwezi kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi nataka nichangie tu katika eneo moja, hili eneo liko chini ya sura ya tatu ya maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2023, Namba 332, ambayo inazungumzia kilimo, mifugo na uvuvi, Ukurasa 124. Ni aibu kwa Taifa letu, na ninamuona Waziri Ndaki ananiangalia sana, kwamba, sasahivi Taifa letu hapa tulipofikia na baada ya kuwa na Wizara nzima ya Mifugo bado watu wafugaji, hatuwaiti

10 NOVEMBA, 2022

wafugaji, wachungaji, wanakimbizana na ng'ombe, ng'ombe waliochoka, ng'ombe waliokondeana, halafu ng'ombe hawa wanaenda kulishwa kwenye mashamba ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema sisi kazi yetu kubwa hapa kwenye Bunge ni kutetea wanyonge. Hakuna watu wanyonge waliozidi wafugaji na wakulima. Sasa unashangaa tunaacha haya makundi mawili yanamalizana. Hivi karibuni tumeshuhudia watu wakikatwa mapanga, watu wakiuana kwa vile makundi ya ng'ombe yanaswagwa kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine na yanashambulia mashamba ya wakulima. Swali langu najjuliza, hivi tuliunda Wizara nzima ili nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifanya *cost benefit analysis* ya Wizara nzima na kazi inayofanyika sijui kama ita-*balance*. Mimi nilitegemea, kama kilimo walivyosema, kwamba wanatenga *blocks* kubwa vivyo hivyo nilitegemea mifugo yetu, wale wafugaji wetu watengewe maeneo. Wale wenye ng'ombe wengi wanaweza kuelezwa wakaambiwa kwamba tunakupa eneo hili kama linakuwa *fenced*, kama wanapeleka miundombinu na wao wachangie ili waweze kufuga mifugo ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba, Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, alilizungumzia sana hili suala la wachungaji akiwa Rais. Aliomba sana Serikali iangalie namna ya kuondokana na kuswaga ng'ombe tuwe wafugaji badala ya wachungaji. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Rais Mstaafu Jakaya Kikwete ametoka imekuja awamu ya tano na sasa ya sita. Leo ndio tunaona vita vikubwa sana kati ya wakulima na wafugaji halafu Serikali tunaangalia. Unashangaa hivi hawa wafugaji wana nguvu gani kuliko Serikali kiasi mtu anaamua kuswaga ng'ombe na kuingiza kwenye mashamba ya wakulima? Kwa hiyo umasikini wetu huu tunauzungusha wenyewe, *vicious circle* ya umasikini wetu wa nchi, matokeo yake tutaanza tena kuomba chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo tunajua faida yake kubwa. Kwanza wenzetu wengi walioendelea wageni wanaokuja nchi hii wana-*import* nyama kutoka Botswana au kutoka nchi zao, nyama yetu ukila hap ani *plastic* ng'ombe wale walivyo. Sasa tunashindwaje kuweka viwanda kule Shinyanga tukasaidia watu wetu wafugaji kule wakatengewa maeneo, wakafundishwa kuweka majani ya kisasa, wakatengeneza hata *bio gas* ili wawe na nyumba zile wasiingie hasara za kutumia umeme huu wa *grid* wakawa na *silage* ile ambayo wanaweza wakitoa *biogas* wanaweka kwenye majani, wanaweka kwenye mimea? Ni kazi ngumu gani kuona kwamba, kule tungeweza kuweka viwanda vya ngozi, viwanda vya maziwa na *by products* nyingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu kwato zile zinatengenezea *jelly*, ile gundi. Sasa sisi Tanzania tunacheza. Angalia wenzetu wa Botswana wameona kwamba sasahivi almasi walikuwa wanaitegemea, Ulaya na Marekani sasahivi wanatengeneza almasi *fake*, hawana soko, wamezamia kwenye mifugo tu. Na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Mchemba ametuwekea *data*

10 NOVEMBA, 2022

jinsi ambavyo wenzetu uchumi umekua katika muda huu mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana na Waziri wangu wa mifugo namheshimu sana, Waziri Ndaki, hebu angalia tuweke *blocks* tuchukue vijana wetu hawa waliosomea mambo ya mifugo tuwawezeshe. Hizi fedha zote zinazotolewa kwenye vikundi wapewe, wawezeshwe, watengenezewe maeneo waweze kufuga kisasa. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Kirumbe Shabani Ng'enda, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Mlagila Jumbe. Mheshimiwa Salim Almas Alaudin ajiandae.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweke mchango wangu kwenye mpango huu wa maendeleo wa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama uelewa wangu uko pamoja na wenzangu ni kwamba, kadiri tunavyojadili mpango huu tunajaribu kuona vipaumbele katika mpango wetu vitakavyosababishia kuweka sura ya bajeti yetu inayokuja ya 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma, miaka mitano iliyopita, ukiangalia maendeleo ya Taifa letu yalijielekeza katika kuwekeza nguvu kubwa kwenye viwanda na suala zima la madini. Na sasa ukiangalia mwelekeo tulionao sasa na hasa ukiangalia bajeti tuliyoipitisha ni kwamba mwelekeo mkubwa sasa tumejielekeza katika kilimo, na hili ni jambo jema sana.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niseme, hata tulipokuwa tumeamua kujielekeza katika viwanda na kuweka nguvu kubwa katika viwanda, viwanda tulivyovikusudia si vingi vilivyowekwa. Viwanda tulivyovikusudia ni viwanda vya kuchakata mazao ya wakulima na wafugaji ili kuyaongezea thamani ili tuweze kuwatoa watu wetu katika umasikini. Hata hivyo viwanda vilivyoibuka vingi vikawa ni vya kutengeneza nondo, saruji, kutengeneza malumalu, sijui kutengeneza nini, mambo chungu nzima ambayo kwa kweli, haya *add value* ya mazao ya wakulima, wafugaji na wavuvi. Kwa hiyo, ulikuja msemu wa wenzetu ambao wako nje, yaani maana ya nje ya Serikali, wana-*challenge* wakasema tumejielekeza katika maendeleo ya vitu kuliko maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msemu huu ulichukua nafasi kubwa sana ya mijadala, lakini tulikuwa *right*. Maendeleo ya vitu waliyokuawa wanayasema, kwamba tulijielekeza katika kutengeneza barabara, kujenga shule, hospitali na viwanja vya ndege. Tulifanya hivi kwa sababu, hata kama ukitaka kuwasaidia watu kuwainua kiuchumi kama miundombinu si rafiki basi hao wakulima wako hawawezi kupata soko zuri la mazao, hao watu wako kama hawana hospitali hawawezi kuwa na afya nzuri na kuweza kumudu uhindani kwenye uchumi, kwa hiyo tulikuwa tuko *right*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nafikiri sasa ni lazima tujielekeze sasa katika maendeleo ya watu. Kazi tuliyoichukua kwa kipindi kirefu, ya miundombinu, shule, sijui hospitali na nini, kwa kweli naweza kusema tumepiga hatua kubwa sana tukijilinganisha na nchi nyingine za Afrika, hatua ni kubwa sana. Nchi zote za jirani zetu hapa hakuna nchi inayoweza ikajilinganisha na sisi katika

10 NOVEMBA, 2022

miundombinu. Tumekopa, tumefanyaje tukasema tutengeneze mazingira yatakayowafanya watu wetu, wakulima wetu waweze kufikisha mazao sokoni, watu wetu waweze kufika mahali kupata huduma za afya nzuri, waweze kupata elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huko tunakotaka kwenda kusaidia maendeleo ya watu ni kupi? Ndio kitu ambacho nataka nikizungumzie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja. Tunataka wakulima wetu wapate bei nzuri za mazao ili kipato chao kiongezeke maendeleo ya watu yainuke. Kwa hiyo, mpango huu lazima utuelekeze katika namna gani tutawatoa wananchi katika kuwahimiza limeni, baada ya kulima halafu kufika mahali mazao yanaoza hayapati soko. Lazima mpango huu utueleze tunafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile mpango huu utueleze namna gani tunawasaidia wasomi wetu ambao wamesoma, hawajapata ajira lakini wanataka kuchangia katika uchumi wa Taifa, mpango huu ni lazima utueleze. Na huu katika kutueleza ni kwamba, watu wengi wanayo mipango mizuri ya kukuza uchumi na kuendeleza Taifa lao lakini hawana mitaji. Wakienda benki si rafiki katika kutoa mitaji kwa watu wanaoanza. Kwa hiyo ni lazima tufike mahali tuseme ni namna gani tunaelekeza benki zetu na vyombo vya fedha kuwezesha watu wetu ambao wana elimu, wana ujuzi, wana maarifa, lakini hawana mitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu mikopo nafuu. Tumeweka mikopo ya vijana wanawake

10 NOVEMBA, 2022

na walemavu asilimia 10 ya Halmashauri. Ni kiasi kidogo sana. Leo tunataka tuone kwenye bajeti yetu itakayokuja tuweke fedha kwa ajili ya kuongeza mfuko wa wanawake na vijana, tusitegemee asilimia 10 za Halmashauri tu, haziwezi kututoa mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimeona Wizara ya Mifugo na Uvuvi wamekuja na mpango mzuri sana wa kusaidia kuinua watu na hasa kwenye uvuvi. Wamekuja na mikopo isiyokuwa na riba ya maboti za uvuvi, mashine, vifaa vya kuhifadhia samaki na rada. Mimi naomba sana tunapokwensa kwenye bajeti inayokuja hebu tuweke fedha za kutosha hapa, uvuvi unaweza ukasaidia kuongeza Pato la Taifa kwa kiasi kikubwa sana. Tunayo maziwa makubwa kama ziwa letu ya Tanganyika pale lakini imefika mahali ambapo uvuvi hauchangii pato la Taifa kwa kiasi kikubwa, ni kwa sababu hatujawawezesha na hawawezi kwenda benki. Hata hivyo fedha hizi zilizotengwa na Serikali kwa ajili ya boti na vifaa hivyo ni chache sana, tunaomba kwenye bajeti hii inayokuja tutazame namna ya kuongeza fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wafanyabiashara. Wafanyabiashara nao lazima tuwasaidie; na katika kuwasaidia ni kwamba, hivi kweli jamani bado tunafikiri ni muhimu kuwa na VAT ya asilimia 18? Mbona huu ni mzigo mkubwa sana? Hebu tuweke VAT kidogo iweze kulipika sana. vilevile mfumo wa VAT, kama ni watu wote wafanyabiashara wawe VAT registered kwa sababu gani; wale waliosajiliwa kule kwenye VAT wanaumia kuliko wale ambao hawakusajiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri... aah, muda umeisha?

10 NOVEMBA, 2022

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Malizia sentensi yako.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ambalo ningemaliza katika hilo ni kwamba, Halmashauri zetu zimeonesha, kwa mujibu wa Taarifa ya CAG zimekusanya vizuri fedha asilimia 94 kuliko hata Serikali Kuu kupitia TRA ambapo kwenye malengo wenyewe walifikia asilimia 86.6. Katika hali hii tuwaongezee nguvu, na katika kuwaongezea nguvu bajeti inayokuja Madiwani na Wenyeviti wa Mitaa tuwaongezee fedha wapate namna ya kusimamia vizuri Halmashauri zetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham. Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ajiandae.

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tazama ramani utaona nchi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nzuri kuliko zote duniani ni Tanzania; na si kwamba, ni Tanzania tu ambayo imejaliwa, Tanzania hiyo ni Tanzania ambayo inatoa mwanamke bora sana duniani anaitwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu...

MHE. HAMISI S. TALETALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

10 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Nani, Mheshimiwa Jumbe kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Hamisi Taletale.

T A A R I F A

MHE. HAMISI S. TALETALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, alipoimba nilikuwa nataka kuingia chini ya meza. Kwa hiyo, nimuombe asirudie tena kuimba nyimbo nzuri akiwa anatutisha, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa...

MHE. ALLY J. MLAGHILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea Taarifa hiyo kwa sababu yeye ni *talented* sina haja ya kumbishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kusisitiza kwamba, Tanzania hii ni nchi ambayo imebarikiwa sana. Inatoa mwanamke bora kabisa ambaye anaitwa Samia Suluhu Hassan ambaye ndiye Rais wa nchi hii. Ni nchi hii duniani ambayo inatoa Spika bora kabisa, *a super woman*, anaitwa Tulia Ackson. Ni nchi hii inatoa Mawaziri bora kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka tu niseme katika hali ya nchi kama hii ni lazima tufike wakati tujue kwamba, sisi tunaangaliwa na dunia nzima. Na tunapoangaliwa na dunia nzima ni lazima tuwe tunakubaliana kwamba, tumekuja hapa Bungeni kwa ajili ya hoja na si kutakiana ajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hili kwa masikitiko makubwa. Jana mchangiaji Mheshimiwa Festo

10 NOVEMBA, 2022

Sanga amechangia vizuri sana kuhusu suala la kuwatetea wananchi juu ya mambo ambayo yanaendelea Mbarali lakini matokeo yake imeonekana yeye hayupo kwa ajili ya kutetea wananchi bali ana maslahi yake. Sisi hapa tumekuja kwa ajili ya kuwatetea wananchi, hatujaja kwa ajili ya kufurahisha watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ameongea hapa Mheshimiwa Saashisha kuhusiana na suala la kutokutumia wataalam vizuri, tunatafutiana ajira. Nina mfano mmoja mzuri naomba niuweke hapa. Pale Bandari ya Tanga tulipokuwa tunasomewa taarifa hapa kulionekana kulikuwa kuna baadhi ya vitu ambavyo hazikuwa sawa. Aliyeibua mambo hayo nataka nikwambie, yupo mfanyakazi aliibua mambo hayo mpaka sasahivi hayupo kazini, alifukuzwa na hakuna mtu anayetaka kumjadili wala kuona kwamba anafaa kuendeleza bandari n ani mtaalam. Kuna jamaa mmoja anaitwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua kumtaja jina kwa sababu, namfahamu na yeye ndiye aliyeibua uozo, walipoona anaibua uozo huo wamemfukuza kazi. Ninaomba wanaohusika wawatafute hao watu watatusaidia kwa mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaongelea mambo ya kuanzisha Bandari ya Bagamoyo. Hivi bandari tulizonazo tumezitumia kwa uhakika?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

10 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Mlagila Jumbe kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora.

T A A R I F A

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali yetu inathamini sana misingi ya utawala bora, na kwa kuwa Serikali yetu imejipambanua kuhakikisha wkamba, inapambana na rushwa na inasimamia haki kwa watumishi wote wa umma ambao wamekuwa ni chanzo cha utendaji kazi bora, matumizi bora ya fedha na suala zima la maadili katika utendaji wa kila siku wa wawatumishi; kwa hiyo, kwa kuwa Serikali imejipambanua hivyo ninaomba tu nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge tuko tayari kumfahamu mtumishi huyo na kufuatilia kama iko misingi ya utawala bora imevunjwa kwa uadilifu na utendaji kazi uliotukuka kwa mtumishi huyo, Serikali itachukua hatua zaidi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe unapokea Taarifa hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri?

MHE. ALLY J. MLAGHILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea Taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Bagamoyo tunaisema sana hapa. Je, hivi Bandari ya Tanga tayari tumeshamaliza kazi zote zilizotakiwa pale, ili iweze kupokea mzigo? Ni kweli Bandari ya Dar es Salaam inafika wakati inaelemewa. Je, Bandari ya Mtwara ambayo ina

10 NOVEMBA, 2022

kina ambacho ni *natural*, ambayo iko vizuri, Je, tumeitumia ipasavyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba Bandari ya Bagamoyo tusiiseme kama bandari. Tukisema *industrial park* itakuwa ni nzuri zaidi, lakini tukisema juu ya bandari ninaomba bandari tulizonazo tuweze kuzitumia ipasavyo, ili...

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jumbe inaonekana watu wameupenda sana uchangiaji wako. Kuna Taarifa kutika kwa Mheshimiwa Soud.

T A A R I F A

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu kumpa Taarifa mchangiaji kwamba, wakati tukiongelea kuhusu *networking* ya bandari, basi pia tuiweke pia Bandari ya Zanzibar umuhimu wake kwa sababu nayo pia ni sehemu ya nchi ya Tanzania. Na huduma itakapotoa itatoa kwa ajili ya nchi nzima. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sawa. Mchangiaji anaweza akaweka huo mchango, lakini tusije tukachanganya mambo, tukaanza mambo ya muungano hapa halafu tukawa tumezalisha jambo lingine zito.

Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe.

10 NOVEMBA, 2022

MHE. ALLY J. MLAGHILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bandari ninaomba likae hivyo, lakini naomba nijielekeze pia kwenye barabara na mchango ambao tunachukua kwenye mafuta wa *road toll*. Tunakoelekea sasahivi ni kwamba tunaenda kwenye magari nyanayotumia gesi; na hapa yupo Dangote anatumia gesi. Tunakoelekea itatokea wakati huo mfuko ambayo tunatoa kwenye mafuta tutashindwa kuufikisha na utashindwa kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wataalamu watusaidie, nchi zote sasa hivi zimeacha ku-charge kwenye mafuta, tutumie teknolojia, tuangalie ni namna ambavyo tunaweza tukapata hiyo kodi kwenye magari baada ya kwenye mafuta. Kwa mfano, kuna *Road Toll*; tunao uwezo wa kutumia teknolojia, Wajerumani wame-advance sana, wana kitu kinaitwa *MOT*, gari linahesabika kwa jinsi linavyotembea barabarani ndivyo linavyolipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mkulima ambaye analima kwa trekta, anatembea shambani, *diesel* anayonunua analipa *Road Toll*, mchenjuaji ambaye yuko kule porini anatumia *diesel* kuendesha mtambo wake, analipa *Road Toll* kwa kununua mafuta. Hii siyo haki. Hebu tutafute njia sahihi ambayo itahakikisha kila mmoja analipa kwa haki. Gari lililobeba mafuta, limelipa *Road Toll*, halafu mtu anayeenda kutumia shambani, analipa *Road Toll*. Hata kuendeleza kilimo inakuwa ni shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba, hebu tukae na wataalam wanaotakiwa, ambao wanaweza wakafanya haya mambo vizuri, watuhakikishie na watuongoze. Sasa hivi zipo *taxi* pale mjini, zote zimehamia kwenye gesi, hazilipi. Hakuna anayelipa tena mafuta.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba hebu tunapozungumza mipango hii twende kwenye *irrigation*. Tuna *irrigation* ambazo ni muhimu sana; kuna *irrigation* ambayo iko sehemu ya pale Malawi na Tanzania ambayo inasisitizwa lakini leo sioni Mpango ukiongelea hiyo, ambayo ni *Songwe River Basin*.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Haya, ahsante sana.

MHE. ALLY J. MLAGHILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, na Mheshimiwa Condester Michael Sichelwe ajiandae.

MHE. SALIM A. HASHAM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye mpango huu wa bajeti. Pia namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kufika hapa siku ya leo. Pia nisiwe mchoyo wa fadhila, bila kumshukuru Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kuhakikisha anaiendesha nchi hii katika usawa na utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo kama matatu ya kuchangia kwenye Bajeti. La kwanza nitagusa kwenye mambo ya barabara. Kwanza niwapongeze Wizara zote kwa kazi nzuri wanazozifanya. Pia nawapongeza Wizara

10 NOVEMBA, 2022

ya Ujenzi inavyopambana, tumeona miradi mingi ambayo inatekelezwa, miradi ambayo imekamilika, lakini hatuwezi kurudi nyuma maana miundombinu ya barabara ndiyo chachu ya maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana niliuliza swali hapa Bungeni kuhusu barabara zetu hasa kwenye Jimbo langu la Ulanga. Majibu ya Mheshimiwa Waziri yalikuwa ni mepesi, lakini sijui ni kwa sababu gani? Kikubwa, ninapozungumzia barabara ya kutoka Kilombero kwenda Ulanga ya kiwango cha lami yenye urefu wa Kilometa 67 ilikuwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015, lakini iliingia kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020. Bajeti zote; mwaka 2020/2021, 2021/2022 na 2022/2023 tumekosekana. Tuna imani labda bajeti ijayo tunaweza tukaingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sababu ya msingi kuomba barabara ile. Jimbo la Ulanga sasa hivi ni kitovu cha madini na pia ndiyo Mkoa wa Madini ambao Mheshimiwa Dotto alikuja kuufungua juzi. Tuna miradi mikubwa sana ambayo inakwenda kufanyika kwenye jimbo lile. Wawekezaji wanaenda kuweka zaidi ya Dola milioni 200. Sasa hivi wako kwenye mchakato wa kulipa fidia kwa wanakijiji ili kuweza kupisha miradi ile. Barabara zetu sasa hivi tunapitisha Noah tu; na gari kubwa inayopita ni Fuso, lakini ikinyesha mvua *network* inakatika kwa maana hiyo barabara haipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshajiuliza hivi hawa wawekezaji tusipowawekea mazingira mazuri, kesho wakianza kukafanya *mobilization*: Je, watawezaje kufanya kazi yao na biashara yao inafanyika masika na kiangazi? Inamaanisha adha kubwa itaenda kuwakuta

10 NOVEMBA, 2022

wananchi wa Jimbo la Ulanga, na pia wawekezaji wale watakuwa kwenye wakati mgumu sana wa kufanya kazi yao. Hiyo ni kampuni moja nimezungumzia, Jimbo la Ulanga tunaenda kufanya makubaliano na kampuni nyingine mbili ambazo zinaenda kuchimba madini ya Kinywe. Madini haya yanaenda kubebwa kwenye magari makubwa. Barabara ile haitaweza kukidhi na kuwasaidia wawekezaji hawa kuweza kufanya kazi zao kwa urahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninapozungumza, nipo hapa na ndugu yangu Mheshimiwa Taletale anakuja, ametoka kunilalamikia suala la barabara. Nikamwambia mimi sio Waziri, Mheshimiwa Taletale, ongea na Mheshimiwa Waziri, mimi mwenyewe nina majanga yangu kibao jimboni kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zetu Mawaziri hawa wanatakiwa watupe kipaumbele sana. Sijui kama kuna mawasiliano katika hizi Wizara. Mheshimiwa Dotto ameshamaliza kazi yake kwenye upande wa madini, kwamba watu wanaenda kufanya kazi zao. Kungekuwa na mawasiliano basi, kwamba jamani, tumeshamalizana na hawa watu wanakuja kuwekeza, waende kwa Waziri wa Ujenzi, jamani, barabara zetu zikoje? Zinaweza kukidhi mahitaji ya wawekezaji? Au hospitali, kwamba watu wanakuja kuajiriwa zaidi ya 1,000, je, hospitali zetu zinakidhi mahitaji ya watu na kuwekeza? Siyo mradi mdogo, watu wanakwenda kuwekeza zaidi ya Dola milioni 200 halafu hamna barabara, hakuna hospitali za maana, tutaenda kuchekesha, na hata hao wawekezaji watatuona hatuko *serious*. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nirudi kwenye Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia. Ndugu yangu Mheshimiwa Francis hapa amesema, nami ilikuwa katika mpango wangu wa kuchangia leo; unamwambiaje mwananchi huyu? Kwanza unamwambia akinunua kifurushi cha siku, kwa wiki atatumia shilingi 10,000; akinunua cha wiki atatumia shilingi 5,000. Maana yake huyu mtu umemhamasisha kwamba anunue kifurushi cha wiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yetu *coverage network* yake ni mbaya, vijiji vingi havina *network* na maeneo mengi hayana *network*. Mkulima amejiunga kifurushi chake cha shilingi 5,000, ameenda zake shambani, baada ya siku nne anakuja mjini anaambiwa kifurushi chake kimeisha. Kifurushi chake kimeenda wapi? Hela yangu nani amekula? Tusijibizane majibu rahisi rahisi, ni lazima watu tujue kwamba hii ni dalili ya wizi watu wanaibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumlazimisha mtu anunue kifurushi cha shilingi 35,000 anatumia wiki mbili, wiki mbili nyingine unamwambia kifurushi chako kimeisha, mimi sioni kama ni sahihi na Waziri yuko hapa anatusikiliza. Tuna jambo la kufanya kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

10 NOVEMBA, 2022

MHE. SALIM A. HASHAM: Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia sekunde thelathini.

MWENYEKITI: Hizo ni za mwenzio. Haya, malizia.

MHE. SALIM A. HASHAM: Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye mawasiliano na teknolojia, tuone sababu za msingi za kufunga kamera kwenye miji yetu mikubwa kwa ajili ya *Security*. Wenzetu Kenya wameshafunga kamera miaka saba iliyopita, sisi *population* inaongezeka, uhalifu unaongezeka, tunawatuma askari wanaenda porini hawajui hata mhalifu yuko wapi? Hili ni jambo la msingi sana, miji yetu mikubwa ikafungwe kamera kwa ajili ya *security*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ajiandae.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii katika dakika hizi za Aziz Ki. Nami moja kwa moja nitafanya lile lengo la kuweka goli katika uchangiaji wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika ugharamiaji wa mpango. Katika hili mara nyingi sana huwa zinatajwa fedha ambazo zitakuwepo katika ugharamiaji wa mpango, na wakati mwingine hutaja

10 NOVEMBA, 2022

vyanzo vya ugharamiaji wa mpango, lakini mara nyingi ule ugharamiaji siyo unaokwenda kutumia fedha zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitaeleza, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake wakati akitaja bajeti ya 2021/2022 alisema kwamba makusanyo yalikuwa ni asilimia 97 ya mapato, lakini fedha za maendeleo, ukitazama taarifa ya Wizara ya Fedha inaonesha kwamba ni zaidi ya asilimia 85. Sasa ukitazama Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2021/2022: Je, ulifikiwa kwa asilimia 85? Huwezi kukuta kwamba ulifikiwa kwa asilimia hizo. Sababu zinazopelekea hivyo ni kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi miradi inapopelekewa fedha ambazo tumepitisha kwenye mpango na bajeti, fedha zile zinakwenda kwanza kulipa madeni, *claims, interest* na *variations* za miradi. Ukitaka kujua hayo, tutazame *percentage* ya miradi ambayo labda tunaisema kwenye mpango: Je, kweli tunapokuja kwenye utekelezaji na tunapotoa tathmini inakuwa imefikiwa vile? Inakuwa haikufikiwa hivyo. Sababu ya kutofikiwa ni hizi, kwamba hizi fedha zinaenda kulipwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano mmoja. Tulijadili sana hapa kuhusiana na barabara katika bajeti ya 2021/2022, tukaja kugundua kwamba fedha nyingi zilizotengwa kwa ajili ya barabara zilikwenda kulipia madeni kuliko kutengeneza zile barabara zilizotajwa. Kwa kuwa yanatokea hayo, japo kuna msemu kwamba “mpango siyo matumizi,” lakini kwa kuwa Mpango huu tunapanga hapa kwenye Bunge hili, nitoe rai moja. Kwanza, Waziri anapoleta gharama za mpango,

10 NOVEMBA, 2022

anapotaja ile *source* ya fedha labda kwa mradi fulani fedha hii, basi kile kianzio kiwe *ringfenced*, na kikiwa *ringfenced* ina maana hakitaweza kuingiliwa kama zilivyo fedha za REA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, Waziri atakapokuwa anawasilisha labda mradi wa maendeleo, mfano *Standard Gauge Railway route* ya kutoka Dar es Salaam – Morogoro, anataka kufanya *percent* ngapi? Ataje *baseline* na malengo yake ili tukija kutathmini mpango, tukute kwamba fedha zilizotengwa kugharamia huu mpango ziwe zimekwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika dhima ya mpango tutasema ni kujenga uchumi shindani. Mimi nasema ushindani katika usafirishaji. Tuna bandari na tunajenga *Standard Gauge Railway*. Bandari tunajenga, lakini kuna nchi tunazoshindana nazo; kuna Angola, *South Africa*, Msumbiji na Kenya. Sisi tuna faida ya kijiografia (*geographically advantage*), kwamba tunaweza tukapeleka kokote, lakini wenzetu wanatumia mbinu nyingine mbadala katika *financing* ya mradi wa *Standard Gauge Railway*. Wenzetu wana-*finance* mradi wote. Tukitazama nchi nyingine Jirani, wamejenga *Standard Gauge Railway*, baada ya kuona haitoshi, wanatengeneza mikataba na zile nchi ambazo ni masoko. Wanatengeneza mikataba na Kongo, Zambia, ili kuondoa ile *geographical advantage* ambayo tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasi kama tunataka kujenga uchumi shindani, ni lazima na haya tuyaangalie. Mpango huu utoe jawabu kwamba tunataka kufanya ushindani katika usafirishaji na hawa wenzetu. Kwa mfano, kuna nchi moja ina bandari lakini

10 NOVEMBA, 2022

imeenda kuweka bandari kavu katika nchi nyingine, ambapo nasi katika nchi ile ni soko letu, watu wataenda kuchukulia bidhaa pale. Kwa hiyo, tunataka mpango huu katika usafirishaji hasa kupitia bandari na reli itoe jawabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nije kwenye umeme wa REA. Kuna takwimu ambazo bado sijazielewa. Tulisema tunafanya vijiji 12,000. Tukatoa ripoti 2021/2022 kwamba vijiji 10,000 tayari vimeshafanyiwa. Ila kwenye mpango vimeelezwa vijiji 8,000 ndivyo vilivyofanyiwa, siyo 10,000 tena. Maelezo ya Waziri yanasema vijiji 9,000. Je, tushike kauli ipi hapa? Kwa maana hiyo kama vilifanyika vijiji 10,000, leo tumerudi vijiji 8,000, ina maana bado vijiji 4,000, na Waziri amesema vijiji 9,000. Ina maana bado vijiji 3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonesha kitu gani? Kitu kinachooneshwa katika tofauti ndani ya Serikali, ina maana kwamba inawezekana vijiji vile tayari vimeshafanyiwa kazi, lakini pengine kwa sisi tunaofikiria kwamba ile gharama yake watu wanataka kuja kuirudisha ipate kutumika visivyo; au kule mwanzo tulipotajiwa vijiji 10,000, ina maana zile fedha hazikutumika kweli kwenye vijiji 10,000 na fedha zile labda badala yake zilifanyiwa vitu ambavyo siyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itupe takwimu sahihi katika miradi ya REA. Kuna takwimu tatu tofauti; kuna 10,000, 9,000 na 8,000, ni ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naunga mkono hoja. (Makofi)

10 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Condester Sichalwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ajiandae.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii adhimu ili nami niweze kuchangia. Kwanza kabisa, nitakuwa sijaitendea haki nafsi yangu kama sitampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Nchi hii Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan. Tuseme ukweli, mama wa watu; mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni, anajitahidi. Ombi langu tu kwa wale ambao amewaamini, wasiendeleo kumwangusha, wamsaidie ili aweze kutimiza kusudi lake la kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia mambo mawili tu, kwa kuwa muda siyo rafiki. Jambo la kwanza kabisa, nataka kuwaongelea wananchi wa nchi hii, wale ambao ni wa kawaida, wanyonge, masikini, wakulima na wote ambao wanafanya shughuli zao ndogo ndogo, wanazalisha mambo ambayo yako ndani ya nchi yetu, ni pamoja pia na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa nchi hii wanajitahidi sana na wanajituma sana katika kuzalisha mazao yao ambayo Mwenyezi Mungu amewasaidia wazalisha, na wengine wanatumia mpaka jembe la mkono katika kuzalisha, lakini ambacho nakiona, tunapaswa tuwekeze nguvu kubwa sana kwenye masoko. Kwenye uchumi wanasema, *demand* inapokuwa *high*, *supply* ikawa *low* au *constant* inapelelea *price* kuwa *high*. Tafsiri yake ni nini? Kama

10 NOVEMBA, 2022

supply itakuwa *constant* au itakuwa *low*, *demand* ikawa *high*, maana yake wananchi hawa chochote watakachokuwa wanakizalisha kwa sababu wanazalisha katika *supply* hiyo hiyo, lakini *demand* inapokuwa kubwa kwenye masoko, itakuwa inaleta motisha ya wao kuendelea kuzalisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mapendekezo ya mpango, nimesoma ukurasa wa 125 ambao unasema kuhusu huduma za biashara na masoko. Waziri wa Fedha na Mipango anasema, kuimarisha miundo mbinu ya masoko, lakini kipengele cha pili anasema, kuimarisha mfumo wa kilimo cha mikataba na upatikanaji wa mikopo ya kilimo yenye riba nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi kipo kipengele ambacho kinazisisitiza balozi zetu kuhakikisha zinatutafutia masoko huko nje. Je, balozi zetu zimesimamaje kuhakikisha zinawatafutia wakulima wa nchi hii masoko ya kutosha ili hata kama *supply* yetu itakuwa *limited*, *demand* iwe *high* ili wananchi hawa waendeleo kupata kwa kiwango kikubwa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia zipo baadhi ya balozi ambazo tukiwasiliananazo, wanasema changamoto kubwa ambayo wanaipata ni wakulima wetu kushindwa ku-*supply* kuanzia mwezi wa Kwanza mpaka wa Kumi na Mbili (*continuously*). Wanashindwa kwa sababu gani? Wanazalisha kwa kiwango cha chini. Kama wanazalisha kwa kiwango cha chini, tafsiri yake ni nini? Hawajawezeshwa. Hapa tunaposema kwenye mikopo yenye riba nafuu, ndipo tunaposema Benki ya Kilimo ihusike na pia Wizara ambazo zimepewa dhamana kwa ajili ya kuziomba benki ambazo zinaweza zikatoa mikopo

10 NOVEMBA, 2022

ya riba nafuu iweze kuwasaidia wakulima wa nchi hii pamoja na wafugaji ambao pia watataka kuwezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka kusoma kidogo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwenye ukurasa wa 15(xv) kinachoongelea miradi ya maji. Mheshimiwa Waziri anasema hivi, “hadi kufikia Juni, 2022 miradi ya maji kwa vijijini ilifikia asilimia 74.5 ukilinganisha na mwaka wa nyuma Juni, 2021 ilikuwa ni asilimia 72.3; na mijini asilimia 86.5 mwaka wa nyuma asilimia 86.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyosoma hapa kwa kweli asilimia 74 ya miradi ya maji ambayo anasema hivi: “kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji ambapo hadi kufikia Juni, 2022 imefikia wastani wa asilimia 74 kutoka mwaka wa nyuma asilimia 72.3.” Tafsiri yake nini? Maana yake ukitembea katika vijiji 100, vijiji 70 vina huduma ya maji. Nilipoona hii ripoti nikajiuliza, kwa hiyo, ni sisi Momba tu ndio tumesahaulika ama! Nikaanza kuuliza baadhi ya Wabunge wenzangu ambao na wenyewe wanatoka kwenye majimbo ya vijijini kama jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeuliza Wabunge zaidi ya 20 hapa, hakuna Mbunge hata mmoja ambaye ameniambia yeye kwenye jimbo lake amefikisha hata asilimia 50 ya upatikanaji wa maji. Swali langu, sisi tunajenga nyumba moja, tuko hapa kuwatumikia Watanzania, hata Mama Samia sera yake anasema anataka kumtua mwanamke ndoo kichwani, nia yake ni ya dhati na nzuri zaidi kwa ajili ya kutaka kuwasaidia akina mama wa nchi hii pamoja watu wote. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhalisia huu siyo wa kweli. Nitolee tu mfano wa jimbo langu, mimi nina vijiji 72. Katika vijiji 72, yaani leo nimeona niwasiliane na Madiwani wote waseme; katika vijiji 72 ziko baadhi ya Kata hazina mradi wa maji kabisa. Sasa nikajiuliza, hiyo asilimia 74 inatoka wapi? Wako pia Wabunge wengine hizo asilimia hazijafika? Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwenye ukurasa wa saba...

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Muda mdogo jamani, eeh!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa saba miongoni mwa vitu ambavyo ni vipaumbele... *(Kicheko)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Okay sawa. *(Kicheko)*

Kengele imeshalia, muda umeisha, lakini Mheshimiwa Mbunge wa Kibamba.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ni mchango mzuri sana wa Mheshimiwa Mbunge, nataka kumpa tu taarifa hayo anayoyasema ni ya kweli kabisa kwamba takwimu hizo zinashangaza na mimi kama Mbunge ninayetokea Dar es salaam upande wa Jimbo la Kibamba, maji ni changamoto, katika kata nyingi hakuna, kwa hiyo ni mchango mzuri na ni kweli kabisa anachokisema. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Nye wa Dar es Salaam huwa mkisimama na mkaungana na wa vijijini kuna muda hatuwaelewi sana. Hivi na nye wa Dar es Salaam mna changamoto kweli kama za Momba? *(Makofi)*

Mheshimiwa malizia sekunde 30.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika vijiji 72 ni vijiji 16 tu ambavyo vina maji na vijiji 56 havina maji. Sasa najiuliza hii takwimu inatoka wapi? Sisi tunajenga nyumba moja, tuwatendee Watanzania haki. Tulienda kuomba kura kwa kutumia ilani hii na kwenye ilani hii ukurasa wa saba, samahani kidogo tu nisome mama yangu. Katika miongoni mwa vitu ambavyo ni vipaumbele ambavyo sisi tulipewa ilani tukanadi kama Wabunge wa Chama cha Mapinduzi inasema hivi; “Kuongeza kasi ya usambazaji wa maji safi na salama ili kutosheleza mahitaji kwa zaidi ya 85% vijijini na zaidi ya 95% mijini.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naamini kwa sababu wanaona tumeshafika mwaka wa pili na ilani inasema 85%, wameamua waseme 74% hii ili ionekane wameteteleza, hapana sio kweli. Kupitia Bunge hili, namwomba Mheshimiwa Aweso, nataka nikafanye naye ziara kwenye jimbo langu, vijiji 10 ili kweli na vyombo vya habari vimchukue nione kama kweli atakuja na hiyo takwimu ya 76%, kwamba kweli kuna maji. Hapana sio kweli. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango ulikuwa umesimama.

10 NOVEMBA, 2022

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kwanza kuweka sawa suala hili. Miradi ya maji ni tofauti sana na shule ambayo unaenda unaweka *specific*, kwamba unapoweka shule ukisema iko kwenye kijiji inakuwa kwenye kijiji. Miradi ya maji ni mtandao, kwa hiyo tunapotaja kwa asilimia na wala hatutaji kwamba tumemaliza vijiji vingapi, bali tunataja *access*, ambacho tumefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye wilaya moja ukiwa na vijiji 10 tu kati ya 70 wananchi hao wataishije kama hawana maji hata kidogo? Kwa hiyo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, umezungumzia mwenyewe hapo mtandao. Ulikuwa unamaanisha nini mtandao? Kwa sababu haimanishi hawana maji kabisa, wasingeweza kuishi. Hata hivyo sio maji ya mtandao yaani ni kwamba wanafuata mtoni au wanafuata mahali, ndio hoja, kwa sababu wewe unasema unamaanisha mtandao kwamba yeye vijiji unavyovitaja mtandao utakuwa kwake sasa zaidi ya 70%? Ndio hoja yake.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Ndio ninachokisema hapa kwamba, ukifungua *pandora* ya takwimu ita-*dilute* hoja ya msingi ya kibunge ambayo anatakiwa ataje vijiji vyake ambavyo havina maji. Pia ukisema takwimu za Serikali inazotoa kwamba zina mashaka, yaani takwimu hizi kubwa za aina hii za vijijini na mijini kwamba zisiwe sawa ni kitu kingine ambacho...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, wewe ambacho ungemsaidia Mbunge na Wabunge wengine waliokuwa wanashangilia hapa, ni namna ambavyo hizo takwimu

10 NOVEMBA, 2022

zinazalishwa. Ingewasaidia Wabunge lakini pia na Mbunge, kwa maana ya kwamba unaposema zile asilimia 74, yako maeneo ambayo umefikia zile asilimia 74, lakini pengine yeye na jimbo lake ndio wako kwenye ile asilimia 26 ambayo hawamo kabisa.

Kwa hiyo ungetueleza namna ambavyo takwimu unavyozipata zile ingemsaidia Mbunge kuelewa kwamba, hata yeye ule mpango wa kufika asilimia 85 kwa speed anayokwenda Mheshimiwa Rais, hata yeye atafikiwa, lakini kwa takwimu ziko sahihi ila yeye kwake hajafikiwa kwa sababu hatujasema asilimia 100, tumesema asilimia 74. Hapo ungekuwa umemaliza mzizi wa fitina kwamba Mheshimiwa kwako hatujafika, lakini sasa kwa namna takwimu zilivyokaa na anavyoeleza hata yeye kwa mlengo wake yuko sahihi, kwa maana ya kwamba ukisema asilimia 30 una maanisha katika watu 10 watu watatu, si ndio. Ukisema 70 kati ya watu ngapi? Ndiyo na yeye anachoeleza, yeye ameamua kwenda huko, basi wewe ungempeleka kwenye takwimu zako.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Hizo hizo.

MWENYEKITI: Hizo hizo za jumla, wewe ungeeleza sasa upande wako umezipataje kwa sababu ndilo swali lake. Umeelewa sljui swali lake Mheshimiwa Waziri au nirudie? Ni hivi yeye ungemweleza takwimu hizi Mheshimiwa Mbunge huwa tunazitengeneza hivi na hivi kwa hiyo ziko sahihi, hata kama kwako hatujafikia asilimia 74, tumefika asilimia 74 kama Taifa.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama hapa kwa sababu ndiye ninayehusika na utoaji wa fedha. Ukipotosha Taifa kuhusu

10 NOVEMBA, 2022

takwimu na mafanikio makubwa kwenye sekta ya maji kwa sababu unaongelea jimbo moja ni makosa. Kama umetajiwa takwimu za Mbeya Mjini unaruhusiwa kuzipinga kwa kutumia Jimbo la Mbeya Mjini, ndio utaratibu wa kiuchumi. Huwezi ukatumia takwimu za wilaya moja ku-*challenge* takwimu za nchi nzima, hujafika kwenye eneo lingine...

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Namna tunavyozipata, tunapata kwa kuangalia kila miradi inayotekelezwa na *targeted population*, ndipo tunapopata asilimia na hivyo ndivyo zinavyopatikana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri hoja iko pale pale, nadhani hatujaelewana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kidogo, yaani ni hivi, kwa mfano, ukisema hivi, takwimu za Mkoa wa Mbeya watu wenye *HIV* si huwa kuna zile takwimu? Sijui asilimia tisa ya wale watu walioko kule na Taifa tunazo takwimu kwamba Taifa letu asilimia ni ngapi? Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wake kwa sababu alikuwa anazungumzia Momba, kwake na akataja za kwake yeye. Akizichukua hizi za Taifa akazipeleka kwake anasema sio kweli. Ambacho na wewe unasema yuko sahihi, isipokuwa ambacho wewe unakibisha ambacho na wewe uko sahihi kwamba kitaifa tumeshafikia asilimia zaidi ya 74, lakini kwako Momba hatujafika kwa sababu uko kwenye zile asilimia 26 ambazo bado hatujafika.

10 NOVEMBA, 2022

Jamani mimi ni Mwanasheria sio mwana mahesabu, kwa hiyo nawasikiliza wote na najaribu kuweka maelezo kwenye takwimu zao wote wawili. Kwa hiyo wote wawili wako sahihi. Jimbo la Momba maji hayajafika kwa asilimia 74, ndio hoja ya Mbunge, kitaifa tumefika asilimia 74, Mheshimiwa Waziri hiyo iko sawa si ndio?

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio.

MWENYEKITI: Kitaifa tumefika 74%, lakini Momba hatujafika 74% ndio hoja kwa hiyo yuko sahihi si ndio?

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hayuko sahihi.

MWENYEKITI: Haya takwimu za Momba yuko sahihi ama hayuko sahihi? Washa kisemeo. Za Momba yuko sahihi, hayuko sahihi?

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maslahi ya muda nadhani Mheshimiwa Mbunge akae na Wizara ya kisekta apate takwimu za jimbo lake halafu a-challenge za jimbo lake. Ninachopinga huwezi uka-challenge takwimu za Taifa zima. Hizo takwimu ziko sahihi na hiyo ndiyo *position* ya Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, mpaka hapa wewe ni Mchumi, mimi sio Mchumi, hebu nieleweshe mimi. Tukisema hivi nchi hii watu wanaojua kusoma na kuandika ni 95%, tunamaanisha nini?

10 NOVEMBA, 2022

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda hivyo ndio utaelewa vizuri. Iko namna hii, tukisema nchi hii ina watu wanaojua kusoma 95%, kama kuna kijiji hakina mtu kabisa anayejua kusoma na kuandika, hatuwezi kusema zile takwimu haziko sahihi.

MWENYEKITI: Sasa wewe unachonibishia mimi maelezo kuhusu Momba ni kipi? Kwa sababu Kijiji hicho utakubali...

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachobishia ni ile kusema takwimu hizi haziko sahihi.

MWENYEKITI: Ngoja ngoja, maana yake ni kwamba hata ukisema asilimia 95, maana yake upo uwezekano wa kijiji kizima kikawa kina watu ambao hawajui kusoma. Kwa hiyo hata wewe ukisema takwimu za maji ni asilimia 74 vijijini, maana yake liko jimbo nchi hii linaweza kuwa halina maji. Sasa Mbunge amekosea nini kwenye hoja hiyo? *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, unachoongea na ninachoongea ni sawasawa.

MWENYEKITI: Sasa unanishangaza unapoendelea kubisha kama tunachoongea ni kimoja, basi umenilewa. Tuendeleo basi.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kimoja ila tunatofautiana tu kuhusu takwimu za kitaifa.

10 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Hapana. Hata takwimu za kitaifa hazijatofautiana kwa sababu ndio uhalisia, yeye anatoka Momba ameeleza za Momba, wewe umeeleza za Taifa na yeye amesema hizo ulizoeleza za Taifa kwake hazijafika, si ndiyo uhalisia? Hebu wataalam wa hesabu mimi ni Mwanasheria jamani. *(Makofi)*

MHE. JOSEPH K. MSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwasaidie. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Wataalam wa hesabu.

MHE. JOSEPH K. MSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Naona wataalam wa hesabu wanataka kunisaidia na wako wengi. Nitawapa nafasi wawili. Mheshimiwa Kasheku Msukuma. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. JOSEPH K. MSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naona taaluma kidogo zimegongana inabidi Daktari nisaidie kuokoa jahazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni jepesi, tunamwomba Mheshimiwa Waziri asi-panic. Kwa mujibu wa maelezo ya Mbunge wa Momba, yeye analalamikia jimbo lake na ulichouliza kwamba katika 74% na 26 % zilizobaki, jibu ni jepesi kwamba ili afike kwenye 100 bado yuko kwenye 26 wala hauumizi akili. Hata hivyo, kupata takwimu za nchi nzima sio kwamba wote tuko 74%. Kwa mfano mimi jimbo langu liko 25%, ukijumlisha unapata zote. Sasa mnachogombana ni nini?

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na hii ndiyo busara ya daktari wa akili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole – Shangai.

MHE. EMMANUEL L. SHANGAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi mlichokuwa mnazungumza ni kitu rahisi tu, kwamba Mheshimiwa wa Momba yeye anasema kwamba kuna vijiji vyake havina maji, na Mheshimiwa Waziri yeye alitakiwa kutujibu rahisi tu kwamba Tanzania tuna vijiji 12,354, *percentage* ya vijiji ambavyo vina maji labda ni 9,000, ambazo ni 74% lakini vijiji ambavyo havina maji labda ni vijiji 4,000 au 5,000 na Jimbo la Momba kuna vijiji 10 havina maji na ambavyo viko kwenye hiyo asilimia. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Jamani hata sisi Wanasheria hesabu tuko vizuri kidogo. *(Makofi)*

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi; ninayo heshima kubwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka wa fedha 2023/2024, pamoja na Mapendekezo ya mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapitia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa tukiwa na takwimu sahihi ya idadi ya watu na majengo kutokana na Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika tarehe 23 Agosti, 2022 ambapo idadi ya watu imefikia 61,741,120. Takwimu hizi

10 NOVEMBA, 2022

zinatuwezesha kuandaa mpango jumuishi na unaotekelezeka. Maendeleo ni takwimu, hongera sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia vyema zoezi la sensa mpaka takwimu zimepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze kwa dhati Kamisaa wa Sensa Tanzania Bara Mheshimiwa Mama Anne Semamba Makinda na Kamisaa wa Sensa Tanzania Zanzibar, Mheshimiwa Balozi Mohamed Haji Hamza. Hongera timu ya watakwimu wote walioshiriki, Makarani wa Sensa, Wenyeviti wa Vitongoji na wananchi wote kwa moyo wa kizalendo walioonesha katika kukamilisha zoezi hili muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa utekelezaji na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2023/2024. Deni la Serikali; takwimu zinaonesha kwamba deni la Serikali limeongezeka kutoka shilingi trilioni 60.72 kipindi cha Aprili, 2021 hadi shilingi trilioni 69.44 Aprili, 2022 hili ni ongezeko la shilingi trilioni 8.72 katika kipindi hicho ambalo ni ongezeko la 14.4%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwendendo wa ukuaji wa deni la Serikali; deni la Serikali lilikuwa kwa asilimia saba (2019/2020), asilimia 13.7 (2020/2021), asilimia 11 (2021/2022) lakini pia takwimu zinaonesha kuwa Serikali ilipokea mikopo mipya kipindi cha miezi miwili, Mei na Juni, 2021 kiasi cha shilingi trilioni 3.799.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu hizi zinazua maswali mengi yasiyo na majibu kama ifuatavyo:-

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kujiuliza kwa nini deni la Serikali liongezeke kwa shilingi trilioni 8.72 wakati katika mwaka husika wa fedha wa kuishia Aprili, 2022 deni lililipwa kwa zaidi ya shilingi trilioni 7.2 na wakati huo huo shilingi ya Tanzania iliimarika kwa wastani wa 0.03%. (sababu ya riba haiwezi kupandisha deni kwa kiwango hicho).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tafsiri yake Serikali ilichukua mikopo mipya yenye thamani ya shilingi trilioni 15.92 kinyume na kiwango kilichoruhusiwa na kupitishwa na Bunge cha wastani wa shilingi trilioni 10.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la Serikali lilikuwa linakua kwa wastani wa asilimia nne lakini ghafla miaka ya 2020/2021 na 2021/2022 deni la Serikali limekua kwa wastani wa asilimia 12.33. Wakati deni la Serikali likiongezeka kwa kasi hiyo ukusanyaji wetu wa mapato ya ndani sio wa kuridhisha ambapo Tanzania inakusanya asilimia 11.40 ya pato la Taifa ikiachwa nyuma na nchi jirani za Kenya asilimia 13.70 na Rwanda asilimia 15.90 ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Taarifa ya Kamati ya Bajeti ukurasa wa tano na sita kipengele cha 2.5 imeshtushwa na kasi ya ukopaji unaoendelea, nanukuu; "Aidha imekuwa ni rai ya Kamati ya muda mrefu kuweka na kutumia kiashiria cha ukumo wa ulipaji wa deni la Serikali kwa mapato ya ndani (*Debt Service to Domestic Revenue Ratio*) ili kuhakikisha kwamba mapato ya ndani yana uwezo wa kugharamia shughuli zote za Serikali pamoja na deni la Serikali." Mwisho wa kunukuu.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa kasi wa deni la Serikali wa namna hii ambao pia hauzingatii uwezo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani usipodhibitiwa kuna hatari nchi yetu kuingia kwenye mgogoro mkubwa wa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo na Serikali kukopa, lakini ni lazima mikopo inayochukuliwa na Serikali izingatie uwezo wa nchi kulipa madeni hayo na ukomo wa kukopa uliopitishwa na Bunge katika bajeti ya mwaka husika, na hii ni kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Katiba na Sheria za nchi (Sheria ya Fedha, Sheria ya Bajeti na Sheria ya Mikopo) zinaeleza bayana utaratibu wa namna ya kukopa na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, kwa nini Serikali ikope zaidi ya kiwango kilichoruhusiwa na Bunge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama miradi yote iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022 ilitengewa fedha na kuidhinishwa na Bunge, je, mikopo ya ziada iliyokopwa na Serikali imetekeleza miradi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba ufafanuzi katika kipindi cha kujadili na kupitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023, bahati mbaya sana Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba hakutoa maelezo yoyote juu ya hoja hii. Ninaomba kushauri tena kama ifuatavyo; kwanza, Waziri wa Fedha na Mipango atoe maelezo ya kina kuhusu ziada ya mikopo ya Serikali katika mwaka wa

10 NOVEMBA, 2022

fedha 2020/2021 na 2021/2022 ili Bunge liweze kuchukua nafasi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, CAG afanye ukaguzi maalum wa deni la Serikali katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022 ili kuweka uwazi na kuondoa mkanganyiko kwa Watanzania kuhusu hali ya deni la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu mikopo iliyochukuliwa na Serikali izingatie uwezo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani badala ya kung'ang'ana na vigezo vya kimataifa ambavyo vinaweka rehani mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo; hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango ukurasa wa 28 kipengele cha 35 amesainisha kuwa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo unatarajiwa kutekelezwa kwa kushirikisha sekta binafsi, lakini pia hotuba ya Kamati ya Bunge ya Bajeti ukurasa wa 13 kipengele 3.1.4.1 (c) naomba kunukuu; "Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kutafuta njia nzuri ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo ambayo itazingatia manufaa mapana ya Taifa kwa vizazi vya sasa na vizazi vijavyo ili kutekeleza mradi huo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushauri huo wa Kamati ya Bajeti yapo maswali mengi ya kujiuliza kabla ya kuanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; kama Taifa tumeshafanya tathmini ya kina na kujiridhisha kuwa mradi wa Bandari ya Bagamoyo unaweza kutekelezwa kwa njia

10 NOVEMBA, 2022

ya ubia na bila kuathiri uchumi wa ustawi wa nchi yetu, tutawezaje kulinda mifumo ya kiusalama ya nchi, mwekezaji binafsi anaweza kuamua kupandisha gharama za usafirishaji na uchukuzi wa mizigo bandarini wakati wowote tutawezaje kudhibiti mfumuko wa bei, tutawezaje kuwalinda wafanyabiasha na wawekezaji wetu wa ndani, tutawezaje kudhibiti mifumo ya ukusanyaji wa mapato nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili; Taifa hivi sasa tuna miradi mikubwa ya kimkakati ambayo iko kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji na yenye mahitaji makubwa ya fedha, miradi hiyo ni pamoja na Reli ya SGR, Bwawa la Mwalimu Nyerere, Bwawa la Kidunda, ujenzi na ufufuaji wa meli, uboreshaji wa bandari zilizopo, ujenzi wa Daraja la Kigongo Busisi, ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato, ununuzi wa ndege mpya na kadhalika. Je, kama Taifa tunao uwezo wa kiuchumi na kimapato kwa sasa kuweza kubeba gharama za mradi mpya wa Bandari ya Bagamoyo wakati tuna miradi mikubwa ya kimkakati inayoendelea maeneo mbalimbali nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; tumejiandaaje kulinda haki za Watanzania katika mkataba huo kwani uzoefu unaonesha mikataba mingi ya ubia tuliyoingia kama Taifa ni ya upigaji na mifano dhahiri ipo na wote tunakumbuka kama *Symbion*, *Richmond*, *IPTL*, *TRL*, *City Water*, *Aggreko* na kadhalika, mikataba ambayo imelitia hasara kubwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne; Kamati ya Bajeti imeonesha mashaka yake kwa chanzo cha fedha kilichopendekezwa na Serikali cha ubia na ndio maana ikashauri itafutwe njia nzuri ya upatikanaji wa fedha kwa

10 NOVEMBA, 2022

ajili ya ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo ambayo itazingatia manufaa mapana ya Taifa kwa vizazi vya sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu mimi Mradi wa Bandari ya Bagamoyo ni mradi mzuri na una manufaa makubwa kwa Taifa letu, lakini tujipe muda kukamilisha miradi ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa maeneo mbalimbali nchini na pia kujipa nafasi ya kutafuta fedha za kugharamia mradi huo bila kuathiri uchumi na ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kufua umeme wa Bwawa la Julius Nyerere (*JNHPP – MW 2,115*); kuhusu utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa Bwawa la Julius Nyerere (*JNHPP – MW 2,115*) kama ilivyotolewa taarifa kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2023/2024 kipengele (b) ukurasa wa 19 na Taarifa ya Kamati ya Bajeti kipengele 3.1.3.1 ukurasa wa 9 na 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikushauri hapa Bungeni kuunda Kamati Teule ya Bunge na nikasema utanishukuru. Leo hii unashuhudia mkanganyiko mkubwa uliobainishwa na Kamati yako ya Bajeti ambayo imeshindwa kupata taarifa za uhakika juu ya kinachoendelea katika utekelezaji wa bwawa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, mkataba baina ya TANESCO na Kampuni ya *Arab Contractors* ya Misri umeongezwa na Serikali bila sababu za msingi, bila kufanya tathmini na bila kubainisha gharama za ongezeko la muda wa mkataba (*variations cost*) zitabebwa na nani?

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, muda ulioongezwa katika mkataba baina ya TANESCO na Mkandarasi Arab Contractors haujulikani hadi sasa kwamba ni miezi 12 au miezi 24, TANESCO inaonesha kwamba mkandarasi ameongezewa muda wa miezi 12 yaani hadi tarehe 15 Juni, 2023 lakini mkandarasi na Wizara ya Nishati wanasema muda ulioongezwa ni miezi 24 hadi Julai, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, huku tunaelezwa mradi umefikia 75% ya utekelezaji, lakini mkandarasi ameongezewa muda mrefu wa miaka miwili kumaliza mradi ulibakiza 25% tu ya utekelezaji hali inayoleta mashaka makubwa juu ya ukweli wa hatua za utekelezaji zinazowasilishwa na Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, mara tunaletewa maelezo hapa Bungeni kuwa TANESCO na mkandarasi wanavutana bila Bunge kuelezwa wanabishania nini. Ni hatari sana kuingia kwenye mabishano huku mradi ukiwa umefikia 75% ya utekelezaji na malipo yakiwa yamefanyika zaidi ya 70%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, sababu hazitolewi za kwa nini malipo halali ya kimkataba ya CSR kiasi cha shilingi bilioni 260 haijatolewa licha ya Serikali kuendelea kufanya malipo kwa mkandarasi yaliyofikia zaidi ya 70% ya madai yote ya mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, Kampuni ya Arab Contractors inapaswa kulipa gharama za ucheleweshaji wa mradi (*variations cost*) kwa muda wa miaka miwili kiasi

10 NOVEMBA, 2022

cha shilingi trilioni 1.3 kwa mujibu wa mkataba ambayo ni 10% ya gharama za mradi kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si Wizara ya Nishati wala TANESCO iliyodai fedha hizo kwa mkandarasi ambaye hivi sasa ameshalipwa madai yake kwa zaidi ya 70%. Kwa nini Serikali iendelee kumlipa mkandarasi bila kukata fedha za CSR na faini ya ucheleweshaji? Madai haya ni haki ya Watanzania kwa mujibu wa mkataba na sio hisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchelewa kwa mradi huu wa Bwawa la Julius Nyerere kumeliingiza Taifa kwenye hasara kubwa ikiwemo kuwepo migao na katakata ya umeme isiyoisha, migao ya maji, Mradi wa SGR kutokufanya kazi baada ya kukamilika, kukosa wawekezaji kutokana na nchi kutojitosheleza kwa umeme, hasara na ajira kuyeyuka kwa shughuli za uzalishaji zinazotegemea umeme, nchi kushindwa kuuza umeme nje ya nchi na Taifa kukosa mapato na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Wizara ya Nishati kuendelea kuwasilisha taarifa zenye mkanganyiko Bungeni kuhusu utekelezaji wa mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, kuongeza muda wa mkataba kiholela na kushindwa kudai madai halali ya kimkataba ya shilingi trilioni 1.56 yanaleta mashaka makubwa na kuashiria kuwepo kwa mianya ya rushwa, uwezo mdogo wa Wizara ya Nishati kusimamia utekelezaji wa mkataba na ni dharau kubwa kwa Bunge lako tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka mwanzo nilishauri kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge ili kuchunguza ukweli wa jambo hili na leo ninashauri mambo mawili yafanyike ili kuunusuru Mradi wa Bwawa la Julius Nyerere na kuepuka hasara inayoweza kutokea mbeleni ya kupoteza matrilioni ya fedha za Watanzania na mradi kuishia njiani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, iundwe Kamati Teule ya Bunge kubaini ukweli na chanzo cha mkanganyiko wa taarifa zinazotolewa na Wizara ya Nishati na kupendekeza hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Bunge liagize Wizara ya Nishati na TANESCO kukata fedha zote za CSR na gharama za ucheleweshaji wa mradi kwa Kampuni ya *Arab Contractors* kiasi cha shilingi trilioni 1.56 katika malipo yatakayoendelea kutolewa kuanzia sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maeneo ya kupewa kipaumbele; Serikali imeweka vipaumbele vingi ambavyo ni ngumu kuvitekeleza kwa ufanisi na ikumbukwe kuwa kupanga ni kuchagua. Ni vyema utekelezaji wa miradi mbalimbali ukafanyika kwa awamu kulingana na uwezo wa rasilimali zilizopo. Nimepitia maeneo mbalimbali ya mapendekezo ya mpango na naomba kushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza Serikali kwa hatua ya kupata mkandarasi na kusaini mkataba wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda hali itakayopelekea kumaliza tatizo la maji la muda mrefu linaloikabili Mikoa ya Morogoro, Pwani na Dar es Salaam.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu, Serikali itekeleze kwa vitendo mradi ulioahidiwa kwa muda mrefu wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria katika Mkoa wa Simiyu ambao maji yatasambazwa katika Wilaya za Busega, Bariadi, Itilima, Meatu na Maswa. Wananchi wa Jimbo langu la Kisesa wanausubiri mradi huu kwa hamu kubwa ili kutatua matatizo ya maji ya kunywa, kilimo, mifugo na shughuli nyingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwenye mipango ya ujenzi wa skimu za umwagiliaji, msitusahau wakulima wa Jimbo la Kisesa na Mkoa mzima wa Simiyu kwa kuwa tunayo maeneo mengi yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa mazao ya mpunga, pamba, mahindi, mbogamboga na kadhalika na Serikali itenge fedha za kutosha katika kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Serikali itenge fedha za kutosha kuwezesha utafiti kufanyika nchini katika taasisi zake za kama *COSTECH, TARI, TALIRI, TAFIRI, TAWIRI* na kadhalika ili kuwezesha kupata taarifa muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ujenzi wa madaraja ya Mwamhuge katika Mto Sanga (mpakani mwa Meatu na Maswa), ujenzi wa daraja la Sanjo (mpakani mwa Meatu na Itilima), ujenzi wa Daraja la Mwabuzo (linalounganisha Meatu, Kishapu na Igunga) pamoja na maombi haya naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita kupitia *TARURA* na *TANROADS* kwa utekelezaji mzuri wa ujenzi wa barabara na madaraja jimboni kwangu Kisesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, ukamilishaji wa ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu; uUjenzi wa

10 NOVEMBA, 2022

zahanati kila kijiji na ununuzi wa vifaa muhimu vya kitabibu, madaktari na wauguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, Serikali itenge fedha za kutosha kwa uboreshaji wa bandari zote katika Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba tunaishukuru Serikali kwa kuendelea kutafuta masoko ya mazao nje ya nchi hongera sana. Tumeshuhudia mkiwezesha kupata masoko makubwa ya mazao kama korosho, soya, parachichi, pamba, choroko, dengu, mabondo, samaki, nyama na mazao ya mbogamboga, lakini kupata masoko ya nje ni suala moja na kumudu mahitaji ya soko ni kitu kingine. Kama Taifa tunapaswa kuwekeza vya kutosha katika kuhudumia masoko ya kimataifa ili kuhakikisha tunazalisha kwa wingi na kwa viwango vinavyohitajika na masoko husika. Hongera sana Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri unayoifanya ya kuiunganisha Tanzania na dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikishwaji wa Watanzania na upatikanji wa ajira; mpango lazima uzingatie ushirikishwaji wa Watanzania katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shughuli mbalimbali za kiuchumi nchini, lakini yapo mambo yanayoendelea ambayo yanakinzana na hii dhamira njema ya Serikali, mifano; moja, wafugaji wa mifugo ya asili wa kijiji cha Ilunde B, Kibondo Mkoani Kigoma kila leo wanafukuzwa kwenye maeneo yao ikidaiwa kuwa ni eneo la Hifadhi la Pori la Akiba la Kigosi Muyowosi. Wananchi hawa wameiomba Serikali kufika na kuhakiki mipaka ili kubaini ukweli bila mafanikio badala yake *operation* za kuwafukuza zinaendelea kila uchao kufukuzwa,

10 NOVEMBA, 2022

kuchomewa moto makazi, kutaifishwa mifugo, kupigwa faini na kupigwa na kuumizwa kinyume na haki na misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kusitisha *operation* zinazoendelea katika Kijiji cha Ilunde B, Wilayani Kibondo Mkoa wa Kigoma na badala yake ufanyike uhakiki wa mipaka ambao utashirikisha wananchi wote na Serikali ya eneo husika ili kuondoa utata wa mipaka uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wananchi wa vijiji 33 vya Wilaya ya Mbarali Mkoani Mbeya kufukuzwa kwenye maeneo ya makazi na kilimo kwa kisingizio kwamba wako ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dkt. Angelina Mabula amepiga marufuku shughuli za kilimo kuendelea katika maeneo hayo ambayo kwa muda mrefu wamekuwa wakiyatumia kwa shughuli za kilimo cha mpunga ambapo mchele huo umekuwa ukiuzwa ndani na nchi jirani za Uganda, Malawi, DRC, Zambia, Visiwa vya Komoro, Sudani Kusini, Kenya na Rwanda ambapo linapunguza tatizo la upungufu wa chakula nchini, kuingiza kipato kwa wananchi na kupata fedha nyingi za kigeni kutokana na mauzo ya mchele nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa maeneo hayo kwa muda mrefu wameiomba Serikali kufika eneo hilo ili kupitia na kuhakiki mipaka baina yao na hifadhi lakini badala yake limetolewa tamko la kuondolewa bila kusikilizwa.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi ya Waziri ambayo yanalenga GN No. 28 inayolalamikiwa na wananchi kila sehemu ambapo imetanua mpaka bila ushirikishwaji wa wananchi na kwa sehemu kubwa haina uhalisia kwa kuwa ramani haijafanyiwa uhakiki wa mipaka na kutoa tafsiri ya ramani chini ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wananchi hawa waachwe waendeleo na shughuli zao za kilimo na Serikali iende ikakae na wananchi hao ili kufanya uhakiki wa mipaka na pande zote kujiridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, TANESCO kuingia mkataba na kampuni binafsi ya kutoa huduma ya kuendesha kituo cha huduma kwa wateja (*callcenter*) ambapo TANESCO ina *otusource* uendeshaji wa kituo chake cha huduma kwa wateja kwa kampuni binafsi kazi iliyokuwa ikifanywa na vijana wa Kitanzania 279 waliokuwa na mkataba na TANESCO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za kukasimu shughuli za uendeshaji wa kituo cha huduma kwa wateja kwa kampuni binafsi hazijawekwa wazi. Vijana 279 wanaachishwa kazi kumpisha mtu binafsi kuendesha huduma hiyo, haya ni mawasiliano nyeti yanayofanywa na wateja kupitia *callcenter* ya TANESCO inakuwaje yaendeshwe na mtu binafsi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu TANESCO ititishie uamuzi wake wa kubinafsisha vituo vya kutoa huduma kwa wateja (*callcenter*) na badala yake iimarisha kitengo hicho na kiendeleo kuendeshwa na shirika hilo huku ajira za vijana 279 zikilindwa.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, wafugaji walioshinda kesi Mahakamani zaidi ya ng'ombe 6,000 lakini Serikali imekaidi kurejesha mifugo yao, licha ya wananchi hawa kushinda kesi Mahakamani miaka zaidi ya mitatu iliyopita mifugo yao haijarejeshwa na Serikali hali inayopelekea familia hizo kuingia kwenye lindi kubwa la umasikini. Sababu za kutorejesha mifugo hiyo hazitolewi na hili sio jambo zuri kwa nchi inayofuata misingi ya sheria ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iwarudishie wananchi mifugo yao au kiasi cha fedha kinacholingana na thamani ya mifugo iliyoshikiliwa kama Mahakama zilivyoamua. Nawasilisha.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge wanaanza sasa kuchangia Waheshimiwa Mawaziri na niwakumbushe matakwa ya Kanuni ya 113 ambayo yanazungumzia Bunge kukaa kama Kamati ya Mpango na nini kinatarajiwa kutoka Upande wa Serikali. Kanuni ya 113(5)(c) hii inahusu Serikali, Mjadala kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Taifa utahitimishwa na Serikali kwa kutoa maelezo mafupi, kwamba imepokea maoni na ushauri wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia katika mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Awali ya yote nianze kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametufanya tuwepo hapa. Pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya

10 NOVEMBA, 2022

Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayowafanyia Watanzania wote. Tatu, nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika kwa namna ambavyo unaongoza Bunge hili kwa viwango hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yamejadiliwa na Waheshimiwa Wabunge, nami niungane nao kwanza kwa kukubali mapendekezo ambayo wamependekeza katika Mpango huu hususani katika Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamezungumzwa, suala la Bandari, Reli, TAZARA, Meli, Barabara na Miundombinu yote yamezungumzwa. Aidha, nianze kwanza na Bandari ya Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Tanga kwa historia ilianzishwa tangu mwaka 1888 lakini mwaka 1891 ndipo ilipokamilika. Kulikuwa kuna changamoto za uendeshaji na ujenzi wa Bandari hii, ndipo Serikali ilipoamua kwamba tuiboreshe Bandari hii ya Tanga. Ilifanyika katika awamu mbili na awamu ya kwanza, ilikuwa ni kufanya *dragging* kutoka kwenye kina kirefu umbali wa kilometa 1.7 mpaka kwenye gati. Awamu ya pili, ilikuwa ni kwa ajili ya kujenga gati mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe ufafanuzi hapa kwa sababu kumekuwa na sintofahamu ya kuelewa kwamba kilometa 1.7 ya *dragging* kwa maana ya kuchimba kile kina iko katika awamu gani katika miradi hii yote miwili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza, ilihusisha ujenzi huo na kuchimba kina kutoka mita tatu

10 NOVEMBA, 2022

mpaka mita 13 ili meli kubwa ziweze kupita na kufika kwenye gati ama Bandari yenyewe ya Tanga. Kwa bahati nzuri mradi huu ulianza mwaka 2019 na umekamilika tayari kwa 100% na thamani ya mradi huu ilikuwa ni bilioni 172.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili, ilikuwa ni kwa ajili ya kujenga gati mbili na hizo gati ni awamu ambayo imeanza mwaka Septemba, 2020 na thamani ya mradi kwa awamu ya pili ilikuwa ni kiasi cha silingi bilioni 256.8. Kwa awamu hii mradi huu una asilimia 79 maana yake Mkandarasi bado yupo *site*. Nimeona nitoe ufafanuzi huu ili ieleweke kwa Watanzania wote na Bunge kwa sababu kulikuwa na mkanganyiko wa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nilitolee ufafanuzi ni suala la Viwanja vya Ndege Nchini. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia kwamba ndege hazitui usiku, ni kweli Ndege hazitui kwa sababu viwanja vichache ndio vyenye taa. Tuna Kiwanja cha Mwalimu Nyerere kina taa, Songwe, Zanzibar na Mwanza. Katika mpango huu ambao sasa hivi Serikali imewekeza, tunakwenda kujenga viwanja vya ndege visivyopungua nane na tunakwenda kuweka na taa za kuongozea ndege usiku na mchana kikiwepo kiwanja chetu cha hapa Dodoma. Waheshimiwa Wabunge ninyi ni mashahidi kwamba kiwanja chetu hiki hakina taa na ndio maana ndege haiwezi kutua usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tulilazimika kuendelea kukijenga kiwanja hiki na kukiboresha kutokana na kwamba Kiwanja kipya cha Ndege cha Msalato ambacho hivi karibuni Mheshimiwa Rais ameshuhudia utiaji saini wa zaidi ya shilingi bilioni 360

10 NOVEMBA, 2022

kitakamilika mpaka 2024/2025. Tukaona kwa sababu Serikali tayari imekwishahamia Dodoma, kulikuwa kuna hoja kwamba kwa nini hatukuona kwamba kuna umuhimu wa kukiacha vile vile tusebiri hiki Kiwanja cha Msalato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba tumeona umuhimu wa kuboresha kiwanja hiki kwa sababu hapa ndipo Makao Makuu ya nchi, hapa ndio Makao Makuu ya Serikali na hapa ndio Makao Makuu ya Chama Tawala. Tukiwa na viwanja viwili katika mataifa mengine ndivyo wanavyofanya kwa maana ya kwamba hata kukiwa na *emergence landing*, inakuwa ni rahisi, inaweza kuwa kukawa na changamoto Kiwanja cha Msalato ndege ikatua hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja huu tayari tumekwishasaini zaidi ya Sh.6,438,450,107/= kwa ajili ya ujenzi wa taa na Mkandarasi ataanza kazi mara moja ambaye anaitwa *Jess Españiola* ambaye ataanza wakati wowote katika Kiwanja chetu cha Dodoma. Vile vile kuna viwanja vingine ambavyo vinaendelea na ujenzi kuna Kiwanja cha Songwe ambacho karibia kina kamilika, Kiwanja cha Songea, Mtwara, Iringa, Manyara ambacho pia tutaanza, kuna Kiwanja cha Kigoma, Tabora, Shinyanga na maeneo mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ligin ambalo limezungumzwa sana hapa ni suala la ATCL kwamba ndege hazitoshi. Ni kweli hazitoshi, lakini katika Mpango huu Mheshimiwa Rais ametuagiza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kununua ndege tano mpya ikiwemo ndege ya mizigo ambayo itaingia nchini mwakani mwezi Machi.

10 NOVEMBA, 2022

Kwa hiyo tutakuwa na ndege 16 zaidi, kwa hiyo hata kwa hizi changamoto za *route* ambazo zinatokea sasa hivi kutokana na kwamba ndege ni chache, ikitokea tu hitilafu kidogo maana yake hiyo *route* inaharibu *route* nzima. Sasa zikiingia Ndege hizi tano katika Mpango huu ambao Waheshimiwa Wabunge wamependekeza nina hakika suala la usafiri wa anga litakwenda kuimarika zaidi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naunga mkono hoja hii ya Mpango na yale yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wamesema hapa tunakwenda kuyaweka na hasa ambayo hayakuwepo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Waziri wa Nishati ajiandae.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Pili, niseme tu kwamba Waheshimiwa Wabunge tumeyasikia maoni yao na ushauri wao na ndoto zao na sisi kama Wizara na upande wa Serikali tutaendelea kuyafanyia kazi kadri ambavyo Mwenyezi Mungu anatumia na upatikanaji wa rasilimali *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nichangie mambo machache tu. Kwanza ni ukweli kihatarishi namba moja ambacho kinatukabili kama Taifa ni mabadiliko ya Tabianchi. Kama Serikali ukiangalia kwamba ukuaji wa *population* unakua kwa wastani wa 3.2% na Sensa iliyopita imetuonesha kwamba umri wastani wa Mtanzania ni kati ya miaka 16 na 18 maana yake *society* ambayo ina watu wenye umri mdogo sana lakini sekta iliyoajiri watu wengi ndiyo ambayo ina mchango mdogo na ukuaji wake ni mdogo ni jambo la ukweli ambalo halipingiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua hatua za maksudi, nalishukuru Bunge, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa niaba ya wakulima, Serikali imeongeza fedha katika mwaka uliopita na tumeanza kuchukua hatua, tunazo ekeri jumla ya Milioni 29 zinazofaa kwa umwagiliaji, huko nyuma kwa muda mrefu tumekuwa tukijenga miundombinu ya umwagiliaji ambayo imekuwa inasubiri na yenyewe kudra ya Mungu mvua inyeshe ndiyo watu waweze kuitumia hiyo miundombinu. Kwa mwaka huu wa fedha tunajenga Mabwawa 13, niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge na Kamati ya Bajeti, hatua ya Serikali kujenga mabwawa katika maeneo ya Kati siyo hatua ya kutilia mashaka. Ni hatua ambayo umefanyika utafiti wa kisayansi na kujiridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajenga bwawa kubwa la Msagali liloko Mpwapwa lenye uwezo wa kuhifadhi Milioni 95m³ ambalo litamwagilia eneo kubwa la umwagiliaji. Tunajenga Mabwawa Dodoma, Simiyu, Mwanza, Singida, Tabora, Kigoma na Manyara. Haya ni kwa mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili ambayo tumechukua mtaona mwaka ujao wa fedha mlitupitishia fedha hapa ya kwenda kufanya *feasibility study* na *design* kwenye Mabonde 22 ya nchi yetu, yakiwemo Mabonde ya *Lake Victoria*, Mabonde yaliyoko Ziwa Nyasa, Mabonde yaliyoko Mto Ruvuma. Mabonde yote haya sasa hivi tumesha-*commission* na watu wanafanya *feasibility study* ambayo tutaanza kuyajenga katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto inayokabili sekta ya kilimo ni tija na tija ina-*equation*; Kwanza ni utafiti, Pili ni uzalishaji wa mbegu, Tatu ni *extension services*, Nne ni kuwa na miundombinu ya uhifadhi na miundombinu ya umwagiliaji. Serikali ya Awamu ya Sita imeanza kuchukua hatua hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye uzalishaji wa mbegu mmetupitishia fedha hapa, kutoka Bilioni 15 kwa ujumla wake mpaka Bilioni 83. Tunafanya nini? Tumeanza kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya kuzalisha mbegu, ambayo toka tunapata uhuru hayakuwepo haya mashamba yakiwa na miundombinu ya umwagiliaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza kujenga mwaka huu tunajenga hekta 95,000 kuongeza mtandao wetu wa umwagiliaji. Miundombinu ya *DADPs* na mingine yote ambayo ilikuwa inasubiri mvua za Mungu na yenyewe tunaijengea mabwawa. Kwa hiyo, nilitaka niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba hii ni hatua ambayo tunaichukua na niseme hapa kwamba kilimo ni *process*, hatuwezi kutegemea matokeoya kwenye kilimo kesho, ni lazima tu-*invest* kwa muda mrefu. (Makofi)

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ninataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge msiwe na hofu na mashamba ya *block farm*, kwa nini? Vijana wengi wanaomaliza Vyuo Vikuu hawaendi kwenye kilimo kwa sababu kubwa tano: Moja, hawana ardhi, Mbili, hawakopesheki, Tatu, Teknolojia zimepitwa na wakati, Nne, suala la masoko ya uhakika. Miradi hii ya jumla ya ekari 188,000 ambayo *phase one* tunaanza na Dodoma na Chunya itatengeneza ajira za vijana 40,000 watakaoenda kulima shambani. Serikali inatumia Bilioni 200 gharama ya ajira moja ni Shilingi Milioni Tano. Kwa hiyo nilitaka tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge maoni yao tumeyapokea, tunayachukua lakini hii ni *process* ya muda mrefu ambayo tutaenda kufanya kazi pamoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Sanga ameongelea miradi ya zaidi ya Bilioni Hamsini tuliyoisaini Mbarali miradi ile haijafa. Tunaenda kujenga zile skimu zote ambazo zilisainiwa mbele ya Mheshimiwa Rais. Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Haya ahsante sana. Tusaidie tu jambo moja, hayo mabwawa makubwa yanayojengwa yanajazwa na maji kutoka wapi? (Makofi)

WAZIRI WA KILIMO: Ahsante. Mheshimiwa Mwenyekiti kuna njia mbili ambazo tutajaza maji kwenye mabwawa na nitaliomba Bunge lako, Kamati ya Kilimo imeshaenda kutembelea imeona na tutafanya *tour* ili waone. Kuna njia mbili za kujaza maji na niseme *specifically* Dodoma najua hofu iko Dodoma.

10 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Wewe nenda hapo kwa sababu muda wetu umeenda Mawaziri wanasubiri nimeuliza swali dogo tu.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna njia mbili tu. Moja tunatega maji ambayo kipindi cha mvua yanasafiri yanayopotea. Nasi wote tunajua hapa katikati ya Dodoma, Morogoro huwa tunakaa masaa mamilioni ya lita ya maji yanapita, hiyo ni njia ya kwanza. Njia ya pili Mkoa wa Dodoma una-*water reserve* nyingi mno *underground*. Tunalo Bwawa hapo Chinangali ambalo linajaza lita milioni 32 kwa visima vitatu ambapo shamba la hekta 1000 litahudumiwa kwa mwezi mzima bila kutafuta maji sehemu nyingine. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilishamtaja Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji Viwanda na Biashara atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ajiandae.

WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie kwenye wasilisho hili la Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Pili naomba niseme Waheshimiwa Wabunge kama Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara tumewasikia, maoni yenu tumepokea na tunakwenda kuyafanyia kazi ili tunapokuja sasa na mpango wa maendeleo kwa mwaka 2023/2024 uwe umebeba maaoni ya wananchi kwa sababu Wabunge ni wawakilishi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya hasa kwa kufungua Taifa

10 NOVEMBA, 2022

letu, kwa kutuletea wawekezaji na kutuletea wafanyabiashara wa kutosha pia kuwapeleka wafanya biashara wa Tanzania kulifikia soko la Dunia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamesemwa mengi kama nilivyosema tumepokea naomba nisemee moja tu nalo ni kuhusu *Bagamoyo Special Economic Zone*. Tunapoiongelea eneo maalum la kiuchumi la Bagamoyo lina miradi kadhaa ambayo bandari ni sehemu mojawapo ya miradi hiyo iliyopo kwenye eneo hili. Kwa hiyo, ningomba sana Waheshimiwa Wabunge na nashukuru mmesema mawazo mema na mazuri ambayo kama Serikali tumeendelea kuyafanyia kazi na niwashukuru sana Viongozi wetu wa Taifa hili kuanzia Rais wetu Mstaafu wa awamu ya Tatu aliona na likawekwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo ambayo imeanza kutekelezwa mwaka 2000 mpaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza sana Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Nne akalibeba na kuanza utekelezaji wake, Mheshimiwa Rais wetu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli naye kwenye Awamu ya Tano alilifanyiakazi na ikafika alipolifikisha. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amelibeba jambo hili na ameliondoa kwenye mkwamo uliokuwepo. Kwa sababu mwanzo ilikuwa inaongelewa bandari peke yake, Mheshimiwa Samia suluhu Hassan amesema tukijenga bandari peke yake bila miundombinu mingine wezeshi hiyo bandari haitofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijenga bandari peke yake bila kuwa na Mji wa viwanda pale Bagamoyo tutakuwa hatujafika dhamira njema iliyowekwa kwenye

10 NOVEMBA, 2022

Dira ya Taifa ya Maendeleo. Katika hili ukijenga bandari bila kuwa na *logistic hub* utakuwa hujafanya lolote. Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo na nikushukuru sana wewe Mheshimiwa Mwenyekiti na Bunge lako Tukufu lilitupitishia bajeti na sasa tunahitimisha kufanya mapitio ya mpango kabambe wa eneo zima la Bagamoyo ambalo tunahitimisha Tarehe 15/11/2022 tukishakuwa na *master plan* mpya itatueleza sasa ni kipi cha kufanyika kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iliulizwa pia kuhusu eneo hili kuhusu fidia wapi tumefikia. Niseme kwa historia nilioitoa yapo maeneo ambayo tayari yalishalipiwa fidia na yako maeneo ambayo yalikuwa hayajalipiwa fidia. Eneo lote ambalo lilitarajiwa enzi hizo kujengwa bandari lote la hekta 800 lilishalipiwa fidia, lakini eneo lote ambalo lilikuwa lijengwe Chuo cha Teknolojia tayari lilishalipiwa fidia nalo ni eneo la hekta 179.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lote pia ambalo lilikuwa lijengwe Chuo cha Uongozi ambalo ni hekta 198 lililipiwa fidia, eneo lililobaki lilikuwa halijalipiwa fidia kwa sababu kulikuwa na changamoto ndani yake na ndiyo maana ya Serikali kuelekeza sasa turejee kwenye mpango kabambe mpya ili eneo hili sasa tuhitimishe na tuwalipe fidia wale waliotakiwa kulipwa, lakini wapo Watanzania wenye maeneo yao kwenye eneo hili ambao wako tayari kuwekeza hatutakiwi kuwalipa fidia kwa sababu wanawekeza kulingana na mpango kabambe. Kwa hiyo, hili tunalibeba tunakwenda nalo niwahakikishie wananchi wa Bagamoyo, niwahakikishie Watanzania tuko tayari kwa ajili ya eneo hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Waziri wa Madini ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia hoja hii ya Mpango. Niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara ya Nishati maoni yao na mapendekezo tumeyachukua na tutayafanyia kazi kwa upana wake. Niongelee tu kwenye maeneo machache mengine ni ya kuweka taarifa sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza kwenye gesi asilia. Kama tulivyosema juzi Serikali imeipa mtaji TPDC wa dola bilioni 1.193. Kwa kubadilisha deni la bomba la gesi kuwa sasa pesa ambayo TPDC inaweza ikaitumia. Kwa hiyo hatuna wasiwasi na tunakoelekea kwamba TPDC itaweza kukopesheka na kufanya biashara katika mazingira ambayo itakuwa na *bargaining power* za kuweza kupata mikopo yenye riba nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili tayari mikataba ya *interest MOU* zimesainiwa kati ya Tanzania na Uganda, Tanzania na Kenya, wenzetu wa Malawi na Rwanda wameonesha *interest*, kwa hiyo tukitoa gesi hii Dar es Salaam na Mtwara kupeleka Uganda hii Mikoa yote ya katikati itapata tukipeleka Kenya Mikoa ya katikati itapata kwa hiyo humu ndani tutaisambaza vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine ambalo nimeona nilisemee kidogo ni eneo la idadi ya vijiji vyenye umeme na visivyokuwa na umeme. Ukurasa wa 32 wa Mpango umeeleza taarifa na ni taarifa sahihi na naomba

10 NOVEMBA, 2022

niseme kwa sasa. Vijiji tulivyonavyo kwa mujibu wa takwimu za TAMISEMI ni 12,345, kwa mujibu wa taarifa za TAMISEMI na kwenye mpango imeandikwa hivyo. Vijiji vyenye umeme mpaka kufikia Tarehe 31/10/2022 ni 9,163, Vijiji ambavyo bado ambavyo vyote viko kwenye REA III round II ni Vijiji 3,182 ambavyo mikataba yake inaendelea kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya takwimu ilitokea kwenye mazingira tuliyokuwa tunafanyia kazi. Huko nyuma kuna vitongoji vikubwa ambavyo vilipewa umeme na wenzetu wakavihesabu kama vijiji. Sasa vimeondolewa kwenye idadi ili tubakie na vijiji halisia na Waheshimiwa Wabunge tunafahamu kwenye maeneo yetu, maeneo ambayo tumeweka umeme kwenye vitongoji lakini vilihesabiwa kama vijiji. Sasa taarifa sahihi ni hii Vijiji 12,345, Vijiji 9163 tayari umeme na Vijiji 3182 umeme bado lakini vina mikataba vyote na vinafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Tatu ni kwenye uhakika wa umeme na wenye gharama nafuu. Mpango wetu umeelaza vizuri kabisa kwenye ukurasa wa 18, ukurasa 32 na kiambatisho C ukurasa wa 1- 3, umeeleza miradi mingi sana ya uzalishaji na usafirishaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mchangiaji alisema hata mpango wa kutoa umeme Mwalimu Nyerere kuuleta Chalinze haupo. Ukurasa wa 33 umeeleza vizuri kabisa kwamba tunatoa umeme Mwalimu Nyerere na tutauleta Chalinze na kazi inaendelea tunatarajia ikamilike mwaka unaokuja na miradi ya kutoka Chalinze kuja Dodoma, kutoka Chalinze kwenda Mwalimu Nyerere yote imeelezwa kwenye mpango.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye miradi ya uzalishaji kuna mwenzetu mmoja alichangia kwamba...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri hapo ndiyo ambapo kidogo huwa tunachanganyikiwa, mwaka ujao kwa maana ya 2023 au mwaka 2024 maana unasema mnatarajia ikamilike mwaka ujao, wakati taarifa tulizonazo ni 2024.

NAIBU WAZIRI WA NSHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kutoa umeme Mwalimu Nyerere kuuleta Chalinze unakamilika mwaka wa fedha huu. Nina maana ya Januari kuelekea Juni, mwaka wa fedha huu. Kwa hiyo, kwa *program* tuliyokuwa nayo itakamilika kabla ya Bwawa la Mwalimu Nyerere kukamilika ambalo kwa mujibu wa mkataba wa *extension* nitakaousema baadae inatakuwa kuwa Oktoba mwakani. Kwa hiyo, ni mwaka wa fedha huu tuliopo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo mpango umeitaja kwa ajili ya uzalishaji. Tunao Mwalimu Nyerere, *megawatt 2115*, tunayo Rusumo unakamilika muda siyo mrefu *megawatt 80*, tunayo Ruhuji inakuja *megawatt 358*, tunayo Rumakali *megawatt 222*, tunayo Kikonge *megawatt 300* tuna miradi ya upepo na jua *megawatt 300*, tunayo Kinyerezi *One Extension megawatt 185*, zote hizo tunatarajia kwamba zitatupatia umeme kwa mujibu inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unipe nafasi kidogo ya kueleza mambo mawili kwenye mradi wa Mwalimu Nyerere.

10 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Sasa kila Waziri anaomba apewe nafasi kidogo tu sijui nimkate mmoja ili ndiyo niwe nimezigawanya hizo? Haya dakika moja malizia.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa sababu ya muda nizungumzie vitu viwili tu. Kimoja muda tuliouongeza kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere ni mwaka kwa mujibu wa mkataba, tumeongeza mwaka mmoja na muda huo utakapoisha ndiyo tutaanza kugombana kuhusu nani kachelewesha mradi.

MWENYEKITI: Mwaka mmoja ndiyo mpaka lini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Oktoba mwakani kwa mujibu wa mkataba tuliosaini. Iko taarifa na mpango kazi wake aliouleta anapoomba miaka miwili sisi tulimwambia tunampa mwaka mmoja na wenzetu wataalam wanaendelea kuchanganua ule mpangokazi wa utekelezaji ili u-fit mwaka mmoja lakini mkataba wa nyongeza *extension of time* ni mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo kuhusu hii habari inayosemwa ya *liquidated damages*, taarifa sahihi ni kwamba *liquidated damage* kwenye mkataba wa Mwalimu Nyerere ni 0.1% kwa kila siku kwa maximum ya asilimia Tano siyo asilimia Kumi siyo zaidi ya hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kwenye CSR tunaambiwa tunatoa taarifa kwamba tungezikata hizi pesa. Mkataba unatueleza kwamba tumpe Mkandarasi atekeleze CSR, tulikuwa hatujakubaliana miradi ya kutekeleza sasa tumekubaliana Mkandarasi ataanza

10 NOVEMBA, 2022

kutekeleza CSR za bilioni 263 na tuko ndani ya muda na tutakamilisha kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sawa, sasa ngoja unajua huu mradi ukitolewa Tarehe hizi zinazotuchanganya sisi wananchi ndiyo kidogo tunapata hizo changamoto. Tunatamani taarifa kutoka upande wa Serikali ziwe zinafanana, mradi kwa maelezo uliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba mradi unakamilika, mitambo ya kutoa umeme kutoka Bwawa la Mwalimu Nyerere mpaka Chalinze mwaka huu wa fedha, nimekuelewa sawasawa? Mwaka huu wa fedha? Sema kwenye kisemeo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

MWENYEKITI: Mwaka huu ambao unaisha Juni na Bwawa la Mwalimu Nyerere ujenzi kwa mujibu wa taarifa yako ujenzi unakamilika Oktoba, 2023.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi.

MWENYEKITI: Haya, ahsante. Sasa hiyo ndiyo taarifa iliyotolewa na Naibu Waziri hapa Bungeni na sisi wananchi tunachukua hiyo ndiyo taarifa sahihi. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ajiandae. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie katika Mpango huu. Nianze kwa kuupongeza mpango pia niseme tu tunapokea maoni na ushauri wa Wabunge ambao wameutoa japokuwa hapo baadae nitatoa ufafanuzi kwa kufafanua baadhi ya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba Wizara ya Ardhi ni Wizara wezeshi, na Mpango wa Maendeleo unaozungumzwa katika suala zima la uwekezaji hususani kwenye miundombinu Wizara ya Ardhi inayo mchango mkubwa kuhakikisha kwamba inaweka mazingira mazuri ili kuweza kuona mpango huo unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha huu ambao tunaendelea na tutakaokwenda kuendelea nao mwaka ujao, tunao ule mradi wa kuimarisha miundombinu kwa ajili ya upimaji. Tunatambua nchi imepimwa kwa asilimia isiyo zidi 30 ni kama asilimia 25. Kwa hiyo kwa sasa tunazo pesa zile ambazo ni Dola za Kimarekani milioni 65 ambazo zitatumika kuimarisha miundombinu ya upimaji na tutakwenda kupima nchi walau katika sehemu kubwa. Lakini pia kuna ile ya uboreshaji milki, ambazo ni Dola za Kimarekani milioni 150. Kwa hiyo ukikamilisha maeneo hayo maana yake tutakuwa na zile *base map* ambazo zitakuwa zinatupa picha ya kuweza kupanga matumizi ya maeneo katika nchi nzima ikiwemo na hiyo miradi ya kimkakati ambayo tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchangiaji jana Mheshimiwa Mbunge wakati anachangia ilionesha kwamba pengine maamuzi ya Serikali ya eneo la Mbarali

10 NOVEMBA, 2022

yangeweza kufifisa matarajio ya Watanzania pengine katika suala zima la kuichumi. Naomba kwanza niwatoe wasiwasi wananchi kwamba, mpango ule ambao umewekwa na Serikali ikiwemo hiyo ya mabwawa kama alivyosema Waziri wa Kilimo uko pale pale na mabwawa yale yapo mbali na eneo ambalo wananchi wameondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile maeneo yale ambayo wananchi wameondolewa ni vijiji vitano na si vijijini 48 kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge alisema. Vijiji hivyo vitano vinavyoondolewa tayari elimu imeanza kutolewa ambapo maendeleo yanaenda vizuri na wanaweka alama kuhusiana na wapi wanaishia. Lengo letu ni kuhifadhi lile eneo ili maji yaendeleo kutiririka katika Mto Ruaha ambayo yanapeleka kwenye Bwawa la Mwalimu la Nyerere. Kwa hiyo tukiharibu miundombinu ya pale maana yake ni kwamba tutajikuta tumeharibu mkakati mzima wa kuwa na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo suala la kusema kwamba pengine labda tuanaondoa uchumi wa wananchi, tunaimarisha uchumi wa wananchi kwa kuwa na miundombinu ya uhakika itakayotuma umeme wa uhakika na uzalishaji utakuwa ni mzuri...

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kuna taarifa, Mheshimiwa Sanga.

10 NOVEMBA, 2022

T A A R I F A

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafuatilia majibu ya Mheshimiwa Waziri. Katika miradi 54 ambayo yamesaini kuna maeneo mawili ambayo wananchi wanaondolewa na miradi inaenda kujengwa. Moja ya eneo hilo linaitwa Mwendamtitu wanaenda kujenga mradi wa umwagiliaji na wananchi wanaondolea. Eneo la pili linaitwa Madibila *Phase II* wanaenda kujenga mradi wa umwagiliaji na wananchi wanaondolewa. Katika maeneo hayo wanayowaondowa Serikali imeshapeleka *combined harvest machine 15* kwa ajili ya wananchi hao ili waweze kuendelea kulima, lakini kwa ripoti ya Mheshimiwa Waziri nampa taarifa kwamba hata dakika hii ninavyozungumza wananchi wanaweka *beacon* kwenye maeneo hayo ili wananchi waondoke na hawana taarifa na hawajashirikishwa.

MWENYEKITI: Kwa sababu Waziri ametaja idadi ya vijiji, kasema ni vijiji vitano na si 48 hivi vijiji unavyovitaja wewe viwili, vipo katika vitano ambavyo Waziri hajavitaja, vinavyoondolewa.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu hajataja majina ya hivyo vijiji, kwa hiyo sijajua ni vijiji gani anavyovitaja lakini ninavyotaja mimi, ni hivi vijiji vya...

MWENYEKITI: Labda hivyo vipo kwenye yale mengine. Mheshimiwa Waziri vijiji vitano vinanavyoondolewa haya mawili sijajua kama unayo ile orodha ya hivyo vijiji vitano ama hauna tunaweza kupata taarifa baadae.

10 NOVEMBA, 2022

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo taarifa yote ya vijiji vinavyobaki ambavyo ni kumi na tano, vijiji vinavyoondolewa ni vitano. Halafu...

MWENYEKITI: Sawa sasa hebu tusaidie hivyo vijiji vitano, hivi viwili anavyovitaja Mheshimiwa Mbunge hapa vimo katika hivyo vitanno au havimo.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vinavyoondolewa ni kijiji cha Luhanga, Madundasi, Msanga, Iyala na Kilambo. Mabwawa yanayokwenda kujengwa katika eneo lile katika Wilaya ya Mbarali, mabwawa yaliyotajwa yanajengwa na umbali wa bwawa ambapo yapo hayako kwenye yale maeneo ambayo wananchi wanaondolewa. Tunalo bwawa mmoja Scheme ya Msesule liko kilometa tano kutoka pale ambapo wananchi wanatolewa, tunayo scheme ya Utoro na Scheme ya umwagiliaji ya Isenyela ziko kilometa 11 kutoka pale mwananchi wanapotolewa. Tunayo Scheme ya Chozi na Scheme ya umwagiliaji ya Heman iko kilometa 30 kutoka pale wananchi wanapotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokisema hapa, lengo la Serikali inachofanya ni kutaka kuweka mazingira mazuri kwa miradi ya kimkakati ambayo ndiyo inakwenda kukuza uchumi, moja wapo ikiwa ni hilo bwawa la Mwalimu Nyerere.

MWENYEKITI: Mimi nimekuelewa Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Mbunge ulikua unatoa taarifa, hivyo vijiji

10 NOVEMBA, 2022

vilivyotajwa kuondoka, Mheshimiwa Waziri amevitaja, hizo *scheme* mbili ulizotaja zipo katika vile vijiji vitano au ni nje kwa kuwa ulikuwa hujamsikia bado Waziri.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo kwenye hivyo vijiji vitano kwenye Mwendamtitu na Madibila *phase II*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo hizo *scheme* zipo upande gani? Hizo *scheme* mbili alizozitaja.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Scheme* ya Madibila *Phase II*, *Phase I* imekamilika, *Phase II* kuna kipande ambacho kinaingia kwenye GN 28 siyo *Phase II 100 percent*. Kuna kipande kinachoingia ndani ya GN 28. Tunachokifanya ni kwamba wakati *technical team* inaendelea kule *ground* na sisi ndani ya Serikali tunaendelea kufanya *consultation*. Kwa hiyo nimwambie ...

MWENYEKITI: Haya hiyo ni nini? Mbarali nini, Madiba *Phase two*, hiyo *scheme* nyingine Mheshimiwa Waziri.

MHE. FESTO R. SANGA: Hiyo *scheme* nyingine ipo Mwendamtitu.

MWENYEKITI: Haya Mwendamtitu? Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, imo au haimo?

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *scheme* ambayo inayoathirika ni Madibila *phase II* tu.

MWENYEKITI: Pekee yake?

10 NOVEMBA, 2022

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, yes.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Ardhi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa kutoa ufafanuzi pia. Zoezi ambalo linaendelea sasa hivi ni kuonesha mipaka kwa sababu kilio cha wananchi wa Mbarali alichokuwa anakisema walikuwa wanalamamikia GN Namba 28. GN namba 28 iliwekwa 2008 kwa Muswada ambao ulipitishwa hapa na baadaye ukaridhiwa na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya ku - *protect* yale maeneo ya hifadhi ambayo yanapeleka Maji Mto Ruaha na unaokwenda mpaka Mtera pamoja na Kidatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kile kinachofanyika pale sasa hivi ni kuhakikisha kwamba, mpaka unaainishwa ili maeneo yale ambayo yanatunza vyanzo vya maji na mapokeo, ile *catchment area* yote ya maji, iweze kubaki wazi na kurudisha ecolojia ya pale ili miradi tunayokwenda nayo isije kuwa imevuruga yote. Kwa sababu tunatambua pia uhifadhi hauruhusu shughuli za kibinadamu; tukiruhusu maana yake tunakwenda kuharibu pia ile hifadhi ya Mto Ruaha.

MHE. BONIPHANCE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

10 NOVEMBA, 2022

MHE. BONIPHANCE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nataka kuiona hii dhana ya kusema sawa tunatunza vyanzo vya maji kwenye eneo. Hivi tatizo la Mto Ruaha kuisha maji, ni kwamba maji hayaendi mtoni au ni kwamba ule mto umekuwa tambarare maji yote yakienda yanapita yote. Lazima hili nalo tulione, Kwa sababu maji yanaweza kuingia masaa yote ya mvua lakini yakaondoka yote yakaenda ziwani. Tutafute *alternative* nyingine ya kuweza kuzuia maji kwenye Mto Ruaha. (Kicheko)

MWENYEKITI: Nadhani alikuwa anachangia zaidi kuliko kukupa taarifa, Mheshimiwa Waziri, malizia mchango wako.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza pamoja na mchango wake lakini majibu anayo pia. Kwa sababu unapofanya shughuli za kibinadamu karibu na eneo la hifadhi ya mto maana yake yale maporoko zile *siltation* inayofanyika inakwenda kuondoa kina cha maji. Matokeo yake...

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

MWENYEKITI: Mheshimiwa una taarifa kuhusu nini tena?

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki anachokizungumza, kwamba maji ya Mto Ruaha yamekauka kutokana na shughuli za wale wananchi wanaolima pale.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa taarifa, wananchi wanaolima lile eneo linaloondolewa ambalo ni hekta 53,000, wanalima kati ya mwezi wa kumi na mbili, wa kwanza hadi wa nne na watano. Yale maji hayachepushwi kuingia mashambani kwa wakulima, lakini ni *estate* mbili ambazo ni za mwekezaji na sisi tunaungana nao wale wawekezaji, ndio wanaotumia maji yanayotoka kwenye Mto Ruaha kwenda *estate* zao. Kwa hiyo, si wale wakulima wanaotumia wao maji. Wanatakiwa mlifahamu hilo.

MWENYEKITI: Sawa, umeeleweka. Mheshimiwa Waziri hajasema wale ndio wanaokausha maji. Sijamsikia akisema maneno hayo, kwamba shughuli zile ndizo zinakausha maji ila alikuwa anaendelea na sentensi kwamba ukifanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya vyanzo. Sasa alikuwa anaendelea kwa sababu alikuwa anamjibu Mheshimiwa Getere. Kwa hiyo alikuwa hajamaliza hoja yake ni nini kwenye hili. Kwa hiyo nampa nafasi Mheshimiwa Waziri, endelea.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kutoa ufafanuzi ni wazi ni kweli nilkuwa naendelea moja wapo nimesema ni kufanya shughuli za kibinadamu. Pia ule uharibifu mkubwa wa mazingira uliopo katika maeneo yale ndicho chanzo pia kwanza cha kukosekana mvua ya uhakika ambayo inaweza ikapeleka maji katika yale maeneo. Kwa hiyo kile kitu kinachofanyika pale kinafanya pia hata mtiririko mzima wa maji, vile vijito vinavyopeleka maji kwenye Mto Ruaha navyo vinakauka. Maana yake ni kwamba hatima yake kutakuwa na ukame ambao hautaweza kurejesha tena ekolojia ya pale jinsi ilivyo. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe unafahamu, historia ya eneo lile namna ambavyo Tume na Kamati mbalimbali ...

MHE. FRANCIS L. MTEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu taarifa nimevumilia sana.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume na Kamati mbalimbali zikiwemo hata na Kamati za Bunge, zimekwenda na majibu yao yalikuwa ni yale ...

MHE. FRANCIS L. MTEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: ... mapendekezo ya kutaka kuhakikisha kwamba shughuli za kibinadamu pale zinasimama ili kulinda mazingira yale na kulinda hifadhi ambayo tulikuwa nayo kama uchumi wa Taifa letu unavyotegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema hayo. Lakini katika eneo hilo pia si wote wanaondolewa kuna vijiji 15 kama nilivyosema vinabaki na vingine 14 ni baadhi ya vitongoji. Unaweza ukakuta kwenye kijiji kitongoji kimoja na nilitaja vyote na orodha ninayo hapa, wakihitaji tunaweza kuwapa. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Haya Mheshimiwa Mbunge wa Mbarali, naona ulisimama.

MHE. FRANCIS L. MTEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda nitoe taarifa kwa Mheshimiwa Waziri kwamba

10 NOVEMBA, 2022

kwa kweli mpaka sasa hivi wananchi wa Mbarali wana taharuki kubwa sana. Hawana elimu yeyote kwa sababu muda wote wamekuwa wakiishi pale kwa matamko, leo kiongozi huyu anafika anasema endeeleni kufanya shughuli zenu bila wasiwasi, sitaki wananchi wangu mbughudhiwe, kwa hiyo wameendelea na mazoea hayo. Halafu wanakolima sehemu nyingine ni mbali kabisa na mapito ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hawaharibu maji kwa yale mashamba ambayo yapo mbali na mapito ya maji. Halafu pia kuna vijiji ambavyo havina mapito ya maji kabisa, kwa hiyo yamepita mbali mno na yale maji, kama alivyoseme Mheshimiwa Sanga, huwa yanatumika wakati wa masika tu, wakati wa kiangazi hakuna kilimo kinachoendelea kule. Ahsante

MWENYEKITI: Sawa ahsante. Sasa yule alikuwa anatoa taarifa kwa hiyo huwezi kumpa taarifa lakini Mheshimiwa Waziri kaa tu. Ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge, nadhani Mheshimiwa Waziri hapo ametoa maelezo kwamba, vijiji vinaondoka kama vijiji ni vitano, vijiji vingine athari zake ni pengine ni vitongoji au kwingine ni nyumba chache. Na amesema anayo hapo taarifa Mheshimiwa Mbunge unaweza kwenda kuitazama. Pia nimemsikiliza mheshimiwa Waziri mchango wake ameeleza kwamba elimu imeshaanza kutolewa. Maana yake zoezi halijaisha bado.

Kwa hiyo wale watu uliosema Mheshimiwa Mbunge na uko sahihi kwamba hawajapata elimu yeyote ni kweli kwa sababu ndio elimu imeanza kutolewa. Kwa hiyo maana yake, wale wanaoondolewa hawendi tu kuswaga kule kama mifugo. Hapana. Wanapewa elimu

10 NOVEMBA, 2022

kwa nini wanaondoka halafu ndio wataondoka hao ambao watukuwa wameathiriwa.

Kwa hiyo, hiyo taharuki nadhani na wewe utafute namna ya kuwatuliza wale wananchi wakiwa wanasubiri kupewa hiyo elimu ambayo ni mahususi. Nawaona Wabunge mmesimama lakini sasa taarifa siwezi kupewa mie kwa sababu mimi ndio ninaezungumza sasa, kwa hiyo, naomba mkae.

Nilishamtaja Mheshimiwa Waziri wa Madini atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, mtoa hoja ajiandae.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia, lakini niseme tu kwamba hoja, michango na maoni ya Waheshimiwa Wabunge kwenye mpango huu sisi Wizara ya Madini tunayapokea yote na kuahidi kwamba tutakwenda kuyafanyia kazi kwa nguvu zetu zote. Hili linatokana na ukweli kwamba sekta yetu ya madini Waheshimiwa Wabunge hawa wamekuwa walezi wakubwa wa kushauri mahali ambako tunaona hatuendi sawa, wamekuwa wepesi haraka kutufikia na kutuambia turekebishe wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *spirit* hiyo hiyo nataka nikuhakikishie na bila kupoteza muda wa Bunge lako, kwamba maoni yote waliyoyatoa Waheshimiwa Wabunge kwenye mpango huu tunaamini mtoa hoja ameyapokea na sisi Wizara ya Kisekta tumeyapokea na tutayafanyia kazi.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda mmoja tu, la kutoa *comfort* kwa Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba wamesema wengi kwamba GST ipewe mamlaka ya kufanya utafiti wa kina juu ya upatikanaji wa madini hapa nchini. Jambo hili ni la kweli, na hivi karibuni Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi tumefanya marekebisho makubwa kwenye sheria ya madini ambayo sasa imewapa mamlaka GST kufanya utafiti wa kina. Kwa sheria iliyokuwepo huko nyuma ni kwamba GST alikua anakomea kwenye kuchora ramani na kutoa taarifa za awali za madini, lakini uchambuzi na utafiti wa kina GST hakuwa na mamlaka hayo. Marekebisho tulioyafanya juzi hapa sasa yamempa mamlaka GST kufanya utafiti wa kina na kutupa taarifa za kina za madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hilo mtaona tofauti baada ya kuwa sheria imeanza kufanya kazi na Serikali imejipanga. Mheshimiwa Rais, ameshakubali kabisa kwamba ni lazima tufanye utafiti wa kina kwa nchi yetu. Hali tuliyonayo sasa hivi, utafiti tulionao wa ki-jiofizikia wa *high resolution* ni asilimia 16 tu ya nchi yetu. Sasa ni lazima tufanye zaidi angalau tufike asilimia 50-60 ili tujipatie uhakika zaidi wa rasilimali hii kutambua ziko wapi; na hata kama tunapata wawekezaji wanaokuja kwetu basi tuwe na uhakika bila shaka yeyote kuwaambia kwamba tuna hiki na kiko mahali gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni madini mkakati, Waheshimiwa Wabunge wengi wameelezea habari ya madini mkakati. Nataka niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba tumeweka utaratibu mzuri sasa, kwa sababu madini mkakati ndio yanayohitajika dunia kwa ajili ya mabadiliko ya kiteknolojia. Watu wanahama kutoka kwenye matumizi

10 NOVEMBA, 2022

ya mafuta na kwenda kwenye matumizi ya betri. Ni lazima kama Taifa tusibaki nyuma na sisi tuchangamkie hiyo fursa. Mataifa makubwa yanakuja kwetu kutafuta madini hayo, kwa sababu tumerekebisha sheria hii, tutakacho kwenda kufanya sasa ni kuangalia *mapping* ya kujua madini mkakati haya yako wapi. Yametajwa ya aina nyingi na; ndiyo maana mtaona miradi mingi mikubwa ambayo inachimba madini mkakati kama *nickel*. Sasa hivi imeanza kuchimba kule Kabanga lakini na mahali pengine. Madini kama *rare earth elements* tunakamilisha majadiliano na PRG ili madini yale yaanze kuchimbwa. Kule Niobium kwenye eneo la *Panda Hill* na kwenyewe tunakamilisha majadiliano ili madini yaanze kuchimbwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka niseme hayo machache ili Waheshimiwa Wabunge wapate *comfort* kwamba mawazo yao na maoni yao yote kwa pamoja tumeyapokea na nikushukuru sana kwa nafasi hii. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, mtoa hoja ajiandae.

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru Sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo. Kwanza nimpongeze Waziri wa Fedha kwa mpango mzuri aliouleta, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na Serikali ya Awamu ya Sita kwa kujipambanua kusukuma maendeleo ya watu. Nishukuru sana kwenye mpango huu kuna mawazo mazuri na

10 NOVEMBA, 2022

uamuzi wa busara wa Serikali kutumia TEHAMA katika kuboresha huduma mbalimbali zinazotolewa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa ujumla wake hatufurahishi sana na mahusiano yaliopo kati ya watoa huduma za mawasiliano na watumiaji wa huduma za mawasiliano, hakuna mahusiano mazuri. Kumekuwa na mashaka makubwa na kutuhumiana kukubwa sana. Sasa Serikali inachukua hatua zifuatazo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; tunadhani kuna mapungufu kwenye kanuni zinazosimamia huduma zinazowasimamia watoa huduma na watumiaji wa huduma katika kuzipata hizi huduma, na hasa kwenye maeneo ya wajibu wa watoa huduma na wajibu wa watumia huduma. Serikali tumefanya uamuzi wa kuzipitia upya kanuni hizi ili tuone mashimo yako wapi ili mahusiano haya yarekebishwe, huduma za mawasiliano nchini ziboreshwe. Hapa niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge mawazo yenu tumeyachukua na mawazo ya wananchi katika hili tumechukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wananchi wanasema tunapobadilisha bei ya bando kwa nini tunapeleka matangazo kwenye vyombo vya habari badala ya kumpelekea mtumiaji moja kwa moja? Tunadhani hii ni hoja ya msingi kwamba siku moja kabla ya mabadiliko mwananchi apelekewe taarifa moja kwa moja kwenye simu yake afanye uamuzi anaendelea na matumizi ya bando hilo au anabadilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili tunalolifanyia kazi, tunao utaratibu, kila baada ya miaka mitano, kunafanyika tathmini ya gharama halisi za usafirishaji wa

10 NOVEMBA, 2022

data katika huduma ya mawasiliano. Gharama ya mwisho ilifanyika mwaka 2018, tathmini ikatupa *range* ya shilingi mbili mpaka shilingi tisa. Sasa ni miaka mitano tunafanya tathmini hiyo, mwezi wa 12 mwaka huu, tathmini hiyo itakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo unavyoenda, kwa sababu kuna uwekezaji mkubwa umefanyika, kuna hatua zinachukuliwa za kikodi, lakini pia kuna taratibu zinaendelea, kwa hiyo, mwelekeo unavyotupeleka, tunadhani matokeo ya tathmini yatashusha gharama za usafirishaji wa *data* nchini. Kwa hiyo, hayo mambo mawili ya msingi tunayafanyia kazi.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nape, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

T A A R I F A

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Waziri anafanya kazi nzuri, lakini wakati anaendelea, nataka kujua jambo moja; huwa inanisikitisha sana na nimelisema muda mrefu pole pole naona haliendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina shilingi 3,000,000 kwenye benki, mimi ni mchungaji, niko porini kule nachunga; salio limeniishia kwenye simu, nataka kutoa

10 NOVEMBA, 2022

fedha kwenye benki kwa kutumia *sim banking*, wananiambia niweke salio nami sina uwezo wa ku-access hili salio, sina, nimeishiwa; kwa nini benki au hii mitandao wasifanye mawasiliano na mimi ili hela yangu inapokuwa nimeichukua bure, ikatwe kwenye benki? Yaani mimi nina hela kwenye simu, halafu inafia porini! Siwezi kutoa hela kwa sababu sina tu vocha ndani? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sasa Waheshimiwa Wabunge, hiyo ni taarifa au unachangia na wewe una hoja yako mpya kabisa umeileta ambayo haikuwa umeizungumza? Mheshimiwa Waziri naomba utiririke na yale maelezo yako, hii taarifa iweke kando kwanza, kwa sababu inaleta jambo jipya. Ni la msingi, lakini ni jambo jipya. (*Kicheko/Makofi*)

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Hoja ya pili ambayo nilitaka kuichangia hapa, kumekuwa na mjadala kwamba kulikuwa na mtoa huduma ambaye aliamua kubadilisha bei ya *bundle* lake kabla hajabadilisha taarifa kwenye bango lake. Asubuhi nilitoa taarifa hapa kwamba Serikali tumechukua hatua, tumemwita TCRA, bahati nzuri, huyu mtoa huduma amekiri uzembe katika kutekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tumechukua hatua zifuatazo: Moja, tathmini iliyofanyika imeonesha walioathirika na jambo hili ni watu 22,107 walitumia huduma wakati zile taarifa hazijabadilishwa. Baada ya kuling'amua hili, Serikali imemwagiza mtoa huduma: kwanza, awarudishie hawa walioathirika MB zao 200 ambazo walitakiwa wazipate kutokana na bango lake lilivyokuwa; pili, awape MB 300 kila mwathirika kama fidia

10 NOVEMBA, 2022

ya usumbufu alioupata kwa sababu ya uzembe uliofanywa na mtoa huduma; na tatu, tumemtaka mtoa huduma awaombe radhi watumiaji wa huduma hiyo walioathirika kwa kuwatumia ujumbe kwenye simu zao kueleza uzembe alioufanya. Hii itakuwa ni hatua za mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Serikali tunatamani tuone kuna mahusiano mazuri kati ya watoa huduma na wapokeaji wa huduma. Sasa mahusiano haya, moja ya eneo kubwa ambalo ni muhimu tukalipitia na hli ndilo ambalo tumeanza nalo kazi, ni kutengeneza hizi kanuni. Zilizopo tuzipitie, lakini kama iko haja, tutengeneze kanuni nyingine mpya, zi-*regulate* mahusiano haya ili mtoa huduma ajue wajibu wake na mpokea huduma ajue wajibu wake. Tunaamini hili likifanyika, mawasiliano nchini yataboreka na matumizi ya TEHAMA yatakuwa bora na uchumi wetu utaimarika.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chumi, hautoi taarifa, lakini eleza hoja yako kwa sababu muda wake umekwisha.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nilikuwa nasema kwamba haya mahusiano ambayo Mheshimiwa Waziri anayasema baina ya watoa huduma na wapewa huduma,

10 NOVEMBA, 2022

mojawapo ya kipengele ambacho kinaweza kutusaidia sisi ni kwamba, biashara yoyote unapowekeza, unahitaji faida. Sasa kwa mfano, unapopitisha miundombinu katika *road reserve* iwe ya *TARURA* au *TANROADS*, kuna gharama lazima ulipie. Kwa mfano, ukipitisha miundombinu ya maji, kwa kila kilometa moja unatozwa Dola 50; ukipitisha miundombinu ya gesi au *oil* utatozwa Dola 50; ukipitisha miundombinu ya waya kama wa simu, utatozwa Dola mbili, ukipitisha...

MWENYEKITI: Hoja yako ni nini Mheshimiwa? Maana unakuwa kama unachangia.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, ukipitisha *fiber* unatozwa Dola 1,000 kwa kila kilometa moja, matokeo yake ndiyo maana gharama zitaendelea kuwa kubwa. Kwa hiyo, lazima tupunguze hii gharama kama ambavyo tumepunguza kwenye gharama za maji, *TANESCO*, sewage na kadhalika.

MWENYEKITI: Yaani hiyo hoja yako inatokana na jambo gani alilolisema Waziri?

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, inatokana na jambo la kwamba haya mahusiano yasiyokuwa mema kati ya watoa huduma na wanaopewa huduma, yanatokana na gharama kama hizi. Zikipungua gharama kama hizi mahusiano yatakuwa mema.

MWENYEKITI: Haya, ahsante sana.

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Waziri, hii haikuwa taarifa, yeye alikuwa anatoa mchango wake. Kwa hiyo, nafikiri na wenyewe utakuwa umeuchukua kama ulivyochukua michango ya Wabunge.

Kuna hili swali alilouliza Mheshimiwa Getere, ni jambo jipya lakini naamini unalifahamu kwa sababu wananchi wanalizungumza kwamba mtu ana salio kwenye simu yake kwa maana ya kwenye *sim banking*. Yaani kwenye benki yake kuna pesa, na yeye anataka kuingia kule kwenye akaunti yake ili atume pesa hapa na pale na hapa, anaambiwa huna salio, na hilo salio linaloulizwa ni la ule mtandao wa simu anaoutumia. Sasa lile sijajua kama ni la kwako au ni la kwako wewe na Wizara ya Fedha kwa pamoja maana linahusu mabenki pia.

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja ni ya msingi na ninajua ni kero kwa watu wengi, lakini kinachofanyika, watoa huduma karibia wote wameweka huduma ya kukopeshwa salio la kutumia kwenye simu na litakuja kukatwa utakapoongeza salio lako baadaye. Huduma hiyo ikitumika, inaweza kutatua hili tatizo ambalo lipo kwa sababu kinachotokea ni kwamba wanatakiwa uwe na salio kwenye simu yako ili upate huduma. Kama huna salio, na katika mazingira uliyopo pengine huwezi ukaongeza salio, ndiyo maana wametoa *option* ya kuomba kukopeshwa salio kwenye simu yako, ukalitumia kwa muda, utakapoweka salio lile la kununua, lile ulilokopeshwa linachukuliwa.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Lingine ambalo utusaidie, hii ya kusema siku moja kwa maana ya saa 24, kwa kweli zitakuwa hazitutoshi. Wakati

10 NOVEMBA, 2022

mnazungumza nao hao watoa huduma, kwa sababu siyo jambo la kushitukiza, nao wanakuwa wameshalifanyia utafiti na hesabu kwa muda kabla hawajaanza kulifanyia kazi. Kwa hiyo, siku moja haitatosha, maana la sivyo mtu anaweza akatoa hiyo taarifa usiku wa manane halafu kesho yake zoezi likaanza. Kwa hiyo, siku zitolewe za kutosha hapo ili mtu aweze kujiambia, hata kama anataka kuhama mtandao, kama anaona huu ni ghali, ahamie mwingine, apewe nafasi.

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokea. Nilipolieleza hili nilitoa kama mfano. Tunaweza kuweka muda mrefu kwa sababu ni kweli kwamba kubadilika hakufanyiki mara moja, ni *process* ndefu sana. Wanaanza wao, wanaleta *TCRA*, *TCRA* ikishakubali wanatakiwa wamtangazie mtumiaji kabla hawajaanza ku-*implement*. Kwa hiyo, tunaweza tukaweka muda wa kutosha wa kutoa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa hapa ni kwamba taarifa zimfikie mtumiaji, kwa sababu malalamiko ni kwamba taarifa hazimfikii mtumiaji, anajikuta ameshaanza kukatwa wakati hana taarifa. Kwa hiyo, tutaweka muda wa kutosha.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, na mtoa hoja ajiandae.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, ambapo kwa siku hizi

10 NOVEMBA, 2022

nne, kwa mujibu wa kanuni wamekuwa wakichangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wamechangia vizuri sana, na ukweli kiwango cha michango kwa sisi tuliokuwepo hapa Bungeni kwa muda mrefu, tunaona ni mizuri. Pamoja na kwamba wakati mwingine umekuwa ukituvumilia na kuturudisha kwenye mstari, lakini ndiyo tunaendelea kujifunza. Nami nimeona niseme siku ya leo kwa sababu kama Mratibu na Msimamizi wa Shughuli za Serikali humu Bungeni na hoja hii ni ya Serikali, na ni Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/2024 nisitoke bila kusema kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote. Mawazo ni mazuri; na kwa kuwa ulikuwa ni mpango na ni mapendekezo, yale yanayowezekana yatachukuliwa, Waziri wa Fedha yupo, naye atakuja atasema, lakini yatachukuliwa. Yale ambayo yatachukuliwa kwa mipango inayokuja baadaye, tutayachukua kwa muda huo unaokuja kwa mwaka unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu haiko vibaya, na wakati mwingine tunapoisema vibaya, tunajidhalilisha kwa sababu yako mazuri ambayo nchi yetu imefanya. Ukuaji wa uchumi katika *vision 2025*, tulisema tunataka tufike uchumi wa kati, na tumefika kabla ya kufika 2025. Jambo hili ni la kujivunia kabisa. *World Bank* wanatupongeza, *IMF* wanatupongeza, wadau mbalimbali wa maendeleo duniani wanatupongeza, lakini mtu anaweza kusema anavyojua au akafanya tathmini yake, nasema tuitendee haki nchi yetu. (*Makofi*)

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, amefungua milango mikubwa ya uwekezaji, sasa Tanzania inaonekana duniani kote. Kazi nzuri inafanyika, biashara zinaenda vizuri, uhuru upo, uchumi unazidi kuchangamka, pamoja na changamoto za kidunia ambazo zimekumba dunia nzima, lakini Tanzania tuko vizuri. Tulidhibiti mfumuko wa bei, ukawa katika *within* kiwango kinachotakiwa, lakini tukadhibiti pia hata ukuaji wa uchumi, tukawa katika kiwango kinachotakiwa kwa kadiri ya makubaliano. Hilo nalo ni jambo la kujipongeza. Hatujipongezi kabisa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni suala la hali ngumu ya maisha kutokana na majanga yaliyoikumba dunia, hata nchi za wenzetu; Ulaya, America na wenyewe tunaona migomo na sisi wote tunashuhudia na tunaona kwenye *television*, huwezi kusema hapa eti kuna Mbunge haangalii *television*. Unayazungumzia mazingira ya hapa ya ugumu wa maisha kama vile ni tofauti na duniani kote. Hapana, tutende haki kwa nchi yetu. Yako mambo mazuri yanafanyika, Rais wetu anafanya mambo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maendeleo Waheshimiwa Wabunge, tumeji-overdose kwa miaka hii saba na Ilani inayotekelezwa Waheshimiwa Wabunge, ni ya CCM. Kinachofanyika hapa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan anaendeleza utekelezaji wa mipango ile ile ya CCM ambayo imefanyika kwa miaka mitano mathalani, kwa miaka sita tu tumeweza kununua ndege 11. Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kalipia zile zilizokuwa zimebakia mbili, kaongeza tano. Zinakuja saba katika kipindi chake. Tunajenga Reli ya *Standard Gauge*, hatuwezi kumaliza mara moja. Tunaelewa. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine mambo mengine mengi unakuta mtu anatumia nguvu nyingi kweli kweli kuelezea ziko humu. Habari zote zipo kwenye Mapendekezo ya mpango. Sema tu ukurasa fulani, pale kama mlivyosema hivi, nami nasema hivi; lakini ni kama vile hakuna kitu kabisa. Waheshimiwa Wabunge, tutende haki kwa nchi yetu na viongozi wetu. Serikali ya CCM ndiyo inayotekeleza mipango ya maendeleo. Lazima tufahamu kinachofanyika. Kila kitu kimeandikwa hapa, mtu anatakiwa kukisoma tu, anakizungumza tofauti kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo fursa nyingi kama nchi. Kubwa ni kujipanga. Tupange ipi, tuache ipi? Hapa sasa hivi ukizungumzia ardhi, kila mtu kwenye ardhi kuna fursa ya mifugo, kilimo, madini na uhifadhi. Fursa hizi zinagombana. Amesema vizuri sana dada yangu Mheshimiwa Naghenjwa, kwamba fursa zinagombana, sisi Wabunge wenyewe tunaingia kwenye ushabiki wa fursa zinavyogombana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nakubaliana na wale waliosema tuwe na Tume ya Mipango. Lazima tuwe na kitu kinachopanga na ku-set *priorities*. Bila kufanya hivyo, fursa zinapigana na sisi tunapigana, na sisi humu ndani tunakuwa mashabiki wa fursa, hatusemi *priority* ni ipi, matokeo yake nchi ndogo zenye fursa kidogo zitapiga hatua kubwa, wenye fursa nyingi tutabakia tunagombana na fursa zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tumechangia vizuri, tuendeleo na tunawashukuru sana. Sisi kama Serikali ni watumishi tu.

10 NOVEMBA, 2022

Kesho niko hapa, kesho kutwa utakuwa wewe utakaa hapa. Siyo Serikali ya Simbachawene wala Mwigulu, wala siyo ya Mawaziri hapa. Tushirikiane wote, michango yetu iwe ya kujenga ili nchi yetu iweze kusonga mbele. Watanzania wametuumini, wametuweka hapa tufanye kazi kwa niaba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, mtoa hoja, aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Utakumbuka tarehe 7/11/2022 niliwasilisha katika Bunge lako tukufu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti pamoja na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe pamoja, Naibu Spika, Wenyeviti wote wa Bunge, Kamati ya Bunge, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa maoni ambayo wameyatoa. Nasi kama Wizara tumeyapokea. Kama ilivyo kwenye kanuni, lengo la wasilisho hili ni ili tuweze kupokea maoni na kuendelea kuboresha *document* hii ambayo tutaiwasilisha tena na hatua nyingine ziweze kufuata mpaka ambapo tutakuja kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeyapokea maoni haya na Waheshimiwa Wabunge zaidi ya 90 wamechangia katika mjadala huu. Nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri ambao wamekwisha kupokea mapendekezo ambayo

10 NOVEMBA, 2022

yanaangukia katika sekta zao na kufafanua katika baadhi ya maeneo ambayo yalihitaji ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba kanuni za Bunge hili ni kupokea maoni na kama ambavyo wenzangu wametangulia kufafanua katika baadhi ya maeneo, naomba nami nifafanue katika baadhi ya maeneo ambayo yanahitaji ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kubwa ambalo nahitaji kulifafanua ni ile hoja ambayo ilitolewa kuwa Tanzania imeshuka toka uchumi wa kati wa chini na kwenda kwenye kundi la zile nchi masikini. Napenda nitoe ufafanuzi huu kwa sababu hoja hii imekuwa ikipotoshwa mara kwa mara. Kwanza tuna mambo mawili ambayo yanafanana ambayo tunapojadiliana lazima tuwe makini tunapoyaongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kuna nchi inapokuwa imepangwa kwenye kundi fulani la kukua kwa uchumi na kipato cha watu wake; pili, kuna ule uwiano wenyewe wa kukua kwa uchumi katika nchi. Yaani hapa tunaongelea ile *growth rate* na kundi ambako nchi yetu imepangwa. Namaanisha nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipopata COVID katika nchi nyingi takwimu ndogo ndogo ambazo tunazipima kwa majira mafupi mafupi, wengine wanapima kwa muda mfupi zaidi, sisi tunapima kwa robo mwaka. Takwimu ya *growth rate* ndiyo takwimu ambayo imekuwa na namba tofauti tofauti tunazozitoa kwa kila wakati. Yaani kabla ya COVID tulikuwa *around 7%*, baada ya hapo tukashuka mpaka *8%*. Tulipoenda kwenye utekelezaji wa mpango wa kuondokana na UVIKO

10 NOVEMBA, 2022

tumepanda tukaenda 9%; tuliweka *projection* za kurudi tena zaidi ya 5% kabla ya vita vya Ukraine, baada ya athari za vita vya Ukraine, tukarudi kwenye *projection* ya 4.7%. Baada ya kuweka mpango mkakati na bajeti hii tuliyoiweka, matarajio yetu tunaenda kupanda tena kuzidi 5%. Hiyo ni *growth rate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nchi iko kundi gani la kipato, ambayo ndiyo hoja aliyoisema juzi Mheshimiwa Profesa Muhongo, kuna namna mbili za kupima na kupanga nchi katika makundi kulingana na pato la Taifa. Yaani *the key measures for income per capita*. Ya kwanza ni *GDP per capita* na ya pili ni *GNI per capita* ambayo zinaongelea pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Dunia (*World Bank*) haitumii *GDP per capita* kupima kundi nchi ilipo, inatumia *GNI*. Katika taarifa zake zote ambazo imekuwa ikitumia Benki ya Dunia huwa inatoa takwimu hizo za *GNI per capita* kwa nchi kila Julai mosi, kila mwezi wa Saba wa mwaka na takwimu zinazokuwa zimetolewa ni zile za mwaka uliopita. Kwa maana Julai Mosi, 2022 ilitoa makundi ya nchi kwa mwaka 2021, tarehe Julai Mosi, 2021 ilitoa makundi ya mwaka 2020 na tarehe Julai Mosi, 2020 ilitoa makundi ya nchi kwenye vipato vyao kwa mwaka 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo hiki alichokisema Profesa Muhongo kwamba tumeshuka mwaka 2022, tathmini hiyo hata haijafanyika, takwimu hiyo itatolewa Julai Mosi, 2023. Kwa maana hiyo zile takwimu alizozitoa sizo na zile ambazo zilishatolewa mpaka sasa ambazo zinaongelea kwa mwaka uliopita, zilizotolewa kwa mwaka huu zinaonesha Tanzania bado

10 NOVEMBA, 2022

tuko kwenye dola 1,140 ambayo tumeshapiga hatua kubwa sana tangu pale tulipokuwa tumepanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho niliona nikiseme, ni kwamba ile nukuu aliyosema imetoka Benki ya Dunia, mimi kwa kuwa Waziri wa Fedha nakuwa Gavana wa Benki ya Dunia. Kwenye *internal memo* ya Benki ya Dunia waliandika kusikitishwa nanukuu ile ambayo ilinukuliwa ikionesha imetoka Benki ya Dunia kama ninavyoweza kusoma hapa. Alisema:

“Honorable Minister we have learned with a shock that it was said Tanzanians GDP per Capita is now 990, trying to make the public of Tanzania to believe that Tanzania has slipped to lower income countries. That was referred that Tanzania is now GDP per Capita range to 990 USD.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakaitaja ile website ambayo ni *trading economies.com* wameiweka hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema; *“It appears to be incorrect as the figures does not confirm. In any case GDP per Capita is not what we use in income classification. Besides the number they have given does not appear to be consistence. This is not from the World Bank. Please note that, some countries have slipped from middle income to lower income but Tanzania has maintained its status since becoming lower middle-income country in 2020. Please note World Bank does not GDP per Capita for income classification and this articles which was refereed is incorrect and is not from the World Bank. (Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi kwa mujibu wa taarifa hizo Benki ya Dunia haijatoa hizo takwimu na Benki ya Dunia wakati tuko kwenye vikao vilivyoisha tu vya juzi mwezi huu uliopita. Benki ya Dunia wakati wanahutubia Mawaziri wa *Caucus* ya huko Afrika, waliwatuma Mawaziri wengine waulize Tanzania imefanyaje kuweza *ku-maintain status* na kuendelea kukua zaidi na kauli hiyo ilitolewa na Rais wa Benki ya Dunia na ikatolewa na Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia. Ni siku hizo hizo tu wasingeweza kuipongeza Tanzania na wakasema tumfikishie salamu hizo Mheshimiwa Rais na wakati ule ule pato la Tanzania liwe limeshuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama kuna watu ambao wanasubiri sana Tanzania ishuke kutoka uchumi wa kati kwenda wa chini, niwahakikishie wanapoteza muda wao, Tanzania haitashuka kwenda kwenye kipato cha chini, inasonga mbele. Itatoka kwenye uchumi wa kipato cha chini kwenda kipato cha kati cha juu. Hii si kwa maneno ni kwa hatua ambazo Mheshimiwa Rais na Serikali anayoongoza inachukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba zinaongea, huwezi kwenye nchi ambayo unajenga bwawa kubwa la umeme kwa ajili ya *grid stabilization* utegemee ukishamaliza mradi huo eti ushuke kutoka pale ulipokuwa uende chini. Huwezi kwenye nchi ambayo unaboresha bandari kwa ajili ya kufungua shughuli kubwa kubwa kwenye lango la nchi ambazo hazina huduma ya maji, ukishamaliza miradi hiyo eti uchumi wako ushuke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kwenye nchi ambayo imeweka bajeti kubwa kwenye historia

10 NOVEMBA, 2022

inayokwenda kwenye shughuli za uzalishaji, bajeti ya kilimo inaenda kwenye umwagiliaji, haya si maneno ni *scheme* ambazo zitaonekana na watu watazalisha na ambao ndio wengi katika Taifa hili. Huwezi ukamaliza kujenga *irrigation schemes* ukaondoka kwenye kutegemea mvua ukaenda kulima kwenye uhakika kwa kutumia mbegu bora, halafu ukishamaliza hapo *GNI* yako na kipato na *position* ya nchi yako iweze kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi hiyo hiyo, huwezi ukaendelea kuboresha viwanda, mashamba kama ya Mkulazi, Mbigili, Bagamoyo *Sugar* ambayo na sukari za kwanza zimeshaanza kutokea ni miradi mikubwa mikubwa, ujenzi wa reli ya kisasa ambayo itafungua uchumi na ni uti wa mgongo wa uchumi, halafu ukishamaliza kuijenga tu nchi ishuke pale ilipokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi ukatekeleza mradi mkubwa kama wa *LNG injection* yake ni ya *billions, trillions*, halafu ukishamaliza kuutekeleza na uka-*take off* ajira zitakazotengenezwa pia na *production* zitakazofanyika halafu baada ya hapo nchi hiyo ishuke kwenye nafasi ilipokuwa iende upande wa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji unaofanyika kwenye elimu, miundombinu ya barabara kutoka kwenye uzalishaji, nyie Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwa Wabunge ambao wameshaka zaidi ya kipindi kimoja watasema. Fedha zilizokwenda kwenye *TARURA* kufungua barabara kutoka kwenye uzalishaji kwenda kwenye *feeder roads* ni nyingi kuliko katika kipindi chochote kile cha historia. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika sekta nyingine, kwa mfano, imenunuliwa mitambo kwa ajili ya kuchimba mabwawa. Mabwawa yale yatanusuru mifugo iliyokuwa inakufa. Watu mifugo yao ikanusuriwa wakaanza kufuga kisasa, hawawezi wakarudi nyuma, wale watu watasonga mbele. Hivyo hivyo mitambo ile itaenda kutengeneza schemes ndogo ndogo ambazo zitaenda kuongeza uzalishaji katika maeneo husika. mazingira bora ya uwekezaji na kuvutia mitaji kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameifanya na wawekezaji wanatiririka, yatatengeneza ajira, tutapunguza *unemployment*, hao watu wote wataenda kuwa na vipato vyao. Watu wengi wa aina hiyo wakishakuwa na vipato vyao nchi haiwezi ikashuka ilipokuwa kwenye daraja lile kwenda chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona niliseme lile na niwaombe Watanzania kama ambavyo *Chief Whip* amesema hapa. Ni vyema tukaipenda nchi yetu na wala tusichanganye, mambo mengine ni ya kitaalam. Kwa mfano, kuna watu wana...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri dakika tatu, malizia kengele ya pili imeshagonga.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati watu wanachanganya *cost of living* na *standard of living* na kipato nchi ilipo. Haya mambo ukilinganisha nchi na nchi utaweka *phenomenon* nyingi za kiuchumi, ni lazima ukitaka kulinganisha sawasawa uweke na *purchasing power* kwa sababu zile

10 NOVEMBA, 2022

exchange rate za nchi na nchi zinatofautiana. Mtu anaweza akawa analipwa vizuri sana, ana kipato kizuri sana, kama eneo alipo na yule mwingine aliko bei za bidhaa zinaenda tofauti yule pamoja na kuwa kipato kikubwa yeye atakuwa na maisha magumu kuliko yule mwingine ambaye huenda ana kipato kidogo, lakini bei zake ziko tofauti. Kwa hiyo haya mambo lazima mara zote tuwe tunafahamu undani wake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine walisema ukomo wa deni la Taifa. Wanasema Bunge labda liwe linaweka ukomo wa kukopa. Hata sasa Bunge limeweka ukomo wa kukopa, kwa sababu nchi yetu kila mkopo tunakopa kwa mradi na kila mradi tunapitisha kwa bajeti. Hakuna sehemu ambako tunakopa bila mradi na hakuna sehemu tunakopa bila bajeti. Tumeweka kwenye kila mwaka ukomo wa kukopa ndani, kukopa nje, misaada, makusanyo, hivyo ndivyo bajeti inavyokuwa. Kwa maana hiyo hakuna siku ambako inaenda inakopwa holela tu kwamba ni *open cheque*, haijawahi kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo yote inakopwa kwa mradi, na busara inayotumika ni kupeleka kwenye miradi ambayo italeti tija kubwa, itafungua uchumi. Fedha zote hizo zinazokopwa zinakwenda kwenye uwekezaji. Wengine wakiona mkopo umetajwa labda dola bilioni mbili labda trilioni nne inakuwa *program* labda na *multilateral* ambayo inachukua si mwaka mmoja na fedha hizo huwa zinakwenda kwenye mradi mahususi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wengine wanaangalia mradi ni endelevu, wanadhani kama mradi ni endelevu deni litabaki lilelile. Hebu niambieni kama fedha ya kwanza iliyoingia ilikuwa ya *lot one* hivi tunaweza; *lot one*

10 NOVEMBA, 2022

imeishia Morogoro, hivi tunaweza tukafika mpaka Mwanza sasa deni likabaki lilelile la *lot* iliyokuwa imeishia Morogoro? Haiwezekani! *You can't eat the cake and have it.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema unataka ukusanye kamoja kamoja ndio upeleke kwenye *lot* ukaimalizie utachukua miaka 100 mpaka 120, ni mkandarasi gani atakayekusubiria tu ukusanye kila mwezi umpelekee? Tunachukua cha jumla tunatekeleza mradi uishe haraka ili tuweze kurejesha pale tulipochukua na hizo ndizo tathmini za kitaalam zinazofanywa kuweza kupima kwamba huyu anaweza akakopesheka. Nchi zozote ambazo zinakua ndizo ambazo madeni yao yanakua. Chukueni tathmini si vizuri kutaja sana nchi, chukueni nchi zile mnazozifahamu ambazo hazina uchumi kabisa muangalie kama zina deni. Maskini yeyote hadaiwi, anadaiwa atalipa kitu gani? Ukiona nchi inayodaiwa sana ni nchi inayokua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi mwekezaji yeyote, mtoa fedha yeyote anaiangalia Tanzania kwa sababu wale wengine hawana cha kuwalipa, ndio maana unaweza ukaona hata miradi inagombaniwa. Hiyo tunatakiwa tuone kwamba tuna fursa kubwa na hizi fursa zitafungua uchumi, zitafungua ajira ili tuweze kuhakikisha kwamba tunajenga nchi yetu na Watanzania wanapata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa tunawaza kila wakati, kuangalia na hilo ndio tatizo kubwa sana...

MWENYEKITI: Malizia Mheshimiwa Waziri.

10 NOVEMBA, 2022

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa leo tulikuwa tunapokea tu maoni, niwahakikishie yote tumeyapokea, Dira ya Taifa mpya, kazi inaendelea kuiandaa na inaandaliwa ikiwa na mwendelezo wa hii itakayokuwa imeisha. Miradi ya *EPC+F* imefanyiwa tathmini na tunaelekeza nguvu kubwa kwenye *PPP* kama nilivyosema kuweza kuhakikisha kwamba maeneo ambayo *Private Sector* inaweza ikashiriki kikamilifu *Private Sector* ipewe fursa ishiriki kikamilifu ili iweze kutengeneza ajira kwa vijana wetu na kuweza kuongeza kipato kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naomba sasa kutoa hoja na nirejee kauli ya mwanzo ambayo niliwasilisha kwamba nimewasilisha maandalizi ya Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2023/2024 na Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti pamoja na Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ngazi hii hatoi hoja Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri subiri kidogo hapo nakuletea maneno ya kusema. Anatakiwa kusema maneno yaliyo kwenye kanuni ya 113, washa kisemeo.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Serikali imepokea Maoni na Ushauri wa Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 113(5)(c).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mambo mawili kabla hatujatoka kwenye Kamati yetu ya Mpango.

Mtakumbuka hapa baada ya mchango wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati nikawa nimesema kwa ufupi zile tarehe alizosisema, kwa sababu nilisema hoja kubwa ni kwamba, wananchi wanachanganyikiwa wanaposikia tarehe nyingi ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nilikuwa nimesema kadri yeye alivyokuwa amesema kwamba, usafirishaji wa umeme yaani ile mitambo ama mfumo wa kusafirisha umeme kutoka Bwawa la Nyerere mpaka Chalinze alisema kwamba itaisha Juni, 2023 kwa maana ya mwaka huu wa fedha. Halafu pia alikuwa amesema kwamba sasa Bwawa la Nyerere kule ule ujenzi unakamilika Oktoba, 2023. Sasa ameleta hapa karatasi anataka kurekebisha hizo tarehe. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilipokaa nimeambiwa nilisema Oktoba lakini nilidhamiria kusema Mkataba wa Ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere uliongezewa mwaka mmoja utaisha Juni, 2023. Kwa sababu mara ya kwanza ulitakiwa kuisha Juni, 2022, kwa hiyo mwaka mmoja niliodhamiria kusema uliongezwa ni Juni, 2022 mpaka Juni, 2023.

MWENYEKITI: Sawa sisi kama Bunge hili wawakilishi wa wananchi ndio swali lilikuwepo hapo. Ni Juni, 2023 mradi unakwisha ama ni 2024?

10 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba wetu wa awali ulikuwa unaisha Juni, 2022. Mkandarasi na sisi tukakubaliana kuongeza mwaka mmoja kwa sababu Juni, 2022 mkataba ulikuwa haujaisha, kwa hiyo tukaongeza miezi 12 mpaka Juni, 2023. Hata hivyo, mkandarasi ameleta *schedules of work* inayoonyesha anaweza kumaliza 2024 na sio kwenye muda wa mwaka mmoja tuliokubaliana kuongeza. Kwa hiyo nikizungumza kwa mujibu wa *extension of time* ya kimkataba ni Juni, 2023.

MWENYEKITI: Ukizungumza hapa Bungeni unazungumza na Wabunge na unazungumza na umma wa Watanzania. Mradi wao wa umeme wa Bwawa la Nyerere unakwisha lini Mheshimiwa Naibu Waziri?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mkataba wa nyongeza tulioongeza utaisha Juni, 2023.

MWENYEKITI: Sawa nilikuwa nakuuliza hivyo kwa sababu huwa nasema siku zote Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri ni kazi yenu kumsikiliza Rais anapozungumza kila mahali. Rais alisema 2024, Bunge linaambiwa 2023. Sasa sijui mtarejea tena Bungeni kusema tumewapa tena mkataba, kwa hiyo unaenda 2024 au mtasemaje? Yaani kwa mfano, Serikali sasa hivi inapata kigugumizi gani kwamba Bwawa la Nyerere kwa namna mazungumzo yanavyokwenda tutamaliza 2024. Mkimaliza 2023 hewala, mkamaliza 2024 wananchi tunajua ni 2024. Mkituambia 2023 tunasimama hapo, mkituambia mnaongeza tena huyu mtu mbona mnakuwa mnamwongeza kila saa. *(Makofi)*

10 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU: Mheshimiwa Spika na Mwenyekiti wa kikao cha Kamati ya Mipango ya Bunge Zima, jambo hili ni la kimkataba. Wewe ni Mwanasheria mkubwa, masuala ya mikataba na mambo mengine yanayoweza kujitokeza hapo katikati huwa yanawekwa kama sehemu ya mkataba. Kwamba kunaweza kukajitokeza jambo ambalo sio la kawaida, mathalani ilitokea Covid hapa uagizaji wa baadhi ya vipuri ukawa ni mgumu. Leo tumefika tulipofika asilimia za utekelezaji wa mradi zinasomeka vizuri, lakini Mheshimiwa Rais alitoa tamko hilo kwamba mradi huu utakamilika *by 2024*. Juzi Mheshimiwa Rais amekutana na Rais wa Misri, sidhani kama kuna maudhui mengine walizungumza pale kama walizungumza mambo matatu mojawapo lazima ni mradi ule kulikuwa na ukubwa na uzito wake na waliongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujajua mpaka sasa wameongea kitu gani, kwa hiyo tunaomba, Bunge, lichukue taarifa hii kwa tahadhari huku tuingojea Serikali kuja kutoa tamko rasmi kwamba ni lini mradi huu utakamilika.

MWENYEKITI: Nakubaliana na wewe Mheshimiwa Waziri, hoja ni kwamba tarehe zinavyotolewa tofauti tofauti, wananchi na Bunge linakuwa halielewi, mngokuwa na tarehe moja ingeeleweka. Sasa ukitutajia ya mkataba ya huku kwingine huo mkataba sisi hatujaitisha hapa kwanza kuusoma, ni ninyi ndio mnatuambia na sisi tunawasikiliza ninyi. Kwa hiyo hata hii tunawasilikiza ninyi pia, isipokuwa tunataka uhakika wa hicho mnachokisema. Pia tunatamani kutokea kwenu

10 NOVEMBA, 2022

mngekuwa na tarehe, pengine siyo tarehe kwa maana ya tarehe 2, lakini mngekuwa hata na huo mwaka basi muwe nao mmoja. Mkitaja miwili tunakuwa tunasubiri, halafu tena mnakuja na maelezo mengine ndio hoja ya msingi.

Waheshimiwa Wabunge Kamati yetu ya Mipango tumemaliza, kwa hiyo tunaelekea sasa kwenye utaratibu wetu mwingine. Katibu!

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Mipango imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae!

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa taratibu zetu tumemaliza kazi ambayo tumepewa na Katiba yetu ya kujadili hiki ambacho tumejadili. Serikali imeleta mapendekezo ya Mpango na sisi tumetoa maoni yetu, nayo watayatilia maanani kama mlivyosikia, wameyasikia yote na wameyachukua yote yale ambayo wataweza kuyafanyia kazi, katika Mpango huu unaofuata sasa ambao kikanuni wataleta tarehe 11 Machi, ama siku baada ya hapo ikiwa itaangukia sikukuu au wakati wa siku za mapumziko, wataleta yakiwa na mawazo yenu.

Waheshimiwa Wabunge, haya tunayosema wataleta na mawazo yenu, ngazi hii Bunge lilikuwa linaishauri Serikali, kwa hivyo Serikali inaweza ikachukua

10 NOVEMBA, 2022

ushauri wetu ama mwingine isichukue. Sasa isije ikaonekana kwamba kila ambacho Mbunge amesema humu ndani atarajie atakikuta kwenye Mpango, hapana. Sasa hivi tulikuwa tunatoa ushauri na ushauri kikatiba kwa ngazi hii Serikali inao uhuru wa kukubali au kuukataa. Sasa wakiukataa tutakutana nao kwenye ule mzunguko wa kuisimamia Serikali kwamba tulisema hivi, hamkusikia mlifanya hivi na mambo kama hayo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo kwa ngazi hii tumeshamaliza kazi yetu ya kuishauri Serikali na wao wataenda sasa watengeneze na wataleta kwetu tena mapendekezo kwa sababu kwa sasa ulikuwa unaitwa mwongozo wa mapendekezo.

Mheshimiwa Waziri tunakupongeza wewe na Naibu Waziri na watendaji wote kwenye Wizara ya Fedha, kwa kufikia hii sehemu mliyofikia na pia kwa Serikali nzima kwa sababu Mpango huu ama mapendekezo haya ni ya sekta zote kwenye nchi yetu. Kwa hiyo tunawatakiwa kila la heri mnapoenda sasa kutazama maoni mliyopewa na Waheshimiwa Wabunge na yale ambayo mtaenda kufanya utafiti zaidi ili kutayarisha huo Mpango.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo hapa kutoka kwa Katibu wa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi, mnatangaziwa kwamba mara baada ya kuhairisha shughuli za Bunge mnatakiwa kwenda Ukumbi wa Msekwa Wabunge wote wa Chama Cha Mapinduzi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo na kwa sababu sasa Bunge ndio tunaweza kutoa maelekezo pale chini, huwezi kutoa maelekezo wakati wa Kamati. Mheshimiwa Waziri Simbachawene alieleza hapo

10 NOVEMBA, 2022

kwamba, Serikali ipewe muda ili itoe taarifa, sio lazima ije itolee humu ndani lakini itoe taarifa kwamba, ule mradi pamoja na hizo asilimia zilizofikiwa wa Bwawa la Nyerere tarehe ni ipi hasa. Sasa kwa sababu tulishapata fursa tukiwa Bunge na sio Kamati tulipata fursa ya kumsikiliza Waziri wa Nishati wakati huo akieleza kwa kirefu kuhusu kwa nini mradi huu umechelewa ama umesogea muda mbele.

Waheshimiwa Wabunge, tulishamsikia pia Mheshimiwa Rais akieleza kuhusu 2024 na ili tusipeleke ujumbe ambao una tarehe zenye kuchanganya au miaka yenye kuchanganya Serikali itatoa ufafanuzi kuhusu jambo hilo. Kama watakuwa tayari pengine kesho, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anatoa hoja ya kuhitimisha Bunge anaweza akasemea hilo, lakini kama litakuwa bado linahitaji muda zaidi na Bunge hili linahitimishwa kesho, basi Serikali itatafuta namna ambayo itatoa hiyo taarifa kuhusu jambo hilo. Kama kutakuwa na sababu basi taarifa itakuja kutolewa Bungeni wakati tutakapokutana tena.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 2.24 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 11 Novemba, 2022, Saa Tatu Asubuhi)*